**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 18 Julai, 2007**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI**:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 234

**Ubovu wa Barabara Jimboni Ubungo**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza :

Kwa kuwa, katika miaka ya 1970 barabara nyingi za Kata ya Manzese, Makurumula, Mburahati, Mabibo na Sinza zilikuwa zimetengenezwa kwa kiwango cha lami, na Barabara hizo ni za udongo na ziko katika hali mbaya:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuandaa mpango kabambe wa kutengeneza Barabara za Miji Mkuu kwa kiwango cha lami?

(b) Je, katika miaka mitano ijayo, Serikali inakusudia kutengeneza Barabara ngapi katika Jimbo la Ubungo?

(c) Je, Barabara ya Kawawa, Kigogo, Maziwa hadi External na Ubungo itatengenezwa lini kwa kiwango cha lami na itawekwa lini chini ya usimamizi wa mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango kabambe wa kutengeneza Barabara za Miji Mikuu kwa kiwango cha lami kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Katika Mkutano wa sita wa Bunge lako Tukufu tarehe 06/07/2006, wakati najibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi Mbunge wa Musoma Mjini nilieleza nia ya Serikali ya kuboresha Barabara za Miji na Manispaa. Katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka huu wa fedha, 2007/2008 Ofisi yangu imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa Halmashauri za Manispaa tano kwa ajili ya kutengeneza Barabara za lami kwa kilometa moja na nusu kwa mwaka. Halmshauri za Manispaa hizo ni Sumbawanga, Musoma, Songea, Mtwara na Kigoma ambazo zitapata shilingi milioni 300 kila moja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alipowasilisha hoja yake hapa Bungeni tarehe 11/07/2007 alifafanua mpango uliopo sasa. Kwa kushirikiana na Taasisi ya ushirikiano ya Japan *(JICA)* Serikali imetayarisha mpango kabambe wa kisera na Maendeleo ya usafiri (*Urban Transport Policy and System Development Master Plan for the City of Dar es Salaam*).

Aidha, katika kutekeleza mpango wa usafiri wa mabasi yaendayo kasi *(Dar Bus Rapid Transit (DART),* Barabara zitakazohusika zitahitaji kupanuliwa na kuboreshwa. Kazi hiyo, inatarajia kuanza mwaka huu wa fedha, 2007/2008.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a), Serikali inayo mipango thabiti ya kuboresha Miundombinu ya Barabara. Mipango na vipaumbele vya kuboresha Barabara hupangwa na Halmashauri husika. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inao mpango wa matumizi ya muda wa kati (2007/2008 – 2009/2010). Mpango huu umeainisha shughuli mbalimbali zitakazotekelezwa katika Halmashauri ya Konondoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jimbo la Ubungo, Serikali inakusudia kuzitengeneza Barabara za Mbezi – Mbopo (km 14.6), Goba – Msumi (km 5.4) na Madale – Kisauke (km 6.7) angalau kwa kiwango cha changarawe kwa kuanzia. Barabara nyingine ni Chuo Kikuu – Changanyikeni na *Wazo Hill/*Tangi Bovu – Goba – Mbezi – Kifulumsinga – Kinyerezi hadi Majumba Sita.

Aidha, Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya sehemu korofi (*Sport Improvement*), matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenances*) na matengenezo ya sehemu fupifupi zenye matatizo (*sport Improvement*) ili kuruhusu Barabara zipitike muda wote hata baada ya miaka mitano aliyoizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inakusudia kuijenga barabara ya Kawawa – Kigogo – Ubungo Maziwa (km 4.8) kwa kiwango cha lami. Katika Mpango wa mwaka 2006/2007, Serikali iliifanyia matengenezo Barabara hiyo kwa kuchonga kwa greda na kuweka vifusi kwenye sehemu korofi ili iweze kupitika wakati ikisubiri ukarabati mkubwa.

Aidha, katika mpango uliopo wa kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam, Barabara hii ni mojawapo ya Barabara zilizoainishwa na kuwasilishwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ili ifanyiwe ukarabati na ikiwezekana itengenezwe hadi kiwango cha lami na iwe chini ya uangalizi wa *TANROADS* mkoa wa Dar es Salaam.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri sana inaelekea kazi hizo zikitekelezwa Jiji la Dar es Salaama litatakata.Ninaomba tu ufafanuzi kidogo juu ya Barabara inayotoka *Mbezi Beach* kwenda Mbezi Louise ambayo tuliahidiwa kwamba ingetengenezwa kwa kiwango cha lami ni lini sasa kazi hiyo itafanyika? Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Katika Bunge lako Tukufu nakuambuka nilimjibu Mheshimiwa Charles N. Keenja, kwamba Barabara hiyo ya *Mbezi Beach* itafanyiwa *designing* na usanifu ili iweze kutangenezwa kwa kiwango cha lami. Sasa hivi Barabara hiyo inafanyiwa usanifu pamoja na *designing* ili baadaye zipangwe fedha za kuhakikisha kwamba Barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Sasa tuhamie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, swali linaulizwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 235

**Vyombo vya Usafiri – Shule za Sekondari**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, vyombo vya usafiri ni muhimu sana kwa shule za Sekondari hapa nchini. Je, Serikali imezipatia shule ngapi za Sekondari za Kata magari hadi sasa kwa lengo la kupunguza tatizo la usafiri katika shule hizo, zikiwemo shule za Godegode, Matomondo, Kimagai, Vinghawe, Mazae, Mwanakianga, Mima, Berege, Ihala, Chunyu,

na shule za Sekondari za Tarafa ya Kibakwe na Rudi ambazo ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli vyombo vya usafiri ni muhimu sana katika shue za Sekondari hapa nchini. Kwa sasa Serikali haijaweza kutoa gari kwa ajili ya shule za sekondari za Kata, lakini imeweza kutoa angalau gari moja kila mkoa ili liweze kutumika katika Shule za Sekondari za Mkoa huo.

Hata hivyo, Wilaya ya Mpwapwa ina shule mbili zenye gari ambazo ni shule ya Sekondari ya Mpwapwa na Wota ambayo yanaweza kutumiwa pia na shule za jirani. Serikali itaendelea kununua magari kwa ajili ya shule za sekondari kadri upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nina swali la nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa shule nilizozitaja ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya na kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema Shule za Sekondari Mpwapwa na Wota wana magari. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anafaahamu kwamba gari la Shule ya Sekondari ya Mpwapwa lina zaidi ya miaka 20 halifanyi kazi. Je, uko tayari kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa gari hilo?

Pili, kwa kuwa Walimu wanaofundisha Shule za Sekondari wako mbali na Makao Makuu ya Wilaya na kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana ya kukosa usafiri. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwakopesha vyombo vya Usafiri angalau pikipiki ili kuwawezesha wafike Makao Makuu ya Wilaya kufuata mishahara yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)** :

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba gari hilo bovu naomba litolewe taarifa Wizarani Mkuu wa Shule anafahamu utaratibu na Idara husika italifanyia matengenezo kama pesa zipo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili. Tunatambua kwamba idadi kubwa ya walimu wako mbali na Makao Makuu na kwamba tatizo la usafiri ni kubwa, kutokana na ufinyu wa Bajeti sitaweza kuahidi hapa kwa niaba ya Serikali au Wizara kwamba tutawakopesha. Isipokuwa walimu wanacho chombo chao ambacho ni *SACCOS* na wataweza kukopa pale kwa kujipunguzia adha na kero. Hadi hapo Serikali itakapokuwa na fedha za kutosha tutapenda kuwaondolea walimu wetu kero kadri tutakavyojaaliwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maelezo ya ziada kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niongezee kwa yale majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kufuatana na swali la nyongeza la Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Walimu wa Shule za Sekondari wana utaratibu wa kukopa fedha kwa hiyo Wizara huwa inawadhamini. Kwa hiyo, wanaweza kukopa Benki ya *NMB* tuna utaratibu huo ambao wanaweza kukopa kama wana shida ya kununua vifaa vya usafiri pamoja na matumizi ya *SACCOS* kama alivyosema.

Lakini pia nadhani tuchukue suala la Mheshimiwa Mbunge tulifanyie kazi tuone kama inawezekana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Devotha M. Likokola nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA :** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri na Waziri wameyatoa juu ya masuala ya usafiri katika Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shule ya Sekondari ya wavulana ya Songea Boys ina matatizo ya usafiri kwa muda mrefu sana na wamekuwa wakipata ahadi mbalimbali za viongozi wa Serikali juu ya suala la gari na ahadi hiyo haijawahi kutekelezwa. Je, Serikali sasa hivi iko tayari kutekeleza ahadi ambayo imetoa kwa Songea Boys juu ya usafiri?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota M. Likokola kama ifuatavyo. Awali ya yote nampongeza kwa kuwa karibu sana na ufuatiliaji wake katika masuala ya elimu naomba nipokee taarifa hiyo, nitafuatilia ahadi hiyo na tutaona ni namna gani tunaweza tukatekeleza ahadi hiyo kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunahamia sasa Wizara ya Maji na swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Masasi Mheshimiwa Alfonce Raynald Mrope.

Na. 236

**Utekelezaji wa Mradi wa Maji Mbwinji**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza: -

Kwa kuwa, utekelezaji wa mradi wa maji Mbwinji uliokusudiwa kuupatia Mji wa Masasi maji safi na salama kwa ufadhili wa Serikali ya China umeshindikana, na badala yake Serikali ikaahidi kuutekeleza mradi huo kupitia ufadhili wa Benki ya Kiarabu *BADEA:*

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu kuchelewa sana kwa utekelezaji wa miradi huo, hasa ikitiliwa maanani kuwa, Serikali ya awamu ya tatu ilitoa taarifa kwamba, fedha zilikuwa zimepatikana toka Serikali ya China na kwamba Mradi ungeanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2005?

(b) Kwa kuwa, upembuzi yakinifu ulikuwa umekamilika mwaka 2005. Je, kuna matumaini gani sasa ya kuanza kujenga na kukamilisha mradi huo kwa kutumia fedha za *BADEA?*

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na kupunguza tatizo kubwa la maji katika Mji wa Masasi na Vitongoji vyake, wakati wakisubiri kukamilishwa kwa mradi wa Mbwinji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Jimbo la Masasi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 mradi wa maji Mbwinji ulikuwa ni miongoni mwa miradi iliyoombewa fedha kutoka Serikali ya China. Ombi hilo halikufanikiwa. Kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi huo kumetokana na mahitaji makubwa ya fedha

ikilinganishwa na uwezo mdogo wa Bajeti Serikali. Imekadiriwa kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 34.5 zinahitajika.

(b) Mhesehimiwa Spika, ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo mwezi Juni, 2006 Serikali ilituma maombi ya fedha kwenye Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi.

Hivyo, Wizara yangu bado inasubiri majibu ya *BADEA* ili kujua kama benki imekubali kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huo. Mawasiliano ya mara ya mwisho kati ya Wizara yangu na *BADEA* yalifanyika tarehe 20 Juni, 2007. Hadi sasa majibu hayajapatikana hivyo fedha za kuanza kujenga mradi bado hazijapatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imechukua hatua zifuatazo ili kupunguza tatizo la maji katika mji wa Masasi na Vitongoji vyake:-

(i) Mwaka 2005/2006, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilitumia Shilingi milioni 4.8 kuchimba kisima kifupi na kufunga pampu ya mkono katika Sekondari ya Mtapika. Katika Sekondari ya Wasichana Masasi, kiasi cha Shilingi milioni 1.5 kilitumika kukamilisha ujenzi wa kisima kifupi na kufunga pampu ya mkono. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 23 kilitumika katika kuchimba kisima kirefu na kufunga pampu inayotumia umeme kusukuma maji yaani (*submersible pump*) kwa ajili ya Hospitali ya Mkomaindo.

(ii) Katika mwaka wa Fedha 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imetoa Shilingi milioni 14.9 kwa ajili ya kununua pampu 2 za visima vya Magumuchila, pampu 1 imenunuliwa na nyingine imeagizwa. Shilingi milioni 17.6 zimetengwa ili kukarabati miundombinu ya maji katika mtandao wa mabomba uliopo. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 316.79 zimepelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa ajili ya miradi midogo midogo yaani (*quickwins*).

(iii) Wakati Serikali inaendelea kusubiri majibu kutoka *BADEA* katika Mwaka wa fedha 2007/2008, mji wa Masasi umetengewa shilingi milioni 346.6 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji ikiwa ni pamoja na mtandao wa mabomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alfonce R. Mrope, swali la nyongeza.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kuhusu suala la msaada kutoka China au huo wa kutoka Benki ya Kiarabu ya *BADEA,* hata Waziri wewe mwenyewe umeonyesha kwamba umekata tamaa. Sasa kama yeye amekata tamaa kwamba fedha hizi hazijapatikana bado nauliza kwamba Serikali inasema nini ? inatoa matumaini gani kwa mradi huu mkubwa ambao kwa kweli bila kutekeleza mradi huu Masasi na Nachingwe zitapata shida sana sana ya maji.

Pili, kwa kuwa Waziri wa Maji Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa alitembelea mwezi Aprili Wilaya ya Masasi na tukampeleka kwenye chanzo kimoja cha maji ya kuaminika sehemu za Mwena na kule tuliarifiwa kwamba yale maji yanaweza kutosheleza kwa kiasi cha *Quebec litre 1500* kwenda Masasi. Lakini kwa bahati mbaya miundombinu …

**SPIKA:** Mheshimiwa swali tafadhali.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Ndiyo! Sasa kwa kuwa kuwa Miundombinu ile ni chakavu namuuliza Waziri ana mpango gani wa kuweza kutengeneza hii miundombinu ili Wilaya ya Masasi walau ipatiwe zaidi ya nusu ya maji inayohitaji kwa sababu sasa hivi inapata Quebec litre 500 ambazo hazitoshelezi hata kidogo?

**SPIKA:** Natumaini majibu yenyewe yatakuwa ni mafupi tu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Alfonce Raynald Mrope kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nimhakikishie kwamba mimi mwenyewe na Serikali bado hatujakata tamaa na Serikali hii ya Awamu ya Nne haitakata tamaa katika mikakati yake na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata maji yaani wananchi wa mijini na vijijini.

Maombi ya *BADEA* tumewakilisha mwezi 3/2006 na bado tunayafuatilia mpaka hivi sasa, inachukua muda kupata majibu katika benki kubwa kama hizo kwa sababu wana taratibu ndefu tu za kupembua maombi ambayo wanayapata na wanayapata kutoka sehemu nyingi sana duniani, kwa hiyo bado tunafuatilia.

Lakini kwa sababu Serikali ina nia thabiti ya kuhakikisha tunapunguza tatizo la upatikanaji wa Masasi tumetenga fedha katika mwaka huu ili kuhakikisha kwamba miradi midogomidogo na uboreshaji wa upatikanaji wa maji hasa Masasi ambayo inalenga swali la pili katika chanzo cha Mwene maji yaweze kusukumwa kwa wingi zaidi kwenye katika Mji wa Masasi kuliko ilivyokuwa hivi sasa.

Sasa hivi tunapata mita za ujazo 5000 kwa siku lakini Mwene ina uwezo wa kupampu mpaka mita za ujazo 1500, shilingi milioni 345 zilizotengewa Masasi mwaka huu wa fedha maana yake ni hiyo ili kuondoa tatizo hilo.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, swali la nyongeza.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Singida Mjini na Singida Kaskazini kuna Bwawa moja la Itamka na tuliambiwa kwamba *BADEA* walikuwa wameahidi kusaidia

ule mradi ambao kimsingi ungepeleka maji kutoka Itamka kwani Itamka wana *catchments area* ambayo inakusanya maji mengi sana na kuyapeleka Singida Mjini na ingetosheleza.

Pia haya maji yangetosheleza vijiji mbalimbali vya Singida Kaskazini.

Naomba tu kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ule mradi unao kuwa *financed* na *BADEA* bado upo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu. Wizara yangu inashirikiana na *BADEA* katika mkoa wa Singida na kwa hivi sasa *BADEA* tayari wanafadhili Mkoa wa Singida na kuna wataalamu na mambo mbalimbali yanayoendelea huko. Kwa hali hiyo, naomba Mheshimiwa Lazaro Nyalandu tutaweza kumpatia hali halisi ya upande wa Bwawa hili la Itama kwa sasa hivi ikoje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa bado tupo Wizara ya Maji swali linaulizwa na Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi kwa niaba yake.

Na. 237

**Ukarabati wa Mtaro wa Ntomoko**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI (K.n.y. MHE. PASCHAL C. DEGERA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Bunge liliridhia kiasi cha Tshs. 100,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa mtaro wa Ntomoko, yaani Tshs. 40 mil/= kwa ajili ya ukarabati na Shs. 60 mil/= kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu vitatu, katika eneo la mtandao wa mtaro huo Wilayani Kondoa.

(a) Je, hadi leo Serikali imetoa kiasi gani cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa mtaro wa Ntomoko umekufa na kama inafahamu inachukua hatua gani kuufufua?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Bunge liliridhia kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa mtaro wa Ntomoko yaani shilingi milioni 40 kwa ajili ukarabati na shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuchimba visima virefu vitatu. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya dharura ya fedha yaliyojitokeza Serikalini fedha hizo hazikutolewa. Aidha, kutokana na hali hiyo kazi zilizopangwa hazikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa mtaro wa Ntomoko bado haujafa ila chanzo cha maji cha Ntomoko kimepungua uwezo wake kutokana na uharibifu wa mazingira unaotokana na mmomonyoko mkubwa wa udongo. Pia na shughuli mbalimbali za wakazi wa maeneo ya chanzo hicho. Kutokana na kupungua kwa maji kwenye chanzo, vijiji 6 tu ndivyo vinavyopata huduma ya maji kati ya Vijiji 16 zilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imepanga kukarabati mradi huu kupitia *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Mapitio ya mradi yatafanyika ikiwa ni pamoja na kubaini vijiji vinavyoweza kuendelea kupata maji kutoka chemchem za Ntomoko na vile ambavyo haviwezi. Wataalamu Washauri watafanya upembuzi wa kina ya maji kwa ajili ya vijiji mbalimbali vya mradi. Aidha katika upembuzi huo matumizi ya maji ya bwawa la Mwasanga yataangaliwa upya.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Estherina J. Kilasi.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji anapojibu swali la msingi amekiri kwamba huo mradi haujafa na katika majibu yake anasema Halmashauri inapanga ina maana kwamba huo mradi umekufa. Sasa wananchi watakuwa na matumaini gani kutokana na ile Bajeti ya milioni 100 ambayo ilikuwa imeidhinishwa kwa ajili ya mradi huu itakuwa tayari kusaidia?

Pili, kwa kuwa Wizara ya Maji ilikuwa imejiwekea kabisa vijiji 10 kila Wilaya kuwapa maji ya uhakika kwa kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha na Halmashauri mojawapo ni Mbarali na Wilaya ya Kondoa Kusini hazita *qualify* kupata pesa za Maendeleo kutokana na kuwa na hati chafu. Je, Wizara ya Maji ina mpango mwingine wowote wa kuhakikisha kwamba ahadi yake ambayo haitokani na pesa za wafadhili zenye masharti ya hati safi au vigezo vingine kuweza kukamilisha ahadi yake ya kuwapa maji Wilaya hizi katika vijiji vyote 10?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwa kufuatana na programu yetu hii ya maji kwa hivi sasa fedha zote zinapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu. Kwa mtindo ambao tunaita *D by D.* Kwa hali hiyo basi, fedha zote zitaweza kukamilishwa kwenye mradi huo hata zaidi ya milioni 100 ni kiasi cha Halmashauri wenyewe kuzipanga; na kwa kuwa fedha zipo kwao watapanga na kuutekeleza mradi huo. Hiyo haina wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, katika vijiji kumi kumi vya maji ni kweli kwamba Wilaya ya Mbarali haikufuzu vigezo na kanuni za matumizi ya fedha. Kwa hali hiyo, katika mwaka 2006/2007 Mbarali haikufuzu. Pia mwaka 2007/2008 Mbarali haikufuzu. Kwa hali hiyo ni kwamba Mbarali haitaweza kupatiwa ruzuku zake katika vipindi hivi viwili vya mwaka ambavyo hawakuweza kufuzu.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kwamba suala hili Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliliongelea kwa kirefu na pia Mheshimiwa Waziri Mkuu aliliongelea na alifafanua kuhusu mambo hayo kwamba wasioweza kufuzu inabidi mpaka wafuzu ili waweze kupewa. Vigezo hivyo vinatokana na makubaliano kati ya Serikali yetu pamoja na wafadhili ambao wenyewe ndiyo wanatoa hizo fedha. Kwa hali hiyo, namsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba azidi kusisitiza katika Wilaya yake ili angalau mpito utakaofuata waweze kufaulu vigezo hivyo ili waweze kupewa fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuko nyuma sana ya wakati, naomba tuvute kasi sasa. Tunahamia Wizara ya Miundombinu, swali linaulizwa na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha.

Na. 238

**Mawasiliano ya Simu**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu wananchi wa Kijiji cha Lekrimuni katika Kata ya Siha Kati Jimboni Siha wamekuwa wakiomba Serikali ipeleke mawasiliano ya simu za mkononi kwenye eneo hilo ili kuharakisha maendeleo yao kama ilivyo kwa vijiji vingine vinavyozunguka eneo hilo kama vile Kandashi, Karasi, Magadini, Naibilie na kadhalika.

Je, ni kwa nini Serikali isiwasaidie wananchi hao ili Makampuni ya simu za mkononi kama vile *Celtel, VODACOM, TTCL* na kadhalika yaweze kupeleka huduma katika Maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ipo kwenye mikakati kabambe ya kusambaza simu za mkononi kwa kutumia teknolojia ya *CDMA (Code Division Multiple Access)* katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa kujua umuhimu wa mawasiliano katika jamii, maeneo mengi Mkoani Kilimanjaro yatanufaika na huduma hii muhimu yakiwemo yale yanayopata mawasiliano kwa sasa kwa kutumia teknolojia ya si waya yaani *wireless local loop system (*WLL*)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ya mradi huo inategemea kumalizika mwishoni mwa mwezi Julai, 2007 ambapo maeneo ya Moshi Mjini, *KIA* na *Petershoff* yamenufaika na utekelezaji wa mradi huo. Awamu ya pili inayotarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Oktoba, 2007, itahusisha maeneo mengi Mkoani humo ambayo ni pamoja na yale yanayopata mawasiliano kwa kutumia teknolojia isiyotumia Waya (*WLL System*) kama yale ya Kindashi, Karasi, Magadini na Naibilie. Wananchi wa kijiji cha Lekrimuni Kata ya Siha Kati, Jimboni Siha watanufaika na utekelezaji wa mradi huu.

Aidha, maeneo mengine Mkoani Kilimanjaro yatakayonufaika na teknolojia hii ni Machame Wilayani ya Hai, Mwanga na Usangi Wilayani Mwanga, maeneo ya Tarakea, Keni, Mkuu na Mashati yaliyopo katika Wilaya ya Rombo. Maeneo mengine yatakayonufaika ni pamoja na Sanya Juu , Wilayani Siha, maeneo ya Same, Mambamiamba, Kihurio, Marindi, Gonja, Ndungu na Kisiwani, yaliyopo katika Wilaya ya Same. Aidha, katika Wilaya ya Moshi Vijijini maeneo ya Mabungo, Hakwe, Marangu Mtoni na Kibosho yatanufaika na teknolojia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya *Celtel* ina mpango wa wa kwenda kufanya utafiti wa namna ya kupeleka mawasiliano katika eneo la kijiji cha Lekrimuni ambapo baada ya utafiti huo kukamilika ujenzi wa mnara utaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa eneo la kijiji cha Lekrimuni Kata ya Siha na vijiji jirani vinavyozunguka eneo hilo havifikiwi na mitambo ya *TIGO* iliyoko katika maeneo ya Kwasadala na Boma Ng'ombe. Hata hivyo, kutokana na maombi haya ya Mheshimiwa Mbunge, Kampuni ya *TIGO* itayafanyia uchunguzi maeneo hayo yote ili yawekwe katika mipango yake ijayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *VODACOM* imeshabaini uhitaji wa mawasiliano katika Kata ya Siha, na kwa kuanzia, ilishaweka mawasiliano maeneo ya Ngarenairobi. Kwa sasa *VODACOM* iko kwenye mchakato wa kubaini maeneo muafaka ya kuweka mtambo Lekrimuni. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, sisi sote tunakubaliana kwamba kupata mawasiliano ya simu ni mtindo wa kisasa wa kuishi; na kwa kuwa tunakubaliana pia kwamba kijiji cha Lekrimuni kipo karibu sana na Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Siha; na kwa kuwa kuna hii *commitment a*mbayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameizungumzia sasa kwamba mwezi Oktoba, 2007 anategemea tutapata mawasiliano hayo.

Ni mambo gani ya msingi ambayo mimi natakiwa niwaeleze wananchi wangu ili waweze kujiandaa kwa ajili ya mwezi Oktoba, 2007 ambapo Mheshimwia Naibu ameizungumzia. Hasa ikikumbukwa kwamba kuna wakati tuliambiwa kwamba *TTCL* ilikuwa na mpango wa kupeleka *line* karibu 3,000 katika vijiji mbalimbali. Ni mambo gani ambayo anafikiri kwamba niyasisitize kwa sababu sasa hivi wananchi wananisikiliza kule ili waweze kujiandae kwa mpango huo ambao ameuzungumzia?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa juhudi anazofanya katika kufuatilia masuala yanayokera wananchi wake wa Siha.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nilipata bahati ya kutembea na Mheshimiwa Aggrey katika Jimbo lake lote.

Sasa ninapenda nimwambie tu Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwamba kubwa ni kuwapa *assurance* watu wake kwamba mawasiliano ya simu yataboreka katika Jimbo lake. Hawatakiwi kufanya lingine isipokuwa watumie simu hizo kwa manufaa na Maendeleo yao wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ana jambo la ziada.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu labda Kiswahili kilinichenga nilizunguka na Mheshimiwa Aggrey Mwanri katika eneo lile. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utulivu. *Order Please*. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Bado tupo Wizara hiyo hiyo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni.

Na. 239

**Ubovu wa Barabara Mkoani Iringa**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, hospitali ya Ikonda iliyoko Makete Mkoani Iringa inayoendeshwa na Kanisa Katoliki inatoa huduma nzuri kwa jamii, huduma bure kwa watoto chini ya

umri wa miaka mitano, yatima na wazee wasiojiweza; na kwa kuwa, hospitali hiyo hutoa huduma kwa Mkoa mzima lakini barabara Wilayani humo ni mbovu sana na hali hiyo husababisha vifo vya wagonjwa kabla ya kufikishwa hospitalini hapo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza miundombinu ya barabara Wilayani Makete ?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swlai la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hospitali ya Ikonda iko Wilayani Makete na inaendeshwa na Kanisa la Katoliki. Hospitali hii inafikika kwa kutumia Barabara ya Njombe-Makete au Kitulo-Makete kupitia Nkenja- Ndulamo au Ipelele – Bulongwa. Barabara zote hizi ziliharibiwa vibaya sana na mvua kubwa zilizonyesha nchini kote kati ya mwezi Desemba 2006 na mwezi Mei, 2007.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoani Iringa huzifanyia matengenezo barabara zote zilizo chini yake kulingana na Bajeti ambayo hupitishwa na Bunge hili Tukufu. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2006/2007 jumla ya shilingi bilioni 2, 856,099,000 zilipitishwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara Mkoani Iringa. Aidha, matengenezo ya baadhi ya barabara yaliahirishwa Mkoani humo kutokana na mvua nyingi zilizonyesha kati ya Desemba 2006 na Mei 2007.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa matengenezo yanaendelea kwa barabara mbalimbali Mkoani Iringa ikiwemo barabara ya Njombe –Makete ambayo Mkandarasi Nyamguruma *Enterprise Company Limited* anafanya matengenezo kati ya Mang'oto na Ipelele kwa jumla ya shilingi milioni 118,645,450. Wizara yangu kupitia *TANROADS* Mkoa wa Iringa ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa kuifanyia matengenezo barabara ya Ndulamo Nkenja –Kitulo. Kukamilika kwa kazi hizo kutazifanya barabara ziendazo kwenye hospitali ya Ikonda kupitika bila shida yoyote.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupewa nafasi hii. Barabara ya Njombe mpaka Makete ni kilomita 110. Katika Bajeti ya barabara hii pamoja na ile ya kutoka Mfumbi mpaka Makete ambazo pia zinapeleka wagonjwa Ikonda ni kilomita 95 na hii barabara imepangiwa milioni 60, wakati barabara ya Njombe-Makete vilevile imepangiwa milioni 60. Hizo ni fedha kidogo kuliko hata zilizokuwa zimetengwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Bajeti ya barabara mwaka huu tumetenga bilioni 600 karibu ni maradufu na zaidi. Sasa naomba Serikali inawambia nini wananchi wa Makete kama wao kiwango kile cha mwaka jana kinapungua zaidi, ina maana

kwamba wao siyo kipaumbele na hasa ukizingatia tatizo kubwa la Makete linalojulikana la Ugonjwa wa UKIMWI ambalo njia pekee ya kuliondoa ni kupiga vita umaskini kwa kuboresha miundombinu ya barabara ili kuto-*isolate* ile Wilaya kule? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunajali sana sana masuala ya usafiri na uchukuzi hasa katika suala la matengenezo ya barabara nchini kote. Tatizo kubwa linalotukumba ni uhaba wa fedha tunazozipata. Fedha zilizotengwa hizo bilioni 600 zitahitaji kutengeneza barabara zote nchini, na nina hakika kila Mbunge angependa sana kuona barabara zake zinapitika, lakini tunaishukuru Serikali kwamba sasa hivi imeipa umuhimu miundombinu hasa barabara ili kuona tunaunganisha Wilaya na Mikoa na Vijiji kwa lengo la kuboresha masuala ya usafiri na uchukuzi nchini.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, matatizo ambayo yanajitokeza katika Wilaya ya Makete ni sawasawa kabisa na matatizo yanayojitokeza pale katika Wilaya ya Njombe. Bahati nzuri Wilaya hizi zinapakana kati ya Njombe na Makete. Je, ingekuwa siyo busara kwa barabara ambayo inapita Njombe kwenda Makete kwa ajili ya huduma ya hospitali. Kwa sababu barabara hii inahudumiwa na Halmashauri na uwezo wa Halmashauri ni mdogo sana kama mwenzangu alivyokuwa analalamika kwamba kiasi kinachotengwa cha bajeti ya barabara ni kidogo. Je, isingekuwa busara sasa hivi hiyo barabara iwe chini ya *TANROADS y*aani Serikali Kuu?

Mheshimiwa Spika, la pili, hili ni la ahadi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hakuna kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kanuni hairuhusu swali la nyongeza ukiacha yule aliyeuliza swali la msingi huulizwa swali moja tu.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yono Kevela, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ningependa tu nimwombe Mheshimiwa Yono Kevela, wanapokaa katika Halmashauri zao walizungumzie suala hilo la uwezo wa kutengeneza barabara hizo. Zipo barabara baada ya mawasiliano ya Halmashauri na *TANROADS* zinaweza kupandishwa daraja. Kama anahisi suala hilo linaweza kuzungumzwa kwenye vikao vyao walizungumze na liwasilishwe rasmi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Wizara ya Fedha. Nimearifiwa kwamba Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, hayupo na alimwachia Mheshimiwa William Shellukindo amwulizie swali lake.

Na. 240

**Zoezi la Wafanyakazi Kujikadiria Kodi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, *TRA* ilianzisha utaratibu wa Wafanyabiashara kujikadiria kodi:-

(a) Je, zoezi hilo limeleta ufanisi gani?

(b) Je, ni matatizo gani yalijitokeza katika zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kujikadiria kodi yaani *Self Assessment System* umeainishwa katika kifungu Na.94 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004. Utaratibu huu hauwahusu wafanyakazi wa kuajiriwa bali unahusu Makampuni, Ubia, Udhamini, Mashirika na Taasisi zingine zinazotakiwa kulipa Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu, zoezi hilo limefanikiwa sana na hii inajionyesha wazi wazi kwa kuongezeka kwa kodi ya mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu, Mamlaka ya Mapato Tanzania haijapata matatizo yoyote ya utekelezaji wa zoezi hilo kutokana na usimamizi mzuri wa mfumo huu ndani ya utendaji wa Mamlaka hiyo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa imeonekana utaratibu huo ni mzuri na katika kudumisha demokrasia je, ni lini watumishi wengine wa Serikali wataruhusiwa kukadiria matumizi yao halafu ndiyo albaki iweze kulipwa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 ina utaratibu maalum kuhusu mtu yeyote aliyeajiriwa, *Taxation and source*, yule mwajiri ndiye anayetakiwa kukata kodi na kuziwasilisha *TRA*. Lakini kama mtumishi ana biashara nyingine zaidi ya ajira tunakuomba umwandikie *Commissioner General* na watakuja kufanya *assessment* na unaweza ukawekwa kwenye mfumo wa kukadiria kodi wewe mwenyewe.

Na. 241

**Upatikanaji wa Umeme wa Uhakika**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini katika ziara ya kukagua Vituo vya uzalishaji umeme nchini iliyofanyika Desemba, 2006 iliripotiwa kutamka kwamba, Nchi yetu itajitegemea kwa umeme kuanzia mwaka 2007 na kwamba, katika kipindi hicho umeme wa nguvu ya maji utakaozalishwa utafikia megawati 1200 na wa Makaa ya Mawe megawati 1000:-

(a) Endapo Serikali iliripotiwa sawa. Je, inaweza kutoa taarifa hiyo mbele ya Bunge, ili Wabunge waweze kufuatilia habari hiyo njema?

(b) Je, Serikali inaweza kuwapatia Wabunge ratiba ya uhakika ya jinsi umeme huo utakavyokuwa unazalishwa?

(c) Je, ni nini hasa kinasababisha mitambo ya gesi inayozalisha umeme kuharibika mara kwa mara hali inayosababisha usumbufu mkubwa wa mahitaji ya umeme Nchini, na nani anastahili kubeba hasara zinazotokana na usumbufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NAMADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Malaum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa dharura wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inajitosheleza kwa nishati ya umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati vinavyopatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mpango wa dharura ulihusu upatikanaji wa mitambo ya kukodi kutoka kampuni zinazozalisha umeme megawati 180 ili kukabiliana na upungufu wa umeme uliolikabili Taifa letu kufuatia ukame ulioikumba nchi yetu kuanzia mwaka 2003 hadi mwanzoni mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mfupi unahusisha ufungaji wa mitambo ya *TANESCO* ya kudumu inayotumia gesi yenye uwezo wa kuzalisha megawati 145.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda kati ni kutekeleza mradi wa umeme wa megawati 200 kutokana na mkaa wa mawe ya Kiwira na megawati 200 unaotumia gesi asilia eneo la Kinyerezi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu unahusisha miradi ya Mchuchuma, *Stigle's Gorge*, Rumakali *Hydro*, Mpanga *Hydro*, Masigira *Hydro* na *Rusumo Hydro.*

(b) Muda wa kutekeleza kikamilifu miradi hii utafahamika baada ya *Power System Master Plan* kukamilika mwanzoni mwa 2008.

(c) Mheshimiwa Spika, matatizo yanayosababisha mitambo ya gesi inayozalisha umeme kuharibika mara kwa mara ni hitilafu mbalimbali za kiufundi. Mikataba iliyopo ina vipengele vya faini kutokana na kutokuzalisha umeme kwa kampuni zinazomiliki mitambo hiyo.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa umeme utokanao na chanzo cha maji *Hydro Power* kwa kweli hauna uhakika na kwa kuwa wataalam wa nishati wamekwishatabiri kuwa baada ya miaka 30 mafuta *Hydro Cabon* yatapungua sana duniani. Je, Serikali inafikiria nini kuwa na mpango kabambe sasa wa kuangalia maeneo ya nishati ya jua wakaanzisha chombo maalum kama *Solar Energy Development Authority* ambacho kitasimamia kueneza nishati ya jua. Kwa mfano, kule Nigeria imeingia ubia na Ulaya inatengeneza umeme wa jua na kuweka kwenye *accumulators* na kuuza nchi za nje pamoja ikiwa na gesi ya kutosha nchini?

La pili, je, Serikali haioni kuna umuhimu pia wa kuhimiza njia ya upepo *Wind Power* kwa ajili ya maeneo na hasa Mikoa yenye kuwa na upepo mwingi. Kwa mfano, Mkoa wa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NAMADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba chanzo cha maji kama chanzo cha nishati ni mojawapo ya vyanzo vya uhakika duniani. Lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kuwa na vyanzo mbadala ili kuungana na vyanzo ambavyo tunavitumia sasa hivi kikiwemo chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, suala la kufikiria vyanzo mbadala tunaendelea nalo hata Wizara sasa hivi inalifanyia kazi; na kwa kweli vipo vyanzo mbadala ambavyo tunavifanyia kazi ikiwemo nishati ya jua.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwenye Sheria Mpya ambayo inakuja mambo hayo tutayaangalia kwa upana zaidi ili kuhakikisha kwamba tunakaribisha sekta binafsi ishiriki kwa viwango mbalimbali, lakini lengo likiwa ni moja tu kuhakikisha kwamba nchi inajiweka katika mazingira mazuri zaidi ya kuwa na nishati hasa ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili la chanzo kinachotegemea upepo. Ni kweli hata hilo tunalifanyia kazi na hapa Tanzania sasa hivi tuna miradi kadhaa ambayo tunaiendeleza ili kuzalisha umeme kwa kutumia hii nishati ya pepo. Kwa hiyo, mambo hayo yote yanazingatiwa; na kwa kweli tunaendelea kufanya kazi. Lakini kama nilivyosema kwenye Sheria mpya inayokuja mambo hayo tutayaangalia kwa wigo mpana zaidi ili kukaribisha Sekta binafsi na washiriki wengine ili kuboresha huduma ya umeme.

Na. 242

**Mchango wa Madini katika Uchumi wa Taifa**

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

Kwa kuwa, madini hasa dhahabu yametoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa:-

(a) Je, bei ya dhahabu katika soko la Dunia, imeongezeka kwa kiasi gani katika kipindi cha mwaka 2000 – 2006?

(b) Je, Serikali imefaidika vipi kutokana na mabadiliko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni, bei ya dhahabu imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Ongezeko la bei linatokana na kuongezeka kwa mahitaji ambako hakuendi sambamba na kiwango cha dhahabu kinachozalishwa. Kati ya mwaka 2000 hadi 2006, bei ya dhahabu iliongezeka toka Dola za Kimarekani 265 hadi Dola za Kimarekani 725 kwa wakia kama ifuatavyo:-

- Kati ya Januari, 2000 na Julai, 2003 bei ya dhahabu ilikuwa chini ya Dola za Marekani 350 kwa wakia;

- Kati ya Agosti 2003 hadi Agosti 2005 bei ilikuwa kati ya Dola za Marekani 350 hadi 450 kwa wakia; na

- Kati ya Septemba 2005 hadi Desemba, 2006 bei ilikuwa kati ya Dola za Marekani 450 hadi 725 kwa wakia.

(b) Mheshimiwa Spika, kupanda wka bei ya dhahabu katika soko la dunia kuliongeza ari ya Makampuni ya ndani na nje ya nchi kuweza (*Local and Foreign Direct Investment (LDI and FDI)* katika utafutaji na uchimbaji mkubwa wa dhahabu.

Ongezeko hili linathibitishwa na kuongezeka kwa leseni zilizotolewa toka mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo; leseni 45 mwaka 2000, leseni 56 mwaka 2001, leseni 85 mwaka 2002, leseni 146 mwaka 2003, leseni 518 mwaka 2004; na leseni 784 mwaka 2005.

Mwaka 2006 leseni zilizotolewa zilikuwa 146. Upungufu huu ulisababishwa na sababu nyingi zikiwemo za maeneo ya utafutaji dhahabu yaliyobakia kuwa machache.

Kati ya mwaka 2000 na 2006 jumla ya leseni za utafutaji dhahabu zilizotolewa zilikuwa 11,780 ambazo ziliipatia Serikali jumla ya Dola za Marekani 439,250, kama ada ya leseni na dola za Marekani milioni 6,775,473.2 kutokana na malipo ya kodi za mwaka.

Mheshimiwa Spika, kampuni zilizopewa leseni hizo zilitoa ajira kwa Watanzania na pia zilinunua huduma na bidhaa za ndani. Aidha, kuongezeka kwa shughuli za utafutaji dhahabu katika kipindi cha 2004 hadi 2006 kuliwezesha kufunguliwa Mgodi wa Tulawaka ambao ulilipa kodi mbalimbali Serikalini jumla ya dola za Kimarekani milioni 8,229,479 kati ya mwaka 2005 na 2006.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba kuanzia mwaka 2000 hadi 2006 mapato ya dhahabu yaliongezeka duniani na akatupa *figure* yameongezeka kwa shilingi 265 mpaka 725 kwa wakia. Ni kwa nini katika vitabu vya Serikali inaonyesha *revenue* katika mwaka 2005/2006 ilikuwa ni bilioni 28.5, lakini mwaka 2006/2007 ika-*drop* mpaka bilioni 27. Hivyo, ni kwa nini wakati mapato ya dhahabu yaliongezeka, lakini *revenue* ndani ya nchi yetu inaonekana yalipungua.

La pili, ningependa kujua, kwa kuwa amekiri kwamba kuanzia mwaka 2000 mpaka 2007 leseni 11,780 zilitolewa. Ningependa kujua katika leseni zote zilizotolewa ni leseni ngapi ambazo hivi sasa zimekuwa *confirmed* wamegundua machimbo ya dhahabu sasa hivi wanazalisha?

**SPIKA:** Swali la pili, linahitaji takwimu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu maswali yote mawili ya nyongeza yanahitaji takwimu. Amesema kutokana na takwimu kuanzia 2005/2006 na 2006/2007 kuna tofauti ya mapato. Lakini niseme kwamba kwa sababu masuala haya hajasema chanzo chake hasa cha kufikia kuuliza swali hili ni nini?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda nimkaribishe Mheshimiwa Mbunge ofisini tumpe takwimu za uhakika, tujiridhishe na kile ambacho amekisema. Halafu tufikie kiwango cha pamoja cha uelewe kwa yale ambayo sisi tumekuwa tukiyasema kama Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, nitafidia muda ule tulioutumia kwa matangazo. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 243

**Ziada ya Mahindi – Rukwa**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Rukwa hutoa ziada ya Mahindi kwa ghala la Taifa *(SGR)* na ziada hubaki kwa wakulima:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa uamuzi wa kudumu wa kuruhusu wananchi kuuza ziada ya Mahindi nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mkoa wa Rukwa ni mmojawapo wa Mikoa inayozalisha ziada ya zao la mahindi, Mkoa huu ni wa muhimu ambako Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* hununua mahindi kwa ajili ya kukabiliana na dharura za njaa. Ni kweli pia kuwa wakati mwingine hata baada ya *SGR* kununua mahindi kulingana na lengo la kuhifadhi na uwezo wa fedha katika msimu unaohusika wakulima wamekuwa wakibakiwa na ziada ya chakula.

Mheshimiwa Spika, takwimu za uzalishaji wa mazao za miaka mitano iliyopita (2004/2005-2006/2007) zinaonyesha kuwa kwa wastani Mkoa wa Rukwa huzalisha jumla ya tani 470,000 za mazao mbalimbali ya chakula kwa mwaka ambapo asilimia 60 ya mazao hayo ni mahindi. Wakati huo huo, mahitaji ya chakula kwa Mkoa wa Rukwa katika kipindi hicho kwa wastani ni tani 330,000 kwa mwaka hivyo kunakuwepo na ziada ya takriban tani 140,000 za chakula.

Katika kipindi hicho cha miaka mitano iliyopita *SGR* imekuwa ikinunua wastani wa tani 17,000 za mahindi kwa mwaka kutoka Mkoa wa Rukwa. Kiwango cha juu cha ununuzi wa mahindi Mkoani humo kilikuwa tani 32,600 zilizonunuliwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja na kuwa na sera ya Serikali ya kuwa na soko huru la bidhaa mbalimbali yakiwemo mazao ya kilimo hususan chakula, Serikali pia inalo jukumu la kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na uhakika wa chakula wakati wote. Katika kufanya hivyo, Serikali kupitia Wizara yangu imekuwa ikiratibu hali ya chakula ya nchi nzima na kuchukua hatua za kuhakikisha upatikanaji wa chakula hasa katika maeneo ya nchi ambayo yana upungufu wa chakula. Hivyo, ziada ya mahindi katika eneo moja la

nchi inaweza kuwa ni chanzo cha upatikanaji wa chakula katika eneo lingine la nchi lenye upungufu kupitia utaratibu wa soko la ndani.Aidha, hatua ya Serikali ya kusitisha kuuza chakula nje ya nchi kwa vipindi fulani ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kinakuwepo chakula cha kutosha nchini ili kuepuka Serikali kuingia gharama kubwa na isiyo ya lazima ya kuagiza chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kutumia utaratibu wa kuratibu hali ya chakula nchini inatumia busara katika kuruhusu uuzaji nje wa mazao ya chakula pale inapoonekana kuwa hali ya chakula inaridhisha na kusitisha kuruhusu hiyo pale ambapo hali ya chakula ni mbaya.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kwamba wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanapoondoa chakula chao ziada hubakia tani 140,000. Na kwamba uwezo kwa kihistoria wa *SGR* kununua mazao mwaka 2004 ilikuwa ni tani 32,000. Sasa swali langu ni kuwa je, kazi ya kulisha wananchi inapotokea upungufu wa njaa katika maeneo mbalimbali ni kazi ya Serikali au ya mkulima*? (Makofi)*

Pili, Waziri anafahamu kwamba kutoa mahindi katika Mkoa wa Rukwa kwa kupeleka mikoa kama ya Dar es Salaam na sehemu nyingine ni gharama na kiasi ufika mpaka shilingi 10,000 kwa gunia moja na inasababishwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kutokuuza mazao isipokuwa Zambia na Congo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu ya ufasaha aliyoyatoa kuhusu swali hili. Pili napenda kutumia nafasi hii kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Wajibu wa kuhakikisha nchi hii ina chakula ni wa Serikali kwa kushirikiana na wakulima kwa sababu wakulima ndio wanaolima chakula. Hakuna namna nyingine yoyote na nchi hii si ya Serikali ni ya wakulima ambao ndio wanaohitaji kuwa na chakula vile vile. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Mzindakaya ajue kwamba nchi ni pamoja na wakulima ambao wanaongozwa na Serikali.

Sasa kuhusu suala la Rukwa ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mzindakaya kwamba Serikali inajua na inathamini mchango mkubwa unaotolewa na wakulima wa Rukwa katika kulisha Taifa letu. Lakini kila inapotokea tatizo Serikali inashirikiana na Mkoa wa Rukwa katika kutafuta ufumbuzi. Mwaka jana Mkoa wa Rukwa ulikuwa umetoa ziada kubwa na Wizara yangu ilitoa kibali cha tani 78,000 kuuzwa katika nchi ya Zambia ili kuondokana na tatizo la kuwa na ziada ambayo haikuweza kutumika katika Mkoa huu

Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wakulima wa Mkoa Rukwa na Mheshimiwa Mzindakaya atakubaliana na mimi kwamba hatuna njia nyingine isipokuwa kupata chakula kinachotokana na wakulima na wakulima lazima washirikiane na Serikali na Serikali lazima ijali matatizo ya wakulima wanaozalisha chakula.

Na. 244

**Ununuzi wa Korosho – Mtwara**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wa Korosho wa Mkoa wa Mtwara wanafanya jitihada kubwa za kuongeza uzalishaji, lakini kila mwaka wanakatishwa tamaa na wanunuzi binafsi wanaonunua chini ya bei iliyokubaliwa kati ya wakulima na wanunuzi; na kwa kuwa, suluhisho la tatizo hilo ni vyama vikuu vya ushirika wa wakulima vya *TANECU* na *MAMCU* Mkoani hapo kununua na kuzisafirisha Korosho nje ya nchi na nyingine kuwauzia wabanguaji wa hapa nchini:-

(a) Je, ni sababu zipi zinasababisha vyama hivyo kushindwa kununua korosho?

(b) Kwa kuwa, msimamo wa Serikali ni kuimarisha Vyama vya Ushirika. Je, Serikali inachukua hatua zipi madhubuti ili vyama hivyo vianze kununua mazao, hasa Korosho kama ilivyokuwa miaka ya nyuma?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mbunge wa Newala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zinazofanya vyama vikuu vya ushirika vya Mkoa wa Mtwara visiweze kununua korosho ni pamoja na:-

· Mitaji midogo ya ndani kutokana na kuwa na idadi ndogo ya wanachama;

· Kuwa na madeni makubwa ya mabenki, hivyo kutokopesheka;

· Uongozi mbovu, ubadhirifu na wizi katika vyama hivyo na vyama vya ushirika vya msingi; na

· Baadhi ya wanachama na viongozi kutokuwa na elimu ya kutosha ya ushirika na ujasiriamali.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali ili vyama hivyo viweze kununua mazao, hasa korosho kuanzia msimu wa 2007/2008 ni kama ifuatavyo:-

· Serikali imevifutia vyama vikuu vya Ushirika vya Mkoa wa Mtwara madeni ya jumla ya shilingi milioni 844,592 yaliyokuwa yanadaiwa na Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya na Taasisi za Serikali kama ilivyopitishwa na Azimio Na. 4 la Bunge lako Tukufu katika Kikao chake cha Bajeti mwezi Julai 2006. Kutokana na hatua hii vyama

vikuu vya *TANECU* na *MAMCU* vinaweza kukopesheka kama vitatimiza masharti mengine ya benki za biashara.

· Serikali imepeleka wakaguzi kufanya uchunguzi wa hali halisi ya vyama vikuu mkoani humo ili wanachama waweze kufahamishwa juu ya hali ya Maendeleo ya vyama vyao; na hatua za kuchukua.

· Uchaguzi wa viongozi wapya umefanyika katika vyama vikuu vya *TANECU* na *MAMCU* ikiwa ni hatua ya kuweka uongozi wenye uwezo na makini katika vyama hivyo;

· Matayarisho yamekamilika ya kuwapatia elimu ya ushirika viongozi wapya waliochaguliwa kuongoza vyama hivyo;

· Serikali imepeleka Watendaji Wakuu wa muda katika vyama hivyo kama hatua ya mwanzo ya kuviwezesha vyama hivyo kujipanga kibiashara;

· Serikali inaendelea na mchakato wa kuhamisha baadhi ya Maafisa Ushirika waliokaa kwa muda mrefu katika maeneo hayo na kuweka wengine ili kuimarisha kazi za ukaguzi na usimamizi wa vyama; na

· Wizara yangu itaendelea kuratibu upatikanaji wa mikopo ya ununuzi wa pembejeo na ununuzi wa mazao, ili kuviwezesha vyama hivyo kutekeleza wajibu wake kwa wakati.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Moja alisema kwamba mitaji midogo ya vyama vya ushirika. Mwaka jana Serikali ilifuta ushuru kwa vyama vya msingi katika Mkoa wa Mtwara. Ushuru ambao kila mwaka ulikuwa unawawezesha vyama vya msingi kuongeza mtaji wao. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo katika msimu unaokuja.

La pili, nchi hii inazalisha korosho karibu tani 60,000 viwanda vyetu vyote nchi hii kama vingepata mtaji wa kununua korosho kwa wakulima vingebangua korosho zote kwa hivyo tusingelihitaji kupeleka korosho ambazo hazijabanguliwa nje. Kwa hiyo, tungeuza korosho nje ambazo zina *value added.*

Je, Serikali inasema nini kuhusu hili kwamba je, inaweza kuchukua hatua kuhakikisha wenye viwanda katika nchi hii wanakopeshwa ili korosho zote zibanguliwe nchini ili tuongeze ajira tufikishe ile milioni moja ambayo imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DAVID M. DAVID):** Kwanza niseme ushuru wa mazao kupunguzwa. Ushuru wa mazao umepunguzwa katika mazao yote yale ambayo yalikuwa yanatozwa ushuru kusudi kumwongezea mkulima uwezo na nguvu ya kuweza kuongeza mazao yake. Kwamba hii tumepunguza mzigo kwa mkulima na sio kwa korosho peke yake kwa pamba pia tumepunguza, kwenye kahawa pia tumepunguza na mazao mengine.

Pili, Serikali inaendelea kuhamasisha wale ambao wanataka kujenga viwanda na vile vile inahamasisha wale ambao wanavyo viwanda vile kusudi waweze kukopa mabenki ili waweze ku-*process* zile korosho zisiende nje zikiwa ghafi. Kama mnakumbuka kuna Kiwanda kinaita Bucco kilipewa *guarantee* na Serikali kusudi kiweze kukopa kwenye benki ya *CRDB* ili waweze kubangua korosho nchini bila ya kuzisafirisha zikiwa hazijabanguliwa. Kwa hiyo, Serikali inaunga mkono na inasaidia katika hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo kama kawaida tunaanza na wageni. Naomba nitambue kuwepo kwa mgeni wa Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wetu wa Maji, naye si mwingine ni mkewe anaitwa Saumu. Mama Kawambwa yule pale, karibu sana Bungeni na watoto wao Karim na Malik Kawamba, wale pale. Ahsante sana, karibuni sana.

Wakati huo huo naomba nitambue kuwepo kwa Ndugu Patrick Mwangunga, mumewe Naibu Waziri wa Maji. Karibu sana Mheshimiwa Mwangunga. Hapa naona nitoe tahadhari kwa wale waliokuwa wanazoea kila mara kumwalika Naibu Waziri kwenda Majimboni na hivi. Leo mzee mwenyewe yupo, kwa hiyo mialiko hiyo iwe ya kiheshima isiwe ya ovyo ovyo. Karibu sana Bwana Patrick. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anao wageni wake viongozi 50 wa wanawake kutoka Vyama vyote huru vya wafanyakazi ambao wamekuja Dodoma kwa ajili ya kuhudhuria warsha ya wanawake viongozi katika vyama vya wafanyakazi kupitia Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUKUTA). Viongozi Wanawake wa Vyama Huru Vya Wafanyakazi naomba msimame. Wale pale. Karibuni sana tunawapongeza kwa harakati zenu za kuendeleza wanawake hapa nchini. Ninyi kama viongozi katika vyama vya wafanyakazi ni muhimu katika hilo kwa sababu mfumo wetu dume bado uko hai. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene viongozi 9 wa Chama cha Mapinduzi na Serikali Kata ya Mlunduzi jimbo la Kibakwe. Wale pale. Karibuni sana na poleni na safari kutoka Kibakwe.

Wapo Madiwani, Maafisa Watendaji Kata, Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka Kata za Bunju, Mburahati na Makuburi wakifuatana na Mchumi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, jumla yao ni 21. Sijui wako wapi wale? Wale pale kwa *Speaker's Gallery*, ahsante sana. Hao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam.Wapo wageni wa Eng. Stella Manyanya ambao ni Padri Mathias Mulumba, Parokia ya Kitale Kenya na Mwinjilisti Gabriel Otiatu kutoka Nakuru, Kenya. Karibu sana. Kila mara tunafurahi kuona Ndugu zetu kutoka Kenya, tunatembelea tukiwa wamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Mnyaa ni Mheshimiwa Diwani Masisa, Diwani wa Geita na Mheshimiwa Pille Martin Diwani wa Geita. Wale Madiwani kutoka Geita wale pale. Karibuni sana, ahsante sana. Pia wako viongozi watendaji wa Chuo Kikuu

Huria cha Tanzania ambao pia nitangaze kwenu Waheshimiwa Wabunge kwamba Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria sijui amekuja, lakini wapo watendaji ambao wanasimamia maonyesho ya machapisho mbalimbali ya chuo hicho kwenye Uwanja wetu wa tafrija wa Bunge. Mnakaribishwa sana Waheshimiwa Wabunge kwenda kuona machapisho mapya na vitabu vya Chuo Kikuu Huria pale kwenye uwanja wetu wa tafrija. Wageni kutoka Chuo Kikuu Huria nadhani wanawasubiri huko huko kwenye viwanja vya tafrija.

Wageni wetu Bungeni leo ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Milambo kutoka Dar es Salaam. Naomba wasimame pamoja na walimu. Karibuni sana vijana, karibuni sana walimu tunapenda sana mnapokuwa mnawaleta vijana kuona jinsi Bunge lao linavyofanya kazi. Karibuni sana na pole na safari ya kutoka Dar es Salaam. Aah!! Waziri Mkuu amesema hongera kwa safari ya kutoka Dar es Salaam na tunawatakia safari njema kurejea nyumbani. Ahsante sana.

Wapo pia Waheshimiwa Madiwani kutoka jimbo la Chalinze wageni wa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Maneno. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. Ahsante sana. Bwana Onesmo Mashiri ni mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri William Ngeleja yeye ni Mtendaji wa Kata ya Igalula kule jimboni. Yule pale. Karibu sana Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Mheshimiwa Anna Abdallah ameomba kwamba wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje wakutane leo saa 5.00 asubuhi chumba Na. 219.

Mengine ambayo ya ziada tu. Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa wanatafuta mikopo midogo midogo nilikuwa napenda kuwaarifu sasa utaratibu ni tayari na kuanzia leo wanaweza kwenda kuipata. Nadhani mnanielewa. Mambo madogo madogo kama haya huwa tunamaliza haraka tu wala hayana tatizo sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Jumamosi tarehe 21 pamoja na kuwa ndiyo siku ya *VIP Race* yaani mbio zetu zile za kilomita 5 saa 12.00 asubuhi ambapo mgeni rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini pia tutakuwa na zoezi la kumwunga mkono Mheshimiwa Rais kuhusu upimwaji wa UKIMWI. Zoezi hilo litafanyika saa 3.00 asubuhi katika eneo ambalo Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma atatuarifu. Kwa sababu jambo hili linatakiwa lifanywe mbele ya wananchi tunaowawakilisha, kama alivyofanya Mheshimiwa Rais kule Dar es Salaam.

Nipende tu kutangaza kwamba atakayepimwa wa kwanza kabisa ni Spika wa Bunge. Kwa hiyo, hakuna sababu yoyote ya Mheshimiwa Mbunge yeyote kutafuta kisingizio cha kutokuwapo saa 3.00 siku ya Jumamosi.

Ili tuweze kuwadhihirishia wananchi na Rais wetu kwamba jambo hili ni muhimu sana kwa afya zetu lakini pia kwa afya za Taifa letu. Saa 3.00 asubuhi katika eneo ambalo tutawatangazia kupimwa *HIV* ukianzia na Spika mwenyewe.

Naomba nitoe ufafanuzi hasa kwa wenzetu wa vyombo vya habari kuhusu mahudhurio ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukishambuliwa sana kwamba humu hatukai sana na kadhalika. Lakini ni kutokukelewa tu.

Mimi ningeomba wenzetu Waandishi wa Habari wanapokuwa na jambo ambalo wanaliona halikukaa sawa wawasiliane. Mimi ni muwazi mlango upo wazi tunatoa maelezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, wananchi wafahamu na hususan Waandishi wa Habari kwamba Bunge linaendeshwa kwa mtindo wa Kamati, hakuna kinachofika hapa mezani bila ya kuwa kimepitishwa kwenye Kamati.

Kwa hiyo, mara baada ya matangazo mathalani kuna Wabunge watatoka, lakini sio kwamba hawapo kazini. Maana yake sura inayojitokeza ni kutuonyesha kwamba ni wazembe tunakwepa wajibu, kitu ambacho siyo kweli.

Wabunge wengi wanakuwa wamo kwenye Kamati na ndiyo maana tuna utaratibu wa kengele. Tukipiga kengele wote sehemu za kazi walipokuwa kwenye Kamati na kadhalika wanarejea Bungeni tunaendelea na kazi. Hata anayetazama *House of Commons* na Mabunge ya Australia na wapi ataona kwamba si kawaida Wabunge wawe wamekaa tu kwenye viti saa zote hadi jioni na hilo sio dalili ya ufanisi.

La pili, hapo nje wapo wapiga kura zaidi ya 200 wanawasubiri Wabunge hawa hawa. Sasa Wabunge tukijifungia humu tusisikilize wananchi nayo ni matatizo. Kwa hiyo, wengine wanakuwa wapo nje wanawasikiliza wananchi jambo ambalo ndilo tulichaguliwa kuweza kulifanya. Kwa hiyo, baadhi ya viti vitakuwa wazi.

La tatu Wabunge wanasafiri, wengine wanatuwakilisha nje ya nchi kwenye Mikutano ambayo Bunge letu linawakilishwa na wengine kwa mfano nitoe Wabunge wote wa Kamati ya Miundombinu walikuwa Dar es Salaam juzi na jana kwa ajili ya uzinduzi wa Mpango mpya wa Bandari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mohamed Missanga na wenzake walikuwa Dar es Salaam. Wako kazini hao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba vyombo vya habari hasa wale ambao wanapenda tu kupiga picha katuni na kuonyesha viti tupu na hivi kwamba ipo sababu. Viti kuwa havina Wabunge si ushahidi kwamba Wabunge hawazingatii kazi yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Maji

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Maji, nilikuwa napenda kusema tu kwamba tumesikiliza na ili kupata muda wa kutosha wachangiaji kwamba Waheshimiwa Mawaziri ingawa wanaruhusiwa hadi dakika 60 kuleta hoja zao watajitahidi wafanye hivyo kwa dakika 30 ili kutuwezesha kupata nafasi ya uchangiaji zaidi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Maji baada ya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri mwezi Oktoba, 2006.

Pia, naishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Jimbo la Ileje, kwa maoni, ushauri na mapendekezo iliyoyatoa wakati Wizara yangu ilipowasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

Maoni, ushauri na mapendekezo hayo yamesaidia Wizara yangu kuboresha huduma za maji nchini kwa kipindi cha mwaka uliopita. Aidha, ushauri, maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo wakati nilipowasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008 yameboresha kwa kiwango kikubwa maandalizi ya mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa sana taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu; Hayati Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), aliyeaga dunia baada ya ajali ya ndege wakati akitekeleza majukumu ya kitaifa.

Pia, Wizara imepokea kwa huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hayati Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge Viti Maalum (Vijana). Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Tunduru na Umoja wa Vijana wa CCM. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. (*Amin)*

Mheshimiwa Spika**,** naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Benard K. Membe, aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge); Mheshimiwa Gaudence C.

Kayombo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Pia, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2006/2007 ambao ni Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura wa CCM kwa kuchaguliwa kuliwakilisha Jimbo la Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, kuchukua fursa hii, kuwashukuru na kuwapongeza mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Alhaj Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge wa Jimbo la Ulanga Magharibi; Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa; na Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya mipango, uchumi, mapato na matumizi, na utendaji wa Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, rambirambi na shukrani hizo, sasa nizungumzie masuala yahusuyo Sekta ya Maji ambayo yameainishwa katika maeneo makuu matano.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kuhusu sekta ya maji yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 6 hadi 10 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika kwa sekta ya maji maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 yamezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika**,** katika mkakati huo, Wizara ya Maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama karibu na makazi yao kwa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma hiyo kutoka asilimia 53.5 ya mwaka 2004/2005 hadi asilimia 65 kwa wananchi waishio vijijini na kutoka asilimia 73 ya mwaka 2004/2005 hadi asilimia 90 kwa wananchi waishio mijini ifikapo mwaka 2010.

Ili kuhakikisha malengo ya MKUKUTA yanafikiwa, mwezi Desemba 2006, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Programu hiyo itatekelezwa katika ngazi mbalimbali na Serikali Kuu itasimamia utekelezaji huo kwa kutoa miongozo ya kisera na kiutendaji, misaada ya kitaalam, mafunzo, nyenzo na

vifaa. Maelezo kuhusu hali halisi ya Sekta ya Maji yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 11 hadi 13 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali kubwa ya maji ingawa haipatikani kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote. Tanzania ina mito mingi, maziwa ya maji na hifadhi kubwa ya rasilimali za maji chini ya ardhi. Pamoja na hali hiyo, yapo matatizo yanayosababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na ukame wa mara kwa mara, uharibifu wa mazingira, uchafuzi wa vyanzo vya maji na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya uvunaji na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, Utoaji wa Huduma za Maji: Kwa sasa huduma ya utoaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa vijijini imeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005/2006, hadi kufikia asilimia 55.7 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Aidha, huduma ya utoaji wa maji safi na salama mijini katika Makao Makuu ya Mikoa imeongezeka kutoka asilimia 74.0 mwaka 2005/2006 hadi kufikia asilimia 78.0 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 4. Ongezeko la huduma za maji kwa viwango hivyo ni la kuridhisha kufikia malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, matukio muhimu katika sekta ya maji mwaka 2006/2007: Maelezo kuhusu Matukio Muhimu Katika Sekta ya Maji Mwaka 2006/2007 yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 14 hadi 24 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 kumekuwepo matukio muhimu katika sekta ya maji ambayo yalilenga katika kuhakikisha kuwa Sera ya Maji ya mwaka 2002 inaenezwa na kutekelezwa kikamilifu. Matukio hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Tathmini ya Wadau kuhusu Sekta ya Maji: Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*), iliitathmini sekta ya maji kwa lengo la kubaini matatizo yanayoikabili, changamoto zilizopo na mbinu za kuiwezesha kufikia malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapundizi (CCM) ya mwaka 2005. Mapitio hayo yalibaini maeneo muhimu ya kutekeleza ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha majadiliano kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na Asasi nyingine zisizo za kiserikali kujadili sekta ya maji;

(ii)Serikali kuanza kuandaa mipango na bajeti kwa kuhusisha sekta nzima badala ya kuangalia mradi mmoja mmoja kama ilivyokuwa hapo awali;

(iii)Kuainisha vigezo sahihi na vilivyo wazi vya kupima maendeleo ya sekta ya maji ; na (iv)Kuipatia sekta ya maji fedha kwa kiwango cha kutosha.

(b) Majadiliano ya Serikali na Washirika wa Maendeleo: Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini ya sekta ya maji, mwezi Desemba 2006, Serikali ikiwakilishwa na

Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilijadiliana na Washirika wa Maendeleo wakiongozwa na Benki ya Dunia jinsi ya kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo jumla ya Dola za Marekani milioni 951 zinahitajika. Kati ya fedha hizo Serikali itachangia Dola za Marekani milioni 251.

(c) Maadhimisho ya Wiki ya Maji: Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Machi kila mwaka, nchi yetu huungana na mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Maji Dunia ambapo huitumia kama kilele cha Wiki ya Maji, ambayo maadhimisho yake huanza tarehe 16 Machi.

Maadhimisho ya Wiki ya Maji kitaifa mwaka 2007 yalizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na yalifikia kilele tarehe 22 Machi 2007 mjini Moshi, ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alizindua Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. *(Makofi)*

(d)Kongamano la Wataalam wa Maji: Mheshimiwa Spika, kila mwaka Wizara yangu hufanya Kongamano la Mwaka la Wataalam wa Maji *(Annual Water Experts Conference, AWEC).* Kongamano hilo huwakutanisha wataalamu wa maji kutoka ndani na nje ya nchi na hupata fursa ya kujadili masuala ya utekelezaji wa Sera ya Maji, kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika sekta ya maji hapa nchini na katika nchi nyingine. Katika mwaka 2006/2007 Kongamano hilo lilifanyika mjini Arusha mwezi Januari 2007 kwa kujadili mikakati mbalimbali ya kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

(e) Mkutano wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini: Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2006, Mkutano wa Nane wa Mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini ulifanyika mjini Kigoma na mwezi Machi 2007 Mkutano wa Tisa ulifanyika Jijini Mbeya. Mikutano hiyo ilitoa maazimio yaliyolenga kusogeza huduma za maji kwa wakazi wanaoishi pembezoni mwa miji na kuboresha ubora wa maji. Utekelezaji wa maazimio hayo, ulianza katika mwaka 2006/2007 na utaendelea katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007 na Malengo ya Mwaka 2007/2008: Maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007 na Malengo ya Mwaka 2007/2008 kuhusu eneo la Rasilimali za Maji, yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 26 hadi 42 ya Hotuba yangu

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi na Tathmini ya Rasilimali za Maji: Rasilimali Za Maji: Wizara yangu huchunguza wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kutumia mtandao wa vituo vya kupima mwenendo wa rasilimali hizo. Hivi sasa mtandao huo una jumla ya vituo 397 vya kupimia wingi na ubora wa maji, vituo 97 vya hali ya hewa, vituo 739 vya kupima kiasi cha mvua na vituo 39 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi. Katika jitihada za kuboresha mtandao huo mwaka 2006/2007, Wizara ilikarabati vituo 53 vya kupimia wingi na ubora wa maji; vituo 10 vya

hali ya hewa; na kujenga kituo kimoja kipya cha kupima mvua. Aidha, Wizara iliendelea kutafuta vyanzo vipya ya maji na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 Wizara yangu iliendelea kusimamia na kuratibu kwa karibu uchimbaji wa visima vya maji nchini kwa lengo la kuhakikisha kwamba taratibu zilizowekwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Maji Namba 42 ya mwaka 1974, zinafuatwa. Wizara pia, iliendelea kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji kwa kutoa hati za haki ya kutumia maji kwa lengo la kuimarisha matumizi endelevu.

Mheshimiwa Spika, Rasilimali za Maji Shirikishi: Usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi ni moja ya maeneo muhimu katika ushirikiano na nchi jirani. Lengo ni kuhakikisha kuwa rasilimali ya maji shirikishi inatumika kwa njia endelevu na kwa manufaa ya nchi husika.

Mwaka 2006/2007 nchi yetu iliendelea na majadiliano ya kuweka mfumo mpya wa ushirikiano katika matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwenye mabonde ya maji ya Mto Nile, Mto Zambezi na mto Ruvuma. Aidha, Wizara yangu iliendelea kuratibu Mradi wa Hifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria unaotekelezwa kwa pamoja na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na uratibu wa Awamu ya Pili ya Miradi ambayo itazijumuisha nchi za Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji mwaka 2006/2007: Wizara yangu iliendelea kutekeleza mkakati wa kuhifadhi ardhi na kutunza vyanzo vya maji katika mabonde yote tisa. Katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendesha zoezi la kubaini vyanzo mbalimbali vya maji na kuweka mikakati ya kulinda vyanzo hivyo dhidi ya uchafuzi unaotokana na majitaka ya viwandani na majumbani. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kuhifadhi ardhi na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Kuhakiki Ubora na Usafi wa Maji: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kuhakiki ubora na usafi wa maji ambapo jumla ya sampuli 3,058 za maji zilichunguzwa kemikali na vijidudu kwa kutumia maabara 16 zilizopo nchini. Matokeo yalionyesha kwamba asilimia 90 ya sampuli za maji zilizochunguzwa zilikuwa na viwango vinavyokubalika kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini: Maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007 kuhusu eneo la Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 43 hadi 57 ya Hotuba yangu

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuunda na kuimarisha vyombo vya watumiaji

maji. Lengo la kuunda na kuimarisha vyombo hivyo ni kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi wa Miradi ya Maji Vijijini: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilikamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kuvipatia huduma ya maji vijiji 46 katika mkoa wa Pwani na Morogoro ikiwa ni hatua za utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji wa Chalinze. Pia Wizara ilikamilisha usanifu wa miradi ya maji katika vijiji 20 kwenye mikoa ya Pwani na Dar es Salaam na kukamilisha upembuzi yakinifu katika vijiji 45 mkoani Mwanza na vijiji 19 mkoani Mara. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kusanifu na kutayarisha makabrasha ya zabuni za ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji 20 katika mikoa ya Pwani na Dar es salaam na usanifu wa awali wa miradi ya maji katika mikoa ya Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji Vijijini: Katika mwaka 2006/2007, jumla ya miradi 21 ilikarabatiwa katika maeneo ya Sumve Mantare, Nyang'hanga/Kabila, Mwanhuzi, Bariadi mjini, Wakichi Kibena, Gabimori, Lushoto mjini, Kayanga Mjini, Ubembe Kwemhosi, Iringa Vijijini, Mugango/Kiabakari, Maswa mjini, Njombe Vijijini, Makonde, Wanging'ombe, Same mjini, Mwanga mjini, Sengerema mjini, Kilwa Masoko, Tunduru mjini, na Sikonge mijini.

Miradi iliyopanuliwa ni katika maeneo ya Madibira, Lesingita, Bunda mjini, Nyamuswa, Malya, Lyamungo, Mrama, Tella, Usari, Urori, Kimashuku, Kifuni, Umbwe, Kindi, Sambarai, Mkomongo, Kombo na Manushi. Pia, ujenzi wa miradi ya maji katika mikoa ya Lindi na Mtwara ulikamilika na watu wapatao 200,000 wananufaika na huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2007/2008, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji vijijini utatekelezwa na Halmashauri kupitia mipango na bajeti zao. Aidha, mahitaji ya fedha na mpango wa kuziwezesha Halmashauri hizo kutekeleza miradi hiyo yameainishwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huo unatekelezwa katika wilaya 14 za Rufiji, Morogoro Vijijini, Mvomero, Kilosa, Kongwa, Mpwapwa, Kondoa, Manyoni, Singida Vijijini, Iramba, Igunga, Kiteto, Kilindi na Handeni.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa iliendelea na upembuzi yakinifu wa kubaini vyanzo vya maji na viwango vya mahitaji ya maji katika miji midogo 9 ya Utete, Ikwiriri, Kibiti, Mvomero, Turiani, Kilosa, Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itasanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni za ujenzi wa miradi ya maji katika miji yote 9.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Mabwawa: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilipanga kujenga mabwawa 21 na kuendelea na ujenzi wa bwawa la Mugumu. Hadi sasa ujenzi wa mabwawa mapya 9 unaendelea kutekelezwa katika maeneo ya Ugunga

(Urambo), Moita na Ingamuriak (Monduli), Nyashitanda (Misungwi), Habiya (Bariadi), Nyambele na Kinyambwiga (Bunda), Matwiga (Chunya) na Iguluba (Iringa Vijijini). Aidha, mikataba ya ujenzi wa mabwawa 3 mapya katika maeneo ya Amasatwa (Kiteto), Emboret (Simanjiro) na Katoro (Geita) imesainiwa na wakandarasi wapo katika hatua za kupeleka vifaa vya ujenzi. Tathmini ya zabuni za ujenzi wa mabwawa mengine mapya 9 katika maeneo ya Masuguru (Bagamoyo), Seke Ididi (Kishapu), Nyambori (Tarime), Sasajila (Dodoma Vijijini), Mwanjoro (Meatu), Wegero (Musoma Vijijini), Ingodin (Longido), Mnazi Mmoja (Monduli) na Bulenya (Igunga) imekamilika na wakandarasi wameteuliwa, na taratibu za kusaini mikataba zinaendelea. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na ujenzi wa mabwawa hayo.

Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) ilichimba visima virefu 429 na kati ya visima hivyo, 364 vina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo milioni 32 kwa mwaka. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu, chini ya *Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji* itaendelea kuimarisha Wakala huo.

Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Skimu Kubwa za Maji Vijijini: Mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuendesha skimu kubwa za maji za Maswa, Handeni, Makonde, Chalinze, Wanging'ombe na Mugango/Kiabakari kwa kulipia matumizi ya umeme, fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa mradi wa maji Chalinze, ununuzi wa vipuri vya mitambo na kulipia mafao ya vibarua. Mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara chini ya *Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji* itaendelea kugharamia matengenezo na uendeshaji pamoja na kuanza kutafuta njia sahihi za kuziwezesha skimu hizo kujiendesha zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini: maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007 kuhusu eneo la Huduma za Maji na Uondoaji wa Majitaka Mijini yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 58 hadi 80 ya Hotuba yangu

Mheshimiwa Spika, Uandaaji wa Miradi ya Majisafi na Majitaka Mijini: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilichunguza mahitaji ya huduma za maji kwa lengo la kuandaa mpango wa muda mrefu wa kukarabati na kupanua mifumo ya majisafi na ujenzi wa mifumo ya uondoaji wa majitaka (*Urban Upgrading Program*) katika miji tisa ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Bukoba, Musoma , Kigoma, Dodoma na Tabora. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kutumia matokeo ya uchunguzi huo, itasanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni za ujenzi ikiwa ni pamoja na kuanza kutekeleza kazi za dharura ili kuboresha mifumo ya maji kwenye miji iliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi na Ukarabati wa Miradi ya Majisafi na Majitaka Mijini: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Makazi la Umoja wa Mataifa iliboresha huduma za maji mjini Bukoba. Katika mwaka 2007/2008 uboreshaji huo utaendelea kwa kukarabati chanzo cha maji na kujenga matangi matatu ya kuhifadhi maji katika maeneo ya Kashura, Magoti na Rwamishenye na kujenga vioski 25 vya maji kwenye maeneo mbalimbali katika mji huo. Pia, Wizara

yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), iliendelea kuboresha huduma za maji katika miji ya Mwanza, Mbeya, Iringa, Songea na Singida.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Kahama na Shinyanga: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga. Mradi huo ambao unagharamiwa na Serikali yetu, utavipatia maji vijiji 54 vilivyoko umbali usiozidi kilomita tano kutoka kwenye bomba kuu katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Hadi kufikia mwezi Juni 2007, utekelezaji wa mradi huo ulifikia asilimia 88 na tunatarajia kuukamilisha katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Majisafi na Majitaka Jijini Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Rasilimali ya Ulaya iliendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za majisafi na majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, wingi wa maji katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo umeendelea kupungua wakati wa kiangazi na hivyo kuathiri uzalishaji wa maji katika mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kuchunguza vyanzo vipya vya maji juu na chini ya ardhi. Matokeo ya uchunguzi yamependekeza kujengwa bwawa katika mto Ruvu maeneo ya Kidunda Wilayani Morogoro na uchimbaji wa visima virefu katika maeneo ya Kimbiji na Mpera.

Mheshimiwa Spika, *DAWASCO* imeendelea kutoa huduma ya maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Huduma hiyo inaendelea kuimarika kutokana na ukarabati wa vyanzo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na Mtoni.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*): *EWURA* ilianzishwa kwa Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na ilianza kazi mwezi Juni 2006. Katika mwaka 2006/2007, EWURA iliendelea kujijengea uwezo wake wa kitaasisi kwa kuajiri watumishi 52 wa fani mbalimbali. Aidha, *EWURA* iliandaa sheria ndogo za kukusanya mapato kwa lengo la kuiwezesha ijitegemee kifedha kwa mujibu wa sheria. *EWURA* inatekeleza majukumu makuu manne kama ifuatavyo:-

(a) Kutoa leseni kwa watoa huduma katika sekta za maji na nishati;
(b) Kukagua miundombinu ya maji, umeme, gesi asilia na bidhaa za petroli;
(c) Kuchochea ushindani katika sekta za maji na nishati; na
(d) Kudhibiti bei za huduma za maji na nishati.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha udhibiti wa sekta za maji na nishati, katika mwaka 2007/2008, Serikali itawasilisha Bungeni miswada minne ya sheria za: *Water Supply Act, Electricity Act*, *Petroleum Supply Act*, na *Natural Gas Supply Act.*

Kutungwa kwa sheria hizo kutaimarisha usimamizi na kutaiwezesha *EWURA* kutekeleza kikamilifu majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Masuala Mtambuka: Maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007 kwa eneo la Masuala Mtambuka yameainishwa kwa kina kuanzia Aya ya 81 hadi 92 ya Hotuba yangu

Mheshimwa Spika, Mafunzo ya Watumishi na Wataalam wa Sekta ya Maji: Chuo cha Maji: Mwaka 2006/2007, Chuo cha Maji kiliendelea kutoa mafunzo yanayolenga kutosheleza mahitaji ya wataalam katika Halmashauri za Wilaya na taasisi nyingine. Aidha, katika mwaka huo Chuo kilikuwa na wanafunzi 57 wa mafunzo ya cheti cha ufundi sadifu na wanafunzi 123 katika mafunzo ya stashahada.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maji, itaendelea kutoa mafunzo ya ufundi katika mfumo wa tuzo za kitaifa za elimu ya ufundi (*NTA system*) chini ya uangalizi wa *NACTE*, na kitasajili wanafunzi wapya 77 wa mafunzo ya stashahada na wanafunzi 300 wa mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Watumishi: Wizara yangu ina jumla ya Watumishi 2,069. Mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliajiri watumishi 220 na kati ya hao 98 ni Wahandisi walioajiriwa kwa mkataba kwa lengo la kuzijengea uwezo Halmashauri, na Sekretarieti za Mikoa kwa lengo la kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Aidha, watumishi 16 walithibitishwa kazini, watumishi 598 walipandishwa vyeo na watumishi 123 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na wataalam wa sekta ya maji kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.Mheshimiwa Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano:-

Mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilianzisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kwa lengo la kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na wadau wa sekta ya maji, kuelimisha jamii na kutoa elimu kuhusu Sera ya Maji, Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Maji, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na masuala ya utendaji na uendeshaji.

Mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kuimarisha kitengo hicho na kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Rushwa, Jinsia na UKIMWI: Vita dhidi ya Rushwa: Mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa. Utekelezaji huo ulilenga kuziba mianya ya rushwa katika maeneo ya manunuzi na ajira kwa kuzingatia taratibu za ushindani ulio wazi katika ajira na manunuzi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Menejimenti Katika Utumishi wa Umma na Sheria ya Manunuzi, Na.4 ya mwaka 2004. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika sekta ya maji kwa kuweka

mkazo kwenye mafunzo ya vita dhidi ya rushwa na utawala bora kwa watendaji wa ngazi mbalimbali na wadau ili kuboresha utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Jinsia: Wizara yangu inatambua umuhimu wa kutoa fursa iliyo sawa kwa jinsia zote katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA sambamba na utekelezaji wa Sera ya Maji. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kutoa fursa kwa jinsia zote katika masuala ya ajira, upandishwaji vyeo, mafunzo na uwakilishi katika kamati na bodi mbalimbali za sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mapambano dhidi ya UKIMWI: Suala la UKIMWI limeendelea kupewa kipaumbele na ni moja ya ajenda katika matukio muhimu ya sekta ya maji. Mwaka 2006/2007 Wizara yangu iliendelea na vita dhidi ya UKIMWI kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kupambana na Janga la UKIMWI. Jumla ya watumishi 787 walipata mafunzo ya mbinu za kujikinga na maambukizi na kuwahamasisha kupima afya zao mapema ili waweze kupatiwa msaada kwa wale watakaobainika kwamba wameathirika. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na kampeni ya kuhamasisha watumishi kutumia mbinu za kujiepusha na maambukizo ya virusi vya UKIMWI, kuwahimiza kupata ushauri nasaha na upimaji wa hiari. Watumishi watakaobainika kuwa na virusi vya UKIMWI na ambao watajitokeza watapatiwa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji: Baada ya kutoa taarifa ya mapitio ya utekelezaji ya mwaka 2006/2007 na baadhi ya malengo ya mwaka 2007/2008 naomba nielezee Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo itaanza kutekelezwa rasmi katika mwaka huu wa fedha. Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu ilikamilisha maandalizi ya Programu hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Washirika wa Maendeleo ambao wamekubali kuchangia gharama za utekelezaji. Ili kurahisisha utekelezaji wa Programu hiyo, Serikali imeandaa utaratibu wa kutuma fedha moja kwa moja kwa watekelezaji, ambao ni Serikali za Mitaa; Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini; Ofisi za Mabonde ya Maji; na Asasi zisizo za kiserikali. Programu hiyo imegawanyika katika programu ndogo nne kama ifuatavyo:-

(a) Programu Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji: Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaimarisha uwezo wa Ofisi za Mabonde yote tisa pamoja na Bodi zake kwa lengo la kuboresha na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji. Kwa kushirikiana na wadau wa mabonde ya maji ya Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu, Ziwa Victoria na Bonde la Kati, Wizara yangu itatayarisha mipango shirikishi ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Mipango hiyo italenga katika kukidhi mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika mabonde hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Mabonde ya Maji ndiyo zitakuwa waandaaji wa mipango na watekelezaji wa kazi za usimamimizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kulingana na mahitaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Ili kuziwezesha ofisi hizo kutekeleza kikamilifu majukumu yake, Wizara yangu itazijengea uwezo kwa

kuzipatia vitendea kazi, kujenga na kukarabati majengo ya ofisi na kuimarisha mawasiliano.

(b) Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini: Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Washirika wa Maendeleo ilikamilisha hatua za awali za kutekeleza Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri za Wilaya;

(ii) Kubaini miradi itakayoleta matokeo ya haraka (*quick-wins*); na

(iii) Kutoa miongozo ya utekelezaji katika ngazi za kijiji, wilaya, mkoa na taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha hatua hizo za awali, kuanzia mwaka huu wa fedha 2007/2008, Programu Ndogo ya Maji na Usafi Mazingira Vijijini itaanza kutekelezwa katika wilaya zote nchini. Utekelezaji wake utakuwa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa kwa kuzingatia mpango wa Serikali wa kukasimia rasilimali na madaraka kwenye ngazi za Serikali za Mitaa. Halmashauri hizo zitawajibika kujipangia miradi ya maendeleo ya maji kulingana na mipango na vipaumbele walivyojiwekea katika kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo yao. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kupitia Sekretariati za Mikoa itabakia na jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji kwa kuzingatia utaratibu na makubaliano *(Participation Agreement)* yaliyofikiwa kati ya Serikali Kuu na Halmashauri hizo, katika kutekeleza Programu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu huo wa kuwezesha na kukasimia madaraka kwenye Serikali za Mitaa, kuanzia mwaka 2007/2008, fedha za kutekeleza miradi ya maji ya maendeleo katika Halmashauri zitatumwa wilayani chini ya Utaratibu wa Kuzipatia Ruzuku za Maendeleo Halmashauri *(Local Government Capital Development Grant System (LGCDG)*. Vigezo vya kugawa fedha kwa kila Halmashauri tayari vimewekwa kutokana na majadiliano na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Wizara yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Wizara ya Fedha. Vigezo vya kugawa fedha kwa kila Halmashauri ni pamoja na kuzingatia idadi ya watu ambao bado hawajapata huduma ya maji na aina ya teknolojia inayotumika katika miradi ya maji katika kila wilaya. Vigezo hivyo ni juhudi za makusudi za Serikali kuinua viwango vya huduma ya maji katika wilaya ambazo huduma hiyo iko chini ili kuleta uwiano wa huduma katika wilaya zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuziwezesha Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa kutekeleza kikamilifu majukumu ya kuendeleza na kusimamia miradi ya maji katika maeneo yao, Wizara yangu kuanzia mwaka 2007/2008 itazipatia vifaa na nyenzo za kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na magari, pikipiki, kompyuta, na vifaa mbalimbali vya ofisi na mawasiliano. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itatoa mafunzo ya kukuza uelewa wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya

Maji kwa Halmashauri na kusaidia upatikanaji wa wataalam ikiwa ni pamoja na wahandisi katika ngazi za wilaya na mikoa ili kuziwezesha kuongeza ufanisi wa kutekeleza miradi ya maji kwa kuzingatia mahitaji ya kila Halmashauri.

(c) Programu Ndogo ya Majisafi na Majitaka Mijini: Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 Wizara itapanua na kukarabati mifumo ya majisafi ya miji ya Tabora na Dodoma kwa kubadilisha mtandao wa mabomba ya usambazaji maji uliochakaa katika mji wa Tabora na kupanua mtandao wa mabomba ya kusambaza maji kwenye makazi mapya mjini Dodoma ikiwa ni pamoja na eneo la Chuo Kikuu kipya cha Dodoma. Pia Wizara itaanza taratibu za kuanza ujenzi wa mfumo wa majisafi katika mji wa Singida na kuendelea na ujenzi wa mifumo ya majisafi na majitaka katika Manispaa ya Songea na Jiji la Mbeya na ukarabati wa miradi ya maji katika Jiji la Mwanza na Manispaa ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu itachunguza mahitaji ya huduma za majisafi na majitaka kwa lengo la kuboresha na kupanua huduma hizo ili kukidhi ongezeko la mahitaji hadi mwaka 2025. Uchunguzi huo utahusu uongezaji wa vyanzo vya maji, ujenzi wa mitambo ya kusafishia majisafi, ujenzi wa mabwawa ya kusafishia majitaka na upanuzi wa mifumo ya majisafi na majitaka katika miji ya Tanga, Moshi, Arusha, Dodoma, Morogoro, Tabora, Iringa, Mbeya, Shinyanga, Songea na Singida. Aidha, Wizara ikishirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kiufundi la Ujerumani (*GTZ*) itatafiti uwezekano wa kuunganisha uendeshaji wa huduma za mamlaka zaidi ya moja (*clustering*) kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea na mpango wa kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka za Maji Mijini katika makao makuu ya mikoa. Chini ya mpango huo Mamlaka za Maji Mijini zitakuwa ndio waandaji wa mipango na watekelezaji wa kazi za kuboresha huduma za maji mijini kulingana na mahitaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Ili kuziwezesha Mamlaka hizo na *DAWASA* kutekeleza majukumu yake, Wizara yangu itagharamia ukarabati wa ofisi, ujenzi wa ofisi mpya, ununuzi wa magari na pikipiki, vitendea kazi na ujenzi wa mifumo ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itazijengea uwezo ofisi za maji za miji 35 ya wilaya kwa kuwapatia mafunzo wataalam wake, kukarabati na kujenga majengo ya ofisi, kununua vifaa vya ofisi, usafiri na mawasiliano. Miji hiyo ni Ngorongoro, Kilolo, Makete, Kayanga, Kasulu, Kilwa Masoko, Nachingwea, Masasi, Orkesumet, Karatu, Katesh na Mugumu. Miji mingine ni Bunda, Tarime, Vwawa, Dakawa, Tandahimba, Newala, Nansio, Misungwi, Sengerema, Kisarawe, Kilindoni, Mkuranga, Mbinga, Mhunze, Ushirombo, Kiomboi, Sikonge, Geita, Urambo, Igunga, Handeni na Pangani Vilevile, chini ya mpango huo utekelezaji wa miradi ya dharura itakayolenga kuboresha huduma za maji katika miji hiyo utafanyika. *(Makofi)*

(d) Programu Ndogo ya Kuimarisha Asasi za Sekta ya Maji na Kujenga Uwezo: Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaimarisha na kujenga

uwezo wa kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika ngazi ya kitaifa kama ifuatavyo:-(i)Kuzipatia vifaa, nyenzo, na kukarabati na/au kujenga majengo ya ofisi na kuweka samani;

(ii) Kuboresha mtandao wa mawasiliano na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa vifaa na nyenzo hizo;

(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara na Sekretariati za Mikoa;

(iv) Kuzijengea uwezo taasisi zisizo za kiserikali na taasisi za kijamii zinazojishughulisha na maendeleo ya sekta ya maji; na

(v)Kuzijengea uwezo Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, Shukurani: napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kuwa mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2006/2007 ni jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha.

Napenda kuzishukuru Serikali za nchi za Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Denmark, Uswisi, Ireland, Ubeligiji, Uingereza, Korea ya Kusini, Sweden, Norway na Marekani. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa za Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya, Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP, UN Habitat* na *UNICEF* na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, kwa misaada na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Aidha, nayashukuru Mashirika ya kidini ya *World Islamic League,* Shirika la *Al Munadhanat Al Dawa Al Islamia,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania, pamoja na Taasisi za *WaterAid*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili (*IUCN*), *World Wildlife Fund* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuisaidia Sekta ya Maji katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako nitumie fursa hii kutoa shukurani za pekee kwa wananchi wote na wadau wengine ambao sikuweza kuwataja mmoja mmoja kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza Sera ya Maji. Pia, shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge kutokana na michango yao wanayotoa ndani na nje ya Bunge hili inayolenga kuboresha sekta ya maji nchini. Naomba waendelee na moyo huo ili kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara yangu.

Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha hali ya maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga, Mbunge Viti Maalum kwa msaada na ushirikiano wake. Aidha, napenda pia, nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Christopher Sayi, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Mashirika na Taasisi chini ya Wizara yangu pamoja na wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Bagamoyo kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kutoa shukurani zangu za dhati kwa mke na familia yangu kwa kunipa moyo na ushirikiano na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mbalimbali ya Kitaifa yanayonikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maombi Ya Fedha Kwa Mwaka 2007/2008 Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni mia mbili thelathini na nane , milioni mia nne kumi na nane, laki sita na sitini na saba elfu na mia sita (238,418,667,600) kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008.

Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia nne ishirini na saba, laki tisa na kumi na tano elfu (13,427,915,000) ambapo Shilingi bilioni nne, milioni mia sita sitini na mbili na laki tatu na themanini na tisa elfu (4,662,389,000) ni Mishahara ya Watumishi (PE), na Shilingi bilioni nane, milioni mia saba sitini na tano, laki tano na ishirini na sita elfu (8,765,526,000) ni fedha za Matumizi Mengine (OC).

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi bilioni mia mbili ishirini na nne, milioni mia tisa tisini, laki saba na hamsini na mbili elfu na mia sita (224,990,752,600), ambapo kati ya hizo Shilingi bilioni sabini, milioni mia saba na hamsini na nne, na elfu nne (70,754,004,000) ni fedha za ndani na Shilingi bilioni mia moja na hamsini na nne, milioni mia mbili na thelathini na sita, laki saba na arobaini na nane elfu na mia sita (154,236,748,900) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia, inapatikana katika Tovuti ya Wizara yangu kwa anwani: *www.maji.go.tz*. Na kabla sijamaliza, naomba nitambue uwepo wa Mrs. Rona Maneno ambaye taarifa yake ilikufiia lakini kwa bahati mbaya hukuweza kumtambua. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, na mimi naomba Mheshimiwa Maneno aniwie radhi, leo majina ya wageni yalikuwa mengi na jina la Mkewe Mbunge wa Chalinze, Mama Rona Maneno, likanipita kwa bahati mbaya. Ninaambiwa sasa hivi ametoka, lakini ilichukuliwe rasmi kwenye *Hansard* kwamba alikuwapo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji 12 na kama kawaida tutaanza na wale ambao hawajachangia. Orodha hii haiwezi kuongezeka. Kwa hiyo, kuleta jina sasa haisaidii sana kwa sababu ni Wizara ambayo inajadiliwa kwa siku moja tu.

Kwa hiyo, majina niliyo nayo hapa ni Mheshimiwa Charles Kajege na Mheshimiwa Ruth Nkya, hawa ndio watatangulia kwa sababu hawajachangia katika hotuba yoyote. *(Makofi)*

Waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Paschal Degera ambaye amewasili, karibu sana Mheshimiwa Degera. Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. Wibrod Slaa, Mheshimiwa Annia Chaurembo, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika. Hawa tisa pengine itawezekana.

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia mara mbili, sidhani kama tutawafikia, nao ni Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Peter Serukamba na huyu wa mara ya tatu ni Mheshimiwa Juma Kilimbah ndiyo vigumu kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa kwa mtiririko huo, nitamwita Mwenyekiti wa Kamati kuanza.

Nilikuwa natoa taarifa hiyo ili wajiandae. Naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa ajili ya Maoni ya Kamati.

Kwa niaba ya Mwenyekiti, naona nakuja Mheshimiwa Mpendazoe. Hii ndiyo raha ya kuwa na Wenyeviti waliotulia kama Mheshimiwa Gideon Cheyo, hana papara na anagawa madaraka kwa wenzie. *(Makofi).*

**MHE. FRED M. TUNGU (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) Toleo la mwaka 2004, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha uliopita (2006/2007), pamoja na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na

ushauri wa Kamati kwa niaba yake na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kutoa pole kwa wazazi, ndugu na jamaa wote kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, ilikutana Dar es Salaam tarehe 4 Juni, 2007 ili kuchambua na kutathmini utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Ili kutekeleza jukumu hilo Kamati ilizingatia utaratibu ufuatao:-

(i) Kupitia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati iliyochambua Bajeti ya mwaka uliopita (2006/2007).

(ii) Kuchambua utekelezaji wa malengo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

(iii) Kuchambua na kupitia kazi zilizopangwa kufanyika mwaka wa fedha 2007/2008 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita, Kamati iliridhika na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati ilioutoa wakati ilipochambua Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita. Aidha, Kamati ilitoa ushauri ili kuboresha na kuongeza kasi katika utoaji wa huduma za majisafi mijini na vijijini na utunzaji wa vyanzo vya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo mafanikio kadhaa katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka uliopita wa 2006/2007. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Serikali ilikamilisha na kuanza kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya maji nchini na kukamilisha uandaaji wa programu ya kuendeleza sekta ya maji ya mwaka 2006 hadi 2025. Utekelezaji wa mkakati na programu ya maji nchini utawezesha kukabiliana na matatizo sugu katika sekta ya maji na kuwezesha mipango na Bajeti kuangalia kwa ujumla sekta nzima badala ya kuangalia mpango wa mradi mmoja mmoja.

(ii) Serikali iliendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji zaidi ya 50 ambavyo vimeainishwa katika awamu hii ya kwanza ya utekelezaji.

(iii) Upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 55.7 mwaka 2006/2007 na kwa upande wa mijini huduma ya majisafi imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2005/2006 hadi kufikia asilimia 78 mwaka 2006/2007.

Ongezeko hili ni sawa na asilimia 4 kwa mwaka, kiwango ambacho kinazingatia kabisa malengo ya MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ambapo ongezeko lilikisiwa kuwa asilimia 3.2 kwa wakazi wa mijini kwa mwaka. Mafanikio haya yanapita hata mipango iliyokuwa imeelezwa katika Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine hadi kufikia mwezi Mei 2007, ujenzi wa mabwawa tisa ulikuwa umekwishaanza na kufikia hatua mbalimbali za utekelezaji katika Wilaya za Urambo, Monduli, Misungwi, Bariadi, Bunda, Chunya, Iringa Vijijini, Kiteto, Simanjiro na Geita. Aidha, tathmini ya zabuni za ujenzi wa mabwawa tisa zilitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2007 katika Wilaya za Bagamoyo, Kijiji cha Sekididi Wilaya ya Kishapu, Tarime, Dodoma, Wilaya za Meatu, Musoma Vijijini, Longido, Monduli na Igunga. *(Makofi)*

(v) Mafanikio mengine ni kwamba visima virefu 429 vilichimbwa na kuvuka lengo lililowekwa la kuchimba visima virefu 410. *(Makofi)*

(vi) Vile vile mafanikio mengine ni uchunguzi wa upatikanaji wa maji chini ya ardhi ulifanyika katika maeneo 850 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Lindi, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

(vii) Vile vile mamlaka za majisafi na majitaka mijini ziliendelea kuimarishwa kwa kukarabati na kupanua miundombinu ya mifumo ya majisafi. Uzalishaji wa maji umeongezeka na muda wa upatikanaji wa huduma ya maji umeongezeka katika maeneo mengi zaidi. Asilimia 78 ya wakazi wa mijini hivi sasa wanapata huduma ya maji safi kwa wastani wa saa 17 kila siku, tofauti na ilivyokuwa asilimia 74 na muda wa huduma wa saa 16 kwa siku mwaka 2005/2006.

(viii) Vile vile makusanyo ya maduhuli nayo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 21.5 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 24.2 mwaka 2006/2007. Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa maji nayo imeongezeka kutoka wateja 183,518 mwaka 2005/2006 hadi wateja 193,300 mwaka 2006/2007.

Aidha, kutokana na jitihada za kufunga dira za maji kutoka 142,401 mwaka 2005/2006 hadi 156,915 mwaka 2006/2007 umesaidia kupunguza upotevu wa maji kutoka wastani wa asilimia 41 hadi 39 mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio hayo niliyoyataja na ambayo sikuyataja hapa yamekuwepo matatizo na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Utunzaji wa vyanzo vya maji nchini unaathirika kwa kiwango kikubwa na vitendo vya uvamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya kuhifadhi mazingira.

(ii) Changamoto nyingine ni kwamba uchakavu wa vifaa katika maabara za Mikoa unaosababisha kutowezesha kupima na kuhakiki kwa ukamilifu ubora na usafi wa maji.

(iii) Vile vile kuna upungufu wa wataalamu na vifaa katika ngazi ya Wilaya unaosababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maji.

(iv) Pia mtandao wa kutathmini na kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ni mdogo na haukidhi mahitaji ya kusanifu miradi ya maji.

(v) Aidha, gharama kubwa za kuendeshea mitambo ya maji na dawa inayosababisha gharama za maji kuwa kubwa kwa watumiaji wa maji Mijini na Vijijini.

(vi) Vile vile sekta ya maji haivutii wawekezaji binafsi kutokana na gharama kubwa za uwekezaji kwenye miundombinu ya maji na ukweli kwamba huduma za maji ni za mwelekeo wa huduma za kijamii zaidi kuliko za biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imepanga kufanya kazi kadhaa zenye lengo la kuhakikisha kwamba rasilimali za maji zinaendelezwa, zinasimamiwa na kutumika kwa njia endelevu na kwa kuwashirikisha wadau wote. Baadhi ya kazi hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga, pamoja na vijiji vilivyokwisha ainishwa katika awamu hii ya kwanza ya utekelezaji.

(ii) Pia kuendelea na uchimbaji na ujenzi wa mabwawa ili kuongeza upatikanaji wa maji nchini hasa katika maeneo kame.

(iii) Kuendelea kuboresha huduma ya majisafi na majitaka mijini.

(iv) Kuendelea kubaini na kufuatilia ubora wa maji katika mabonde mbalimbali hapa nchini. Wizara itazifanyia uchunguzi sampuli 1,500 za maji kutoka vyanzo mbalimbali nchini ifikapo mwaka 2009.

(v) Kuendelea na usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji nchini na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea kwa ufupi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka uliopita 2006/2007 na matarajio kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Kamati inaipongeza Serikali kubuni na kuendeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Shinyanga na Kahama. Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni ya makandarasi kwa wakati ili kuepuka ongezeko la deni na riba. Aidha, Serikali iendelee kuzingatia maombi mbalimbali yaliyotolewa kuhusu kuvihusisha/kuviingiza vijiji kadhaa ambavyo viko nje ya kilometa tano ya njia ya mabomba ya mradi huu katika awamu zitakazofuata, mfano kijiji cha Mwanhili,

Itongutale na Mwasubi ambavyo viko katika kata ya Mbunambio Wilaya ya Kishapu, pamoja na vijiji vilivyoko ndani ya kilometa tano ambavyo vilisahaulika mfano kijiji cha Mahando na Mwamazengo vilivyoko Wilaya ya Misungwi.

(ii) Kwa kuzingatia idadi kubwa ya watu katika Jiji la Dar es Salaam, wingi wa viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali na kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam ndiyo kitovu cha biashara nchini hivyo kusababisha matumizi makubwa ya maji, Serikali iongeze kasi ya kushughulikia tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iharakishe ujenzi wa bwawa la Kidunda na kutoa kipaumbele zaidi.

(iii) Ofisi za mabonde ya maji ni mamlaka muhimu za kuimarisha, kutunza na kulinda vyanzo vya maji nchini. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuzijengea uwezo kwa kuzipa rasilimali mfano watu, fedha, vitendea kazi vya kutosha ili ziendelee kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika maeneo yao.

(iv) Kutokana na uchafuzi wa vyanzo vya maji nchini unaosababishwa na utupaji majitaka kutoka viwandani na kwenye makazi ya watu mijini, Kamati inaishauri Serikali ifanye ukarabati na kupanua miundombinu ya majitaka ili kuiboresha na kuiimarisha mifumo hiyo.

(v) Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni na kuanzisha mradi mkubwa wa Kitaifa wa Maji na Usafi wa Mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo ambao umewapa wananchi matumaini makubwa kote nchini.

Kwa kuwa mradi huu unategemea kwa asilimia kubwa fedha za nje ambazo huchelewa kuletwa, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kubuni mbinu za kutegemea zaidi fedha za ndani ili kupunguza athari katika utekelezaji.

(vi) Ili kukabiliana na tatizo la maji katika maeneo kame nchini, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza mpango wa ujenzi wa mabwawa na uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo kame nchini, ziongezwe na zisambazwe katika Taasisi mbalimbali kuwa na mipango ya kuvuna maji ya mvua. Aidha, Serikali iimarishe huduma za wakala wa maji ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

(v) Kutokana na upungufu wa watalaamu wa maji nchini hususan katika Halmashauri za Wilaya, Kamati inaishauri Serikali iendelee kukiimarisha na kukiboresha Chuo cha Maji cha Rwegarulila ili kiweze kutoa mafunzo ya watalaamu wenye shahada za taaluma ya maji. Mpango huo uwe endelevu ili hatimaye wapatikane wataalamu wa kutosha na kuajiriwa katika Halmashauri zote. *(Makofi)*

(vii) Pia kutokana na ukweli kwamba wawekezaji wengi hawavutiwi sana kuwekeza katika miradi ya huduma za Maji, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mikakati wa kuwavutia wawekezaji binafsi katika sekta ya maji. Mazingira yaendelee kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuharakisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maji Kitaifa kama njia endelevu ya kuwapatia wananchi huduma ya maji Mijini na Vijijini. *(Makofi)*

(viii) Pamoja na kutambua kwamba Wizara hii ni kati ya Wizara zilizopewa kipaumbele katika mgao wa Bajeti ya Serikali katika mwaka huu wa fedha, bado kiwango kilichotengwa kwa Wizara hii ni kidogo. Matatizo yapo mengi na ahadi za miradi ya maji zipo nyingi sehemu mbalimbali hapa nchini. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa Wizara hii na kuiongezea fedha katika Bajeti mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa maji katika nyanja au sekta zote za uchumi mfano sekta ya madini, kilimo, mifugo na sekta zinazohusu ustawi wa jamii kama afya na elimu, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuipa kipaumbele sekta ya maji miongoni mwa sekta za elimu, afya, barabara na kilimo zilizopewa kipaumbele katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zinazoikabili sekta ya maji, mfano kubadilika kwa hali ya hewa kunakoambatana na ukame katika maeneo mengi nchini, ongezeko la watu nchini, ongezeko la uzalishaji mali hasa viwandani na uharibifu wa vyanzo vya maji, Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuipa kipaumbele zaidi sekta ya maji kuliko ilivyo sasa kwa kuitengea fedha za kutosha ili kuhakikisha rasilimali za maji nchini vyanzo vya maji zinatunzwa na kuendelezwa na kukamilisha miradi mbalimbali iliyoanzishwa ili kuwaondolea wananchi kero ya kutopatikana kwa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Bajeti ya Wizara na baada ya kuridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake, kwa kauli moja Kamati ilipitisha Bajeti ya Wizara. Kwa hiyo Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maji Fungu la 49, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi 13,427,915,000/= na matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 224,990,752,600/=.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao wakati Kamati ilipochambua na kupitia Bajeti ya Fungu 49 - Wizara ya Maji. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Kwanza Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati,. Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Chacha Wangwe na Mheshimiwa Fred Mpendazoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha taarifa hii kwa kumshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipa Kamati hii, kila tunapokutana na Wizara. Aidha, nawapongeza watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa na Naibu Katibu Mkuu Bwana Christopher Sayi kwa ushirikiano wao wakati Kamati ilipochambua Bajeti ya Fungu 49 - Wizara ya Maji. Nawashukuru kwa mara nyingine tena Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa ushirikiano na ustahimilivu wao ambao umefanikisha kazi hii muhimu. *(Makofi)*

Naomba pia kutumia fursa hii, kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa ushirikiano wao wanaonipa ninapokuwa jimboni. *(Makofi)*

Mwisho napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damiani S. L. Foka, kwa ushirikiano wake mzuri anaotoa kwa Kamati na Katibu wa Kamati hii Ndugu Frank Mbumi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, umesoma vizuri kwa utulivu. Namuita sasa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel. Wakati Mheshimiwa Meryce anakuja ningependa tu Waheshimiwa Wabunge mfahamu kwamba masuala ya maji yako rohoni mwake kwa sababu mmewe ni Mhandisi wa Maji. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa hai na wazima. Pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) kwa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na maafa na majanga mbalimbali ambayo yote ni miongoni mwa mitihani yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tuwaombee wenzetu wote waliokwishatangulia makazi mema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia ya hayati Mheshimiwa Amina Chifupa. Marehemu alikuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya vijana wa Kitanzania na Watanzania kwa ujumla. Marehemu alikuwa ni miongoni mwa watu shupavu na asiyeogopa kusema ukweli, namuomba Mwenyezi Mungu ampe makazi mema.*Amin.*

Mheshimiwa Spika, kila mtu anajua kuwa maji ni uhai. Takribani asilimia 79 ya mwili wa mwanadamu unategemea maji, sayari yetu ya dunia asilimia 75 imezungukwa na maji. Inakisiwa katika eneo la wastani wa 2500 maili. Kaskazini na Kusini ya *Equator* huzalisha maji yatokanayo na unyevu ambayo ni mara mbili ya maji yote yalioko kwenye bahari, maziwa na mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili lina wastani wa wakazi wasiopungua asilimia 70% ya wakazi wote wa dunia na ndio wenye matatizo makubwa ya maji yalio salama. Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla maji mengi kuliko nchi nyingi katika Bara la Afrika. Tumezungukwa na maji katika maziwa makubwa kila upande na yenye kutoa maji safi yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na wanyama kwa ujumla. Kaskazini kuna Ziwa Victoria, Magharibi Ziwa Tanganyika na Kusini Ziwa Nyasa. Kuna maziwa madogo madogo ndani ya nchi yetu kama vile Ziwa Manyara, Ziwa Natron, Ziwa Eyasi, Ziwa Rukwa na idadi kubwa ya mabwawa madogo na makubwa. Mito midogo ni mingi sana inayojaza mito mikubwa inayo katiza nchini mwetu kila upande kama vile Kagera, Malagarasi, Mara, Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji, Ruaha, Ruhuhu, Ruvuma. Mito hiyo yote inatiririsha maji safi na mengi katika bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii ili niweze kutoa maoni ambayo Kambi ya Upinzani inaona yatafaa na kusaidia kuwezesha kupata mbinu ambazo zitaweza kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili Wizara hii na pia kuondoa matatizo yanayo wakabili Watanzania, kwa ujumla katika kupata maji yalio salama kwa matumizi yao ya kila siku, matumizi ya shughuli za uzalishaji katika kilimo na viwandani.

Mheshimiwa Spika, athari za kukosa maji salama ni kubwa kwani kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa watoto walio chini ya umri wa miaka 16 hufa kila sekunde 8 kila siku, kila mwaka. Sababu kubwa ni uchafu wa maji na matumizi ya maji yasiyosalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimali maji tuliyonayo, tutumie rasilimali hii kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata uhakika wa maji miaka inayokuja. Kwa mujibu wa wachambuzi wa masuala ya maji raslimali ya maji salama hapa kwetu ni kilometa za ujazo 89 ambazo ni sawa na ujazo wa mita 2,700 kwa mtu kwa mwaka, inakadiriwa kuwa ujazo huo kwa mtu unapungua kadri idadi ya watu inavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona juhudi za kupambana na upungufu huo hazijafanywa vizuri, kwa maana kuwa mabadiliko ya hali ya hewa ndicho chanzo kikuu cha upungufu huo. Aidha, Serikali badala ya kutumia vizuri misitu yetu kwa uvunaji, yenyewe inawapa watu ambao hawaangalii athari za maji, mfano ni msitu ya Geita ambao umemilikishwa kwa kampuni ya madini. Mahitaji ya madini ni ya muda mfupi, mahitaji ya misitu ili tupate maji ni ya muda mrefu na endelevu.

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali inapofanya maamuzi yake hasa kwa masuala yanayoathiri mazingira kuwa na vigezo vinavyoweza kuonyesha hasara na faida

katika muda mfupi na mrefu ili kuepuka maafa yanayoweza kuathiri upatikanaji wa maji baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la upungufu wa maji linalotokana na kampeni ya kupanda miti ambayo haifanyiwi utafiti wa taathira zake kwa maji, kwa mfano, upandaji wa miti ambayo inauwezo mkubwa sana katika kutumia maji kwa ustawi wake, mfano mzuri ni miti ya mikaratusi ambayo hunyonya maji kwa kiwango kikubwa hadi kuathiri vyanzo vya maji.

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuwatumia wataalamu katika kueneza zoezi la upandaji miti, kwani sio kila miti inafaa katika kuhifadhi mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji na MKUKUTA, ukuaji wa uchumi katika sekta zote za uzalishaji unatakiwa uende sambamba na ukuaji wa sekta ya maji, hivyo basi maji ni kichocheo muhimu sana katika sekta zote za uzalishaji kama vile viwanda, uzalishaji umeme, kilimo cha kisasa, ufugaji bila kusahau matumizi ya majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maji hapa Tanzania unachangiwa kwa kiasi kikubwa na ushindani mkubwa uliopo miongoni mwa watumiaji katika sekta mbalimbali za uchumi vile vile uharibifu unaofanywa katika vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na angalizo madhubuti kuhusu kuendeleza hazina ya maji iliyopo chini ya ardhi na uelewa mdogo wa vyanzo vya maji yaliopo kwenye hewa na hili linasababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo japokuwa chini ya ardhi na kwenye hewa kuna maji mengi sana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kumekuwa na utofauti mkubwa wa kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka eneo moja hadi lingine kwa mfano maeneo mengi ya Wilaya hutofautiana kwa kiasi kikubwa, kuanzia kwa kiwango cha asilimia 3 na 97, kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi ni jukumu la Serikali yoyote ile na hii ni lengo moja katika malengo ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA), Malengo ya Maendeleo ya Milennia na dira yake ya maendeleo ya 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la MKUKUTA ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2009/2010 zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania waishio vijijini wanapata maji safi na salama ndani ya dakika thelathini kutoka makazi yao. Hii ni maana yake ni kwamba akinamama 65 kati ya 100 waweze kutumia dakika thelathini tu kupata maji ifikapo mwaka 2010. Wakati huo huo, katika maisha halisi kuna ongezeko la pengo la upatikanaji wa maji safi na salama kati ya matajiri na masikini na kati ya watu waishio maeneo ya vijijini na mijini pengo hili lililochochewa na ubinafsishaji na sera za ulipaji madeni zilizowekwa na Serikali yetu na Benki ya Dunia *(WB)* Shirika la Kimataifa la Fedha *(IMF)* na kundi la wahisani kuanzia katikati ya miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati wa kufanya kazi na kwa kweli tusilale mpaka malengo ya MKUKUTA katika sekta ya maji yafikiwe. Tujipime kila mwaka kuwa

tumefikia wapi na Waziri wa Maji kila mwezi wa Juni au Julai atoe taarifa Bungeni kufanikiwa au kutofanikiwa katika kufikia malengo ya MKUKUTA katika mwaka uliokwisha. Hakuna kulala mpaka kieleweke! Kueleweka ni wananchi wote kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji na magonjwa ya mlipuko, inakadriwa kuwa idadi kubwa ya watu katika Bara la Afrika hawana huduma ya maji safi na salama kutokana na hali hiyo inakadiriwa kwamba 50% ya watu katika nchi maskini duniani wanaugua magonjwa yanayosababishwa na huduma duni za maji safi na uondoaji wa maji taka. Taifa letu la Tanzania ni mojawapo ya hizo nchi maskini na ni mojawapo ya nchi inayokabiliwa na tatizo hilo na hii inathibitishwa na vilio vya wananchi wetu hasa waliopo vijijini wakitaabika na kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na magonjwa hayo ya mlipuko, kutokana na ukosefu wa huduma bora ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa MKUKUTA, malengo ni kuwa hadi ifikapo mwaka 2010, magonjwa ya mlipuko imekisiwa kuwa uwezekano wa kutokea uwe umepungua kwa nusu. Kwa takwimu zilizopo zinaonyesha magonjwa ya milipuko yanatokea mijini na sio vijijini. Hii inaonyesha kuwa pale ambapo Serikali inatumia fedha nyingi ndipo penye matatizo.

Kambi ya Upinzani inaliona hili kama kushindwa kiutendaji kwa mamlaka husika katika kutimiza wajibu wao kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1960 na 1970 chini ya Rais Mwalimu Julius Nyerere, maji yalihesabiwa kuwa haki ya Watanzania wote. Juhudi za lazima zilichukuliwa kuongeza upatikanaji wa maji kwa kuzingatiwa usawa, ili kuondokana na miongo mingi ya kuwepo kwa matabaka na kutokuwepo kwa matabaka na kutokuwepo kwa haki miongoni mwa watu kutokana na sera ya kuwagawa watu iliyoendelezwa na Serikali ya kikoloni. Mfano katika Mji wa Dar es Salaam, wakazi wa mji huo walipata maji kwa saa 24, tena kwa uhakika miongoni mwa wakazi wake. Tatizo lililopo ni sera endelevu katika mipango yetu. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa ili kuwe na sera endelevu, mipango yetu ifikirie sana ukuaji wa miji, pia ikizingatia kuwa miji yetu mingi haikupangwa vizuri hivyo kusababaisha uharibifu wa miundombinu ya maji. Aidha, gharama za maji zinahitaji kuangaliwa kwani si kila mtu ataweza kulipia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, hatua ya kutekeleza Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria ni nzuri sana na hii ni kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa hapa mwaka jana ya kuwa gharama za mradi ni shilingi bilioni 193.57. Hata hivyo, kama ambavyo tulitaka ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu miundombinu ya umwagiliaji wa malambo ya mifugo katika vijiji ambavyo mabomba yanapita ambavyo ni takribani 54.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kuhusiana na miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na mifugo kwani maeneo hayo husika ni nyeti kwa kilimo na mifugo. Wananchi wanafuatilia sana mradi huu kwani isije kuwa

wanapelekewa maji kwenye migodi tu na kuacha wananchi bila maji ya matumizi ya nyumbani na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hili ingekuwa ni vizuri kama tutaelezwa kuwa katika ujazo wa maji yanayotarajiwa kutoka Ziwa Viktoria ni ujazo kiasi gani kwa matumizi ya kilimo, mifugo, viwanda na majumbani. Hii ndio njia nzuri ya kuondoa muingiliano katika matumizi na ugomvi unaoweza kujitokeza hapo baadae.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ianze kuandaa miundombinu ya kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa vijiji vyote ambavyo maji hayo yatapita ili tuondokana na adha hii ya kuwa omba omba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais juu ya maji. Wakati Mheshimiwa Rais anatembelea Mkoa wa Mara Wilaya ya Tarime tarehe 15 Agosti, 2006 aliwaambia wana Tarime kuwa tatizo la maji haliwezi kuishinda Serikali hivyo aliahidi kutafuta shilingi bilioni 9 ili kuondoa tatizo hilo Tarime. Kambi ya Upinzani inataka Serikali iwaambie wananchi hao ahadi hiyo ya Rais itaanza kutekelezwa kuanzia mwaka gani wa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio Tarime tu ambapo ahadi za maji zimetolewa na tarehe 25 Oktoba, 2005 akiwa anaomba kura Urais katika Wilaya za Masasi na Ludewa alidokeza kuwa Rais mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa alikuwa na mpango nyeti kabambe wa kumaliza matatizo sugu ya maji katika Wilaya hizo. Kwa kuwa wajibu wetu ni kufuatilia kauli hizo na mipango ya Serikali, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze hatua hizo za utekelezaji wa mipango hiyo imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, aidha akiwa katika mchakato wa kuomba kura tarehe 13 Septemba, 2005 alitoa ahadi yake ya kutenga milioni 680 za Benki ya Dunia ili kuimarisha mradi wa maji katika Wilaya ya Kondoa. Bahati nzuri tulimsikiliza Mheshimiwa Paschal Degera alivyokuwa akielezea tatizo sugu hili la maji na fedha chache zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajiuliza kama kweli nia ya ahadi hizo ilikuwepo au ilikuwa ni mbinu ya kuombea kura? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa maji nchi jirani, biashara ya uuzaji wa maji hasa ya kunywa ni moja ya bidhaa ambayo inaonesha mafanikio makubwa kwa nchi na wafanyabiashara wanaojikita katika biashara hiyo. Kama inavyojulikana nchi yetu ina rasilimali maji ya kutosha na nzuri ikilinganishwa na nchi nyingine katika Bara hili. Licha ya kuwepo kwa faida hiyo na umuhimu wa rasilimali hii bado imekuwa ni vigumu kwa Serikali kuliona jambo hili. Hii ni kwa sababu ni kiasi kidogo sana cha maji yanayotoka nchini mwetu kwenda nchi za jirani kama Kenya na Uganda, Komoro, *DRC* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni kiasi kikubwa cha maji kutoka nchi jirani yametanda na kuuzwa katika aina mbalimbali za chupa yanapata wanywaji kwa wingi. Hivyo basi unakuta maji yanayotengenezwa ndani ya nchi yetu yanakuwa ndani ya ushindani

mkubwa mno, ndani ya mkoa wote wa Kagera maji ya kunywa yaliyoenea na kutumika kwa wingi ni maji ya Ruwenzori kutoka Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni biashara ambayo haijapangiwa programu nzuri ya kujua mahitaji ya ndani, ukubwa wa masoko ya nje na namna tunavyoweza kuingia katika ushindani wa biashara hiyo ambayo kwa kiwango kikubwa kimesaidia katika kuongeza ajira kwa vijana wetu. Hapa Kambi ya Upinzani inataka kujua ni nini tatizo linalofanya tushindwe kusambaza maji kwa kiasi kikubwa angalau kwa majirani zetu. Kama tatizo ni udhaifu wa viwanda vyetu vya kuzalisha maji kwamba vinashindwa kuzalisha maji kwa kiwango kinachotakiwa, basi Serikali ishawishi makampuni mengine yanayotumia tekinolojia ya maji kama ilivyoonyeshwa kwenye Maonyesho ya Sabasaba, kutokana na hewa kuweza kutoa kuzalishaji wa maji kwa ajili ya kilimo, viwanda na soko la nje. Tungependa kupata kauli ya Serikali katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa endapo Serikali itasimamia kikamilifu programu hizi na kukubali kutumia tekinolojia mbalimbali za maji, uwezekano wa kuondokana na matatizo ya maji safi katika shule, kambi za vyombo vya ulinzi, hospitali na vituo vya afya pamoja na umwagiliaji utapungua kwa kiwango kikubwa sana. Aidha, soko letu la maji litapanuka na kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kongamano la mwaka la wataalamu wa maji, kongamano ni njia mojawapo ambayo inahakikisha kwamba sera ya maji inaeleweka na kuhamasisha utekelezaji wake. Kupitia makongamano hayo wataalamu hupata fursa ya kubadilishana mawazo na kujadili mambo mbalimbali. Makongamano mengi yamekuwa yakiandaliwa na kufanyikia mjini ambapo kwa kiasi kikubwa wakazi wake walio wengi wanauhakika wa kupata maji safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo kuu la makongamano haya ni kuhakikisha kwamba sera ya maji inaeleweka, basi itakuwa vizuri zaidi kama makongamano haya yataelekezwa vijijini zaidi ambapo kunaaminika kuwa na vyanzo vingi vya maji na wananchi huko wanashindwa kuvitunza kama invyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi ni wadau muhimu sana ambao wanatakiwa kushirikishwa katika hatua zote za awali kuanzia utafutaji wa vyanzo vya maji, uchimbaji visima na mabwawa, wanahitaji kupewa taaluma na taarifa ya jinsi ya kuvitunza vyanzo hivyo vya maji na hiyo itawezekana pale tu watakaposhirikishwa kama wadau muhimu.

Mheshimiwa Spika, tumeona na hata kupata kusikia kutoa huduma kwa baadhi ya visima vilivyochimbwa na Serikali au na mashirika mbalimbali yaliyojitolea misaada lakini kumekuwa na udhaifu wa utunzaji kutoka kwa wananchi wenyewe hii ni kutokana na kutoshirikishwa kikamilifu katika hatua za awali.

Mheshimiwa Spika, suala la kufanyiwa utafiti kwa baadhi ya maeneo katika mikoa mbalimbali ni la muhimu ili kuweza kuelezwa ni mahali gani pana uwezo wa kutoa maji mengi. Ni vyema baada ya utafiti huo wananchi wakajulishwa na baada ya utafiti huo taratibu za uchimbaji zikafuata, vinginevyo malalamiko ya wananchi kupitia

Wabunge wao yatakuwa hayamaliziki hasa wanapoona kuwa kila baada ya muda utafiti hurudiwa tena na bila ya ufumbuzi wa matatazo yao, hivyo kuzidi kupoteza matumaini ya maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili linawachosha wananchi kwani wao wanaendelea kusubiri huku wakiteseka kwa adha na shida wanazozipata kwa kukosa maji safi.

Kambi ya Upinzani tunakubali kuwa katika utafiti huo kuna maeneo ambayo hayawezi kuchimbwa visima. Basi ni muhimu kutafutwe suluhisho la haraka ili tuweze kuwakomboa wananchi hao kutoka katika janga la kuweza kupata magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Spika, mfano katika taarifa ya habari mwezi uliopita katika Mkoa wa Kigoma wananchi wapo katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na kukosa maji safi ya kutumia kwa matumizi mbalimbali, wananchi hao wanatumia maji kutoka katika visima vilivyochimbwa na shirika la wakimbizi ambavyo hata hivyo havina uwezo wa kutoa maji ya kutosha na ni vibovu hivyo kuhatarisha maisha ya watoto waendapo kuchota maji hayo. Hii yote ni kwa sababu hawana njia nyingine ya kuweza kupata maji. Ukiachana na mkoa huo kuna sehemu nyingi ambazo wananchi wake wamekuwa wakilalamika juu ya ukosaji wa maji safi kwa matumizi yao mfano, maji kuwa na sumu na hivyo kuathiri binadamu na hata mifugo watumiapo maji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni muda ambao Serikali inatakiwa ione umuhimu wa kujenga malambo ya kutosha ili kuweza kutumika kuogesha na kunyweshea mifugo, hali hii inasababisha usumbufu kwa wananchi kwani inapotokea mifugo imetumia maji kabla ya wananchi inawabidi kusubiri kwa muda mrefu mpaka maji yatulie ndipo waweze kuchota maji, uchimbaji wa malambo ni hatua muhimu sana kwani itasaidia kuwaepusha wananchi na magonjwa ya mlipuko. Wananchi wana nafasi nzuri ya kuweza kuhifadhi na kutunza vyanzo vyao vya maji kwa afya yao wakiwezeshwa kwa elimu na nyenzo.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa idadi kubwa ya watu katika Bara la Afrika hawana huduma ya maji safi na salama. Kutokana na hali hiyo inakadiriwa kwamba 50% ya watu katika nchi maskini duniani wanaugua magonjwa yanayosababishwa na huduma duni za maji safi na uondoaji wa maji taka. Taifa letu ni mojawapo ya hizo nchi maskini na ni mojawapo ya nchi inayokabiliwa na tatizo hilo na hii inathibitishwa na vilio vya wananchi wetu hasa waliopo vijijini wakitaabika na kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na magonjwa hayo ya mlipuko, kutokana na ukosefu wa huduma bora ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malipo ya maji kwa watumiaji wa maji wenye uwezo mdogo hili limekuwa ni tatizo kubwa kwao kwani maji yanalipiwa kiasi kikubwa tofauti na uwezo wao. Kwa mfano kwa wakazi wa Dar es Salaam hili imekuwa ni tatizo kubwa na kero kwa muda mrefu. Dar es Salaam dumu moja la maji linagharimu shilingi 20 kwa maji yanayotembezwa na magari aina ya kenta. Hii ni nafuu sana lakini huduma hii inafanyika katika sehemu chache sana, kwani huduma hii ipo kwa wakazi wa Kimara na maeneo machache sana jijini. Sehemu nyingine wanatumia maji yanayotembezwa katika

mikokoteni hii inawagharimu shilingi 200 mpaka 300 kwa dumu moja na hii inakuwa ni vigumu sana kwa wananchi wa kawaida kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji hata hivyo, limekuwa zaidi kutokana na mabadiliko katika sera ya kuondoa maji kama bidhaa ya lazima na ya haki kwa kila mtu na badala yake na bidhaa ya anasa. Hii ni imetokana na Serikali kujitoa kwa sehemu kubwa kwenye huduma hii muhimu na kuwaachia wafanyabiashara ambao hawajali maslahi ya wananchi hasa wanyonge na badala yake wanaangalia faida pekee. Angalia Serikali ingetoa maelekezo ya mara kwa mara kudhibiti uholela wa bei ya maji ambayo kimsingi ni hitaji la msingi la binadamu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Serikali ingeweza kuwekeza kwenye miundombinu ya maji na kuweka mfumo wa vioski vya kuuza maji kwa kiwango cha shilingi 20 kwa dumu au ndoo ili kumwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kupata maji badala ya kuwaachia wafanyabiashara wakubwa kuuza maji hayo kwenye chupa au plastiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya sekta ya umma yaongezwe, sambamba na kushirikishwa kwa taasisi za jumuiya za kiraia na jamii yenyewe. Vyanzo viongezwe katika sekta ya maji kwa kuweka usimamizi madhubuti kuhakikisha kwamba maliasili hii inafika katika ngazi za Wilaya na vijiji na kumnufaisha mtumiaji ambaye ni mwanamke, mwanaume na mtoto, kwa ujumla jamii nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya mwaka 2006 ilikuwa maji na Utamaduni, ambavyo inawakilisha pamoja na mgawanyiko wa upatikanaji wa maji miongoni mwa jinsia katika ngazi ya nyumba na Taifa. Kiutamaduni kazi ya kuchota maji huwahusu zaidi watoto na wanawake kwa kubeba kichwani kwa umbali mrefu. Japokuwa utekaji wa maji kwa familia unatambulika kama kazi ya wanawake na watoto, lakini linapokuja suala la kulipia huduma hii ya maji, vijana wa kiume huigeuza huduma hiyo kama shughuli ya kibiashara kwa kutumia mikokoteni na baiskeli na si kwa kubeba vichwani kama wafanyavyo wanawake na watoto. Vijana hao hufanya hivyo kwa manufaa yao wenyewe na si kifamilia na wakati mwingine hukodiwa na wafanyabiashara matajiri wa maji, wanaume hunufaika kutokana na tatizo hilo la maji, ambapo wanawake na watoto wanatoboka vichwa kwa kubeba ndoo vichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo faida wanayoipata wanaume hao ni ndogo ukilinganisha na faida wapatazo wamiliki wa visima wanaowauzia wafanyabiashara ya maji, kibaya zaidi ni kwamba faida zinazoenda kwa wafanyabiashara hao matajiri na wafanyabiashara wadogo zinatokana na maji kutoka vyanzo vya Taifa na hii ni mojawapo ya kuifanya biashara ya maji kuwa ya anasa zaidi kuliko kuwa haki ya mwananchi yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utamaduni huu unapaswa kuachwa mara moja ni jambo ambalo Serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka ili kuwaokoa akina mama hawa pamoja na watoto kutoboka vichwa kutokana na adha ya maji.

Mheshimiwa Spika, maji yanatakiwa yatambulike kama haki muhimu ya kila mtu na si bidhaa ya kiuchumi; haki za Kimataifa  za wanawake na usawa wa kijinsia utambuliwe katika masuala ya upatikanaji  wa maji safi na salama na Serikali; sera ya kufanya maji kuwa bidhaa ya anasa kama Mashirika ya Kimataifa ya kifedha duniani iwe *WB, IMF* na Mashirika mengineyo huyafanya maji kuwa bidhaa ya kiuchumi kama masharti ya kufadhiliwa kuendeleza huduma hii iachwe; mpango wa kulipia maji maeneo ya vijijini ambako sehemu kubwa ya watu wake ni masikini ipitiwe  upya na wahusika; ushirikishaji wa  jumuiya ya kiraia uzingatiwe katika upangaji wa sera/Bajeti, utekelezaji, usimamizi, ikiwamo utoaji wa huduma ya maji ili kuongeza ushirikishaji na uwazi na kama Serikali ina nia na lengo la kuondoa tatizo hili la maji na kuwasaidia wananchi wake ni muhimu mjadala wa Kitaifa kuhusu maji uitishwe ambapo wananchi watakuwa na uwezo na watakuwa huru kuuliza maswali mbalimbali na kutoa maoni yao kwani wao ndio wadau wakubwa na ndio waathirika katika adha hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesi ya *City Water* Kambi ya Upinzani inataka kujua maendeleo ya kesi ya kampuni ya *City Water* na gharama kiasi gani zimelipwa mpaka sasa na kwa kampuni ipi ya uwakili?  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, japokuwa Serikali imeweka kipaumbele katika maji kwa maendeleo ya Taifa, lakini bado kuna tatizo kubwa na la msingi kuhusu wataalamu wa maji *(water engineers).* Kwa kuwa kulingana na hali halisi kijiografia ya nchi yetu uhakika na usalama wa maji hauwezi kuwepo bila kuwepo na wataalamu wa maji wa kutosha. Aidha, hili linatakiwa liende sambamba na mpango kabambe wa kusambaza maji kwa kila vijiji 10 kwa kila Wilaya kwa Tanzania nzima, kama Serikali inasema ukweli kwa hili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni mkakati gani ulioandaliwa kwa wataalamu wa maji kuwepo angalau katika Wilaya, tarafa zetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.  *(Makofi)*

**SPIKA:**Ahsante Mheshimiwa  Meryce Emmanuel na *timing* yako nzuri sana, umekwenda na kengele.  Ila tu taarifa mnapotoa mara nyingine zinaleta utata, tarehe 25 mwezi wa kumi taarifa ya Upinzani inadai mgombea wa Urais wa CCM alikuwa Masasi na Ludewa, kwa jiografia ya nchi yetu mgombea wa namna hiyo itabidi awe ametumia usafiri wa anga na Ludewa hakuna kiwanja, kwa hiyo, haikuwa ni ndege ni helkopta na tunajua nani anatumia helkopta.  *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Charles Kajege, ameomba udhuru kidogo ametoka, kwa hiyo, nitamwita kwanza Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya awe mchangiaji wa kwanza, baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na ajiandaye Mheshimiwa Paschal Degera.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo. Kabla sijachangia ningependa pia niungane na wenzangu kutoa salamu zangu za rambirambi kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Morogoro ambao ni wapiga kura wangu kwa familia ya aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, hayati ndugu yetu Juma Jamaldin Akukweti ambaye alikufa kutokana na ajali ya ndege aliyoipata akiwa anatekeleza majukumu ya Kitaifa.

Pili, ningependa pia kuchukua nafasi hii kuipa pole familia ya hayati Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, ambaye alikuwa ni Mbunge wa Vijana kupitia Umoja wa Wanawake wa Tanzania. Napenda pia niwape pole Umoja wa Vijana wa CCM kwa kupotelewa na mwakilishi wao ambaye alikuwa ni mahiri sana, alipenda kutetea sana haki za vijana na maslahi ya vijana.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kutoa pole na salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa kwa wale wote waliokufa kwenye ajali za mabasi katika mkoa wa Singida, Kilimanjaro na mahali pengine popote. Zaidi ningependa kutoa pole kwa familia ya marehemu aliyekuwa Mbunge mwenzetu hayati Mheshimiwa Stephen Kazi ambaye pia alifariki akiwa katika harakati za kusaidia ushirika katika Mkoa wa Mwanza pamoja na wenzake. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa pia kuwapa pongezi zangu walioteuliwa katika nafasi mbalimbali akiwepo Mheshimiwa Bernard Membe, kwa kupewa nafasi ya kuwa Waziri wetu wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge pamoja na wale wote ambao walihamishwa kutoka kwenye Wizara zao kwenda Wizara nyingine, ninaamini kwamba yote ni majukumu na watalitumikia Taifa vizuri, Mwenyezi Mungu awape afya njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu Waziri wake na wataalamu wao kwa kutengeneza hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Baada ya kutoa pongezi hizo pia nisisahau kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, katika Ilani yetu, Mheshimiwa Rais pamoja na sisi Wabunge tulikuwa tunazungumzia kuondoa adha ya maradhi na kuhakikisha kwamba tunaboresha afya za wananchi wetu, Serikali imefanya juhudi kubwa kwa kipindi hiki kuhakikisha kwamba pale ambapo waliahidi kuboresha huduma za maji wameanza tena kwa spidi kali, kwa kasi mpya na ari mpya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo basi, ningependa nichangie kwenye maeneo machache kidogo. Eneo ambalo ningependa kuzungumzia ni kwamba ni vizuri tukaelewa kwamba waathirika wa ukosefu wa maji katika nchi yetu ni wanawake. Wanawake ndiyo ambao wanatunza familia, wanawake ndiyo wakulima, wanachangia sana katika kuboresha uchumi wa nchi hii.

Sasa mwanamke anapotumia muda mrefu kwenda kutafuta maji maana yake ni kwamba anashindwa kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

La pili ambalo ningependa niliweke bayana kabla sijachangia pia, ni kwamba tunapokosa maji ya kutosha na maji safi yaliyo salama ni kwamba tunatengeneza mazingira ya milipuko ya maradhi pamoja na kuongeza maradhi ya ngozi maana yake ni kwamba juhudi za Serikali nyingi zitakuwa zinaelekezwa katika kutibu magonjwa ya milipuko pamoja na maradhi mengine ambayo yanatokana na ukosefu wa maji. Kwa hiyo, ili tuweze kupunguza hayo na kuboresha maisha ya wanawake wa nchi hii ningependa kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Mheshimiwa Waziri amesema amezungumzia kwamba kuna mamlaka ya mabonde ya mito yetu. Sasa hizi mamlaka nimejaribu kuangalia hotuba sijaona kwamba wameweka bayana majukumu ya mamlaka. Mamlaka hizi zingefanya kazi vizuri kwa sababu zinagharamiwa kwa hela za walipa kodi. Nina imani kwamba madhara au athari tunazozipata kutokana na ukame zisingekuwa kubwa kiasi ambacho tumeona.

Mheshimiwa Spika, tuna mamlaka ya Bonde la Mto Ruvu, tuna mamlaka ya Bonde la Mto Wami. Nazungumzia hiyo kwa sababu hiyo mito iko katika Mkoa wa Morogoro. Tukiangalia Mto Ruvu sasa hivi Mto Ruvu unapungua maji kwa sababu mbili muhimu. Ni kwamba wakati mvua zinanyesha, maji yanafurika na yanapotokea na katika kupotea yanaleta mafuriko, watu wanaumia. Sawa, watu wangeumia halafu baadaye tukawa na maji ingekuwa ni vizuri. Lakini wakati wa ukame tunakosa maji, sasa ningependa nishauri Wizara kwamba kwenye hii mito mikubwa ambapo kunatokea mafuriko kuwepo basi na mpango wa kutengeneza *storage dams.* Tukiwa na mabwawa ya kuweza kuweka *reserve* ya maji badala ya maji kufurika na kuwaumiza wananchi na mashamba yao haya maji yangeweza yakatunzwa kwenye *point* mbalimbali kabla hatujafika kwenye maeneo ambayo wanachukulia maji kwa ajili ya mji wa Dar es Salaam na miji mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni maji mengi yanapotea Mto Ruvu. Ni maji mengi ya Mto Ruvu yanayofanya mashamba ya mpunga, pamoja na mashamba mengine yaharibiwe. Lakini tungekuwa na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba tunavuna yale maji ya mvua tukaweka kwenye *storage dams* wakati ambapo tunakuwa na ukame tukayaachia haya maji yakatiririka kusudi miji kama Dar es Salaam, Morogoro na Chalinze, tukaweza kupata maji kwenye *continuous basis* ingekuwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba sasa hivi tunaona kwamba mito mingi inaelekea kukauka kwa sababu ya matumizi mabaya, watu wengi wameanza kulima kilimo cha mabondeni. Sasa kile kilimo cha mabondeni pamoja na kupeleka ng'ombe kwenda kunywa maji katika hiyo mito, kumefanya hiyo mito inajaa mchanga na matokeo yake ni kwamba sasa mito inaanza kukauka. Nitoe mfano tu, kuna mto mmoja unaopita pale Dumila kabla hujaingia kwenye mji mdogo wa Dumila, kuna mto ulioko pale.

Mimi ningependa Mheshimiwa Waziri anaporudi kutoka kwenye Bunge lako Tukufu aangalie ule mto sasa hivi hakuna mto ni bwala la mchanga linaanza kutokea pale

na ule mto ndiyo ambao ulikuwa una maji yaliyo mengi katika mto Wami ambao ninaamini kwamba ndiyo unaotegemewa sana katika mradi wa Mto Wami kwa ajili ya Chalinze na maeneo mengine ambayo yanakuja mpaka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukiendelea vile ni kwamba na ule mto kuna wakati ugeuka, sasa mimi ninaamini kwamba yule bwana anayehusika na Bonde la Mto Wami ataanza kuona kwamba kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba anatunza lile Bonde la Mto Ruvu na Bonde la Mto Wami kwa sababu mto unajaa mchanga na siyo mchanga tu kuna hatari ya kupoteza hata ile barabara kama tutapata mvua nyingi kama tulizozipata mwaka huu. Naomba aangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba nimeona katika hii hotuba kuna mabwawa ambayo yamechimbwa lakini Mkoa wa Morogoro hakuna bwawa hata moja, naomba niwaambie kwamba anapotoka huku pia akitazama kuna eneo linaloitwa Wami Dakawa, Wami Sokoine na eneo lingine linalofuata linaitwa kwa Makunganya. Kuna wananchi wanaishi kule na wanategemea maji ambayo yanatokana na mashimo yaliyoachwa na wachimba barabara ambayo kwa vinginevyo tunasema kwamba imekuwa basi ni baraka ya uharibifu wa mazingira, ni kwa sababu walichimba wakaacha kuyafukia, sasa tunapata maji mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye yale maji humo humo watu wanaoga, wanachota maji ya kunywa na humo humo unakuta ng'ombe wanakunywa maji kwa hiyo inakuwa ni *competition* kati ya wanyama na binadamu kwa matumizi ya yale mabwawa. Lakini bahati mbaya yale mabwawa pia hayatoshelezi na wale wananchi hawapo mbali na mto Wami, mimi naomba Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wale ndugu zetu wanaoishi kule wengi wao wakiwa ni wafugaji wanahitaji maji kwa ajili ya wanyama wao na wahitaji maji pia kwa ajili ya matumizi yao. Kama tutakuwa na mpango endelevu wa kuwapa maji ni kwamba hawa ndugu hawataenda kuzunguka na wanyama wao kuendelea kuleta uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nizungumzie juu ya wajibu wa *EWURA*. Nimeona kwamba wajibu wao mmoja ni katika kurekebisha bei za maji na nishati. Tunasema *tariff* za maji kwenye miji yetu ambayo ina mamlaka zinategemea sana zile *tariff* za umeme unaotumika katika kupampu na bei za madawa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kila wakati *TANESCO* itakuwa inapandisha bei za umeme wao ina maana kwamba na bei za maji katika miji yetu ambayo ina mamlaka zitapanda. Bei zikipanda ni kwamba ni watu wengi watakatiwa maji kwa hiyo, watu wengi wanakwenda kuchota maji ya mito na matokeo yake ni kwamba tunapata milipuko ya kipindupindu na kwa mfano mmoja ni eneo la Chamwino katika Mkoa wa Morogoro, walio wengi hawana uwezo wa kifedha inabidi wakachote maji katika Mto Ngerengere kwa sababu hawawezi kuvuta maji, gharama ni kubwa na hawawezi wakalipa zile gharama ambazo zinatozwa na Mamlaka ya Maji.

Mimi ninaomba yafuatayo kwamba katika maeneo ambayo kuna watu wengi ambao hawana uwezo wa kuvuta maji Serikali yetu iangalie kama tunaweza tukawa na

mpango kabambe wa kuweza kuwapatia wale wananchi maji kwa namna ambayo inakuwa ni maji ya jamii waweze kuchangia kwa pamoja kiasi ambacho wanaweza wakamudu kuchangia kama wananchi wa eneo lile. Kwa mpango huu tunaweza tukapunguza matatizo ya maji katika maeneo ambayo kunakuwa na milipuko ya kipindupindu.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine katika maeneo vijijini hakuna mabwawa wala visima vya maji kwa hiyo, kazi kubwa inayokuwa kule ni wanawake kutembea kuchota maji au kununua. Lakini wale wanaowauzia maji siyo maji ambayo yanaweza yakatumika kwa matumizi ya binadamu na matokeo yake siyo mazuri watu wanaugua. Naomba Wizara iangalie namna ya kuweza kuboresha uwezekano wa kupata maji katika maeneo ya vijijini.

Lakini Wizara hii ingekuwa ni vema ikashirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu mito kama Mto Ruvu na huu mto kama niliouzungumzia wa Dumila kuna wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu ndiyo ambao wanaharibu sana vyanzo vya maji na ndiyo ambao wana *contaminate* maji kwa *mercury* kwa hiyo, mimi napenda wakishirikiana kwa pamoja wafanye maboresho ya kuweza au mpango wa kuwaelimisha hao wachimbaji wadogowadogo kama wanahitaji maji basi wawe na pampu za kuweza kupampu maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hizi pampu katika kijiji kimoja katika Tarafa ya Matombo zimeibwa zote na wachimba madini wa Mto Matombo, matokeo yake ni kwamba vile visima vimevunjika na watu wameamua kuvifumua wachote maji na kwa bahati mbaya kwa kipindi cha mwezi mmoja wamekufa watoto wanne wakitumbukia kwenye kisima kwa sababu wachimba madini wanaochimba pale Mtamba nafikiri na Kibangile wameiba zile pampu za maji na Tawa. Sasa naomba hizi Wizara mbili ziangalie namna ya kudhibiti hawa wachimbaji kwa sababu hata tukisema tuweke mlinzi pale tunakuwa hatuna hela za kumlipa kwa hiyo, anaweza akashirikiana nao kutuibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya maji vijijini ni mengi na watu wanachimba visima halafu wakati wa mvua maji ya kutoka chooni yanapofurika yanakwenda kule ndiyo tunapata matatizo. Mimi naomba *engineers* wa maji wajaribu kuangalia namna ya kushirikiana na Idara ya Afya wakati watu wanapoomba kuchimba visima wafanye *survey* nzuri ili waweze kuwa wanavipeleka maeneo ambayo hayatapata *contamination* wakati wa mvua tuweze tukapunguza haya matatizo ya watu kupata mlipuko wa kindupindu na maradhi ya kuharisha wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda pia nizungumzie juu ya mpango kabambe wa uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo ya vijijini. Sasa hilo jambo sijui ni nani anaachiwa mara tuzungumzie Serikali za Mitaa, Wizara na hata Wizara ya Afya ni nani anayehusika kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mpango maalumu wa kuweza kuboresha au *to promote* uvunaji wa maji ya mvua katika vijiji vyetu, tusisubiri tu wahisani siku wakiondoka tutafanya nini? Ni mpango ambao kwenye kijiji

akifundishwa kijana mmoja kutegengeneza ile mitungi na kuweza kutumia mianzi au mabati ya bei nafuu wanaweza wakavuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji taka, naomba kusema kwamba mji wa Morogoro pamoja na sisi Madiwani tuna kazi kubwa kuhakikisha kwamba nyumba zinazojengwa hasa nyumba za Msajili wa Majumba hazileti maji taka katika mito yetu.

Napenda pia Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara inayohusika na nyumba nafikiri ni Miundombinu ambayo ni Ujenzi yaani *National Housing* waangalie namna ambayo wanaweza wakatusaidia sisi wananchi wa Morogoro kwa sababu zile nyumba zilijengwa zamani na waliojenga mpaka sasa hivi hakuna mpango wa kuweza kurekebisha mfumo wa kutoa maji taka katika majumba haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo inaleta madhara kwa sababu Mto Morogoro unatumiwa na wengi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawaomba Waheshimiwa Wabunge katika hizi Wizara za siku moja moja jitahidi hata kama dakika kumi umalize na kwa taarifa tu ni kwamba mambo yanaeleweka vizuri yakiwa ni machache yaliyolengwa kuliko kuendelea tu.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kwa kuwa nimeshamuona Mheshimiwa Charles Kajege, amesharejea akishamaliza Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, ataingia Mheshimiwa Charles Kajege wakati huo bado Mheshimiwa Paschal Degera, ajiandae.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, katika Tanzania tuna vyanzo vya maji kadhaa, mojawapo ni Mito, Maziwa na maeneo ya Singida, Tabora na hapa Dodoma tunategemea sana vyanzo vya maji kwa visima virefu *(deep wells).* Mara nyingi kule Singida kwa mfano kisima kimoja kinaenda mpaka mita 100 hadi 150 tumechimba visima vingine vimeenda hadi mita 250 hadi 300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya maji ni ya gharama kubwa sana kuyapata. Ziwa Victoria ni rasilimali kubwa sana hapa Tanzania, Ziwa Victoria walifanya upembuzi yakinifu nafikiri nimeona baadhi ya michoro kama maji yangetoka Ziwa Victoria yangeweza kunywesha watu wote wa Mwanza, Musoma, Shinyanga, Mkoa mzima wa Tabora, Singida na yale maji yangeweza kufika hapa katika Mkoa huu wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo mradi ungekuwa ni ile tunaita *mega projects,* lakini miradi mikubwa na ya gharama ndiyo miradi inayokuwa na ndiyo yenye uwezo mkubwa

sana wa kuweza kuchangia katika uchumi wa nchi. Tatizo liko wapi? Ziwa Victoria ni sehemu ya *Nile River Basin* na wanasema *Nile River Basin* ina kilometa za mraba milioni 3.3. Katika hizo kilometa za mraba 81,000 ni Maziwa yaliyopo katika ule ukanda na kilomita 70,000 za mraba ni *swamp areas.* Na kuna nchi 10 ambazo wanaziita *repairing states* ambazo zinahusika na wamiliki wa hili Bonde la Mto Nile. Tupo sisi Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Malawi, *DRC,* Burundi, Rwanda, Sudan na Egypt kama nilivyowataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi takriban 280 milioni wanaokaa katika hili Bonde linaloitwa *River Nile Basin* na wanatarajia kufikia mwaka 2025 kutakuwa na takriban wananchi milioni 591 katika eneo nililolitaja. Mahitaji ya maji kwa ujumla yataendelea kuwa makubwa sana. Mto Nile kama tunavyojua ni mto mkubwa na mrefu kuliko yote duniani. Katibu zaidi ya maili 4187.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi mikubwa iliyowahi kujengwa duniani ikitumia maji ya Mto Nile ambayo yametokea Ziwa Victoria ni mradi mkubwa sana unaoitwa Lambo la Aswadi kule Egypt. Lambo hili lilianza kujengwa mwaka 1959 baada ya Egypt na Sudan kutiliana sahihi makubaliano yao ya matumizi ya Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni wa pili kwa ukubwa duniani na wanasema una *stretch* kilometa nne, wamejenga pembeni ya Mto Nile, kilometa nne za bwawa na urefu unaenda hadi kilometa moja na katika karne ya 20 hii imekuwa ni *one of the miracles of the science* katika *construction. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba wa mwaka 1929 uliotiwa sahihi na Balozi wa Uingereza aliyekuwa anaishi Cairo, kwa niaba ya Serikali ya Uingereza na kwa niaba ya Mataifa mengine madogo madogo yote ambayo yalikuwa ni makoloni ya Muingereza na Egypt, umekuwa ni mkataba mbaya sana ambao umesababishia Tanzania na nchi zinazoizunguka hasara ya mabilioni ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu uliotiwa sahihi na wale wanaojiita waliokuwa wakoloni wetu jambo la kwanza uliipa Misri haki ya kutumia zaidi ya *cubic metre 55.5* za maji ya Mto Nile na wakasema kwamba Egypt itakuwa na *vital power* kama kuna kanchi kengine kule Uganda, sijui Tanzania mtachokonoa tu kujaribu kutumia maji wanakuja na wana uwezo wa kukagua na wana uwezo wa ku-*react. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka ijayo Mataifa haya yana uwezo wa kwenda vitani kwa sababu ya tatizo la maji. Kama nilivyosema *population* ya watu 280 milioni inaweza kuongezeka kwa wastani wa 2.5 hadi kufikia watu 591 milioni katika miaka 20 ijayo. Uwezekano mkubwa sana wa kuweza kuingia kwenye *conflict* za maji utakuwa ni mkubwa. Baada ya Sudani kupata Uhuru mwaka 1956, Sudan waka-*renegotiate* ule mkataba na nchi ya Egypt, wakapata mkataba ulioitwa *Nile Waters Treaty* na ulikuwa ni baina ya nchi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu na labda nirudi nyuma kidogo, Mto Nile unakisiwa kuwa na *cubic metre* za maji 84 bilioni kwa mwaka, *flow* inayopita lakini

wanasema *10 billion cubic metre* zina-*evaporate,* zinapotea wakati wa ku-*flow,* wakati wa jua kali na kadhalika. Kwa hiyo, zinabaki *cubic metre* 74 bilioni. Katika ule Mkataba mwaka 1959 Egypt wakapewa *rights* za bilioni 55.5 na Sudan chini ya ule mkataba wakapewa *right* ya bilioni 18 ya *flow* ya maji, jumla ukipiga hesabu unapata *cubic metre* bilioni 73, hizi ni nchi mbili tu kati ya nchi kumi ambazo zina haki ya kutumia maji ya *Nile Basin. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema katika maisha *you don't get what you deserve, you always get what you negotiate.* Na mkataba huu ulitengenezwa kwa niaba yetu na nchi ambayo ilikuwa inatutawala. Waethiopia wamepata Uhuru muda kidogo baada ya ule mkataba na wamekatazwa kabisa kuingia kwenye huu mkataba na wanapata shida sana.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Ethiopia ni nchi mojawapo inayopata matatizo makubwa kutokana na wao kutokuweza kutumia maji ya *Blue Nile. Blue Ni*le inatumia asilimia 53 ya maji yanayoingia katika huu mto Nile na tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Spika, tatizo ni watu wanaokufa ka njaa Ethiopia. Tatizo ni watu wasio na maji katika nchi ya Tanzania, watu wanaopata matatizo yanayotokana na maradhi yanayotokana na maji *(water born diseases)* zaidi ya *90% of all the diseases are water born.* Na sisi tunauliza haki ya kuweza kutumia maji ya Ziwa Victoria. Tanzania ipo kilometa 600 hadi ufike Egypt wao ndio wanaotumia maji zaidi ya 98% ya matumizi yote ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imebuni mradi wa maili 105 kutoka Ziwa Victoria mpaka Kahama na hizi nchi nyingine zote zimepiga kelele na Egypt ilikuwa imehakikisha hakuna *development donor* yoyote atakayetoa dola. *World Bank, UNDP, Arab Fund* na hao wengine wote walikataa kuisaidia Tanzania. Tanzania ilipoamua kutumia fedha zake wenyewe mradi huu wa kwanza na wa kihistoria umewekwa katika vitabu vya kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu yeyote anayetusubiri sisi Watanzania kwa upendo na anayetuangalia anataka aje atusaidie kuijenga nchi yetu. Ni lazima tu-*renegotiate* mkataba huu na mimi naungana na Serikali na alisema Mwalimu Nyerere, haukubali wala hautambui mkataba uliowekwa na wakoloni na chini ya matarajio tuliyonayo, uwezo wa Tanzania kuweza kumaliza kabisa matatizo ya maji ya mikoa niliyoitaja hadi mkoa wa Dodoma, upo kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria, na sisi hatusemi kwa sasa hivi twende kwenye *irrigation,* labda *irrigation* itachukua maji mengi ambayo itawafanya ndugu zetu wa Egypt waweze kufikiria mbinu nyingine za kupambana na sisi, lakini maji ya wananchi kunywa *(drinking water)* ambayo ni salama kwa ajili ya wananchi wetu, tuna haki kabisa kufikiria miradi mikubwa itakayotuokoa na hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ya Uingereza imehusika moja kwa moja kuweka mkataba ambao hautusaidii, mkataba ambao unazinyonya nchi nane zinazohusika na Ziwa Victoria na Mto Nile, mimi ningependa kupendekeza kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Tanzania, yenyewe au iungane na nchi zingine

zinazohusika, kuishitaki Serikali ya Uingereza kwa mkataba ambao kwa hesabu za kawaida unaiingizia Tanzania hasara ya mabilioni ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1929 Waingereza waliuweka ule mkataba kwa maslahi yao ya kivita, kiulinzi, lakini hapakuwa na maslahi yoyote ya nchi hizi ambazo zinahusika. Tanzania, Burundi,Uganda, Kenya, *DRC,* Eritrea, hawa wote hawafaidi chochote na huu mkataba, na huu mkataba ni mbaya na ni lazima ukataliwe kinaga ubaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania ichukue hatua na ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze atafanya nini kuishitaki Serikali ya Uingereza itulipe fidia kwa hasara zote ambazo tunazipata kutokana na mkataba huu ambao ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema yafuatayo, sisi tunakwenda mita 200 Singida, tumechimba Visima Ilongelo na sehemu nyingine, *you go up to 250 metre deep* hakuna maji. Gharama ya kuchimba kisima kimoja kama ingekuwa na *distribution mechanism* kutoka Ziwa Victoria, ikasambaza maji mpaka makao makuu ya nchi, tungeweza kumaliza theluthi moja ya matatizo ya maji Tanzania na huu mradi hauwezi hata kufikia gharama ya hii waiata Bwawa la Aswadi ambalo limegharamiwa zaidi ya dola za kimarekani bilioni moja na hata wao walienda Urusi *(USSR* ya zamani) ndio ikawapa Wamisri fedha za kujenga lile *dam.* Inawezekana tusipate fedha zote lakini ukichanganya kukopa na kuchanganya na fedha zetu za muda mrefu tunaweza kujenga mradi mkubwa utakao kuja hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mapendekezo yangu kuwa ule mradi uanze kubuniwa na ni mapendekezo yangu kuwa Serikali ya Uingereza ishitakiwe kulipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Pia napenda nitumie fursa hii kuungana na wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwa kuomboleza msiba wa ndugu yetu rafiki yetu, Mheshimiwa mwenzetu Amina Chifupa, tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Spika, bila shaka utakubaliana na mimi kwamba maji ni uhai, vile vile kwamba maji ndiyo bidhaa pekee duniani ambayo kila kukicha, kila mwanadamu anaitumia lakini kwa bahati mbaya bidhaa hii bado ni adimu sana katika Jimbo langu la Mwibara na hasa katika vijiji vya Igundu, Kwilamba, Bulomba, Mchigondo, Nasimo, Magunda, Kwilili na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la maji linawafanya wananchi wa Jimbo la Mwibara walio wengi waamke usiku wa manane na kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta maji, kwa bahati mbaya wananchi wengi ambao wanapata tatizo hili ni

wanawake ambao wanatumia muda wao mwingi katika kutafuta maji na hivyo kushindwa kushiriki katika shughuli nyingine za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali yetu iko serious katika kuwakomboa wanawake naomba Serikali yetu kwanza iwapatie wananchi maji ili wanawake ambao ndiyo wanaosumbuliwa na tatizo hili na wao waweze kuwa na *free time* waweze kufanya shughuli nyingine za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa Serikali yetu ina nia njema na ya dhati ya kutatua tatizo hili lakini kuna baadhi ya maamuzi ambayo nafikiri kwamba huenda yakasababisha kufanikisha kwa lengo hili likawa ni gumu kidogo. Kwa mfano, ukiangalia katika Bajeti yetu pesa ambazo zinatolewa katika kukabiliana na tatizo hili bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba Serikali inategemea sana pesa za wafadhili, ukiangalia katika Bajeti hata ya mwaka huu katika kila mradi mkubwa wa maji, pesa zinazotumika ni pesa za wafadhili, sasa kama Serikali inatambua ukubwa wa tatizo hili na unyeti wa tatizo hili ninapenda kuona kuanzia mwakani na Serikali yenyewe inatoa pesa za kutosha zinazotokana na mapato yetu ya ndani kuweza kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho naona huenda kikatukwaza mpaka muda huu sijaona programu ya Wizara ambayo inaonyesha kwamba kwa mfano mwaka huu ni vijiji kadhaa vya Mikoa kadhaa ambavyo vitapatiwa maji na kwamba baada ya hapo tukajua kwamba mwaka unaokuja vile vile ni vijiji kadhaa. Sasa kwa jinsi ambavyo Wizara inakwenda tutashindwa baadaye na hata Wizara yenyewe itashindwa kufanya *assessment* ya maana ya kuonyesha kwamba sasa tatizo la maji ambalo wameshalitatua ni kiasi kadhaa ama vijiji kadhaa vimeshapewa maji. Kwa hiyo, hii na yenyewe naona kwamba ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni uamuzi wa Serikali wa kuamua kutopeleka miradi katika Halmashauri ambazo zimepata hati chafu. Hapa mimi napata kigugumizi kwa sababu wananchi hawahusiki katika kusababisha hati kuwa chafu, wanaosababisha ni Watendaji wa Halmashauri, sasa kama ni kuadhibiwa usipopeleka miradi wanaoadhibiwa ni wananchi na wala siyo viongozi au watendaji wa kwenye Halmashauri.

Mimi naiomba Serikali isipate kigugumizi kuwaadhibu watendaji na badala yake kuwaadhibu wananchi, kwa hiyo, naona kwamba Serikali ibadilishe uamuzi wake ili kwamba miradi iende kote licha ya matatizo ya hati chafu au zurni ili wananchi wasiweze kuadhibiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba katika Bajeti ya mwaka huu nilipokuwa napitia katika kitabu cha miradi, kuna mradi wa maji ambao unaitwa *Rural Water Supply and Sanitation* iko katika programu na nilipokuwa naangalia nikakuta kwamba kuna baadhi ya Mikoa ambayo imepata mabilioni ya pesa katika miradi hiyo, lakini mkoa wangu na baadhi ya Mikoa kama miwili haikupata. Nilipokutana na uongozi wa Wizara hii yaani katika *level* ya Mawaziri wakasema kwamba wao hizi pesa

hazikupita moja kwa moja katika Wizara ya Maji bali zilitolewa moja kwa moja na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama Wizara ya Fedha inakuwa na nguvu kiasi hiki kwamba inapata pesa halafu haishirikishi Wizara husika katika kuona namna ya kuzigawa hapa kutakuwa na matatizo makubwa. Mimi nafikiria kwamba kwa busara Wizara ya Fedha basi iwe inashirikiana na Wizara zinazohusika katika kuzigawa hizi pesa ili kuweza kurekebisha kasoro zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ninaloliona ni hii zana ya *Development by Devolution* tunasema kwamba madaraka yote yamekwenda katika Halmashauri zetu, lakini kama tutaachia Halmashauri zetu ndiyo zifuatilie kila aina ya mradi kwanza naona kuna matatizo mengi la kwanza ni *capacity*.

Halmashauri zetu nyingi sana uwezo wao ni mdogo sana na hilo liko wazi, lakini kitu kingine ni kwamba kama Wizara katika *level* ya Wizara hazitaweza kufuatilia moja kwa moja *then* tutawezaje kujua ni nani afuatilie. Hii nazungumzia kwa sababu katika hoja ya jana Wizara ya Afya nilipomuhoji Waziri wa Afya kuhusiana na matatizo yanayojitokeza akasema kwamba katika *level* ya Wizara siyo wa kulaumiwa, sasa kama wao Wizara hailaumiwi tukizilaumu Halmashauri *then* Wizara inafanya kazi gani katika kuwajibika katika hizi Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kujua ni namna gani katika *level* ya Wizara inaweza kupata takwimu au hali halisi ya utekelezaji kama Wizara zetu haziwezi ku-*get involved* moja kwa moja katika kuona utekelezaji wa miradi hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeomba kwamba tusitumie muda mrefu nami nakubali, kwa hiyo, naomba niishie hapa kwa kuiomba Serikali yetu iangalie masuala haya kwa makini ili tuweze kutatua matatizo ambayo yanatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwako Mheshimiwa Charles Kajege na kwa ufanisi mkubwa ambao utawezesha na wengine nao waweze kupata nafasi. Ni zamu sasa ya Mheshimiwa Paschal Degera wa Kondoa Kusini atafuatiwa na jirani yake hapo hapo Mheshimiwa Estherina Kilasi na ajiendae pengine kama itawezekana Mheshimwa Dr. Wilbrod Slaa, lakini kama asipopata nafasi atapata nafasi ya jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paschal C. Degera, karibu.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya leo na mimi niweze kuchangia hotuba ambayo Waziri wa Maji ameisoma leo. *(Makofi)*

Kabla sijatoa mchango wangu naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Kusini kutoa rambirambi zangu kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nifanye marekebisho kidogo ya mambo ambayo yalitajwa katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii alitaja jina langu ukurasa wa 10. Sasa napenda nimhakikishie ama nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Rais wakati alipofika Kondoa kwenye Kampeni sina hakika kama ni tarehe hiyo lakini alitoa ahadi ya kutoa shilingi hizo milioni 680 na hiyo ahadi imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahadi hiyo imetekelezwa na huo ni mradi ambao ulikuwa ni kuboresha mfumo wa maji Mjini Kondoa na hivi sasa kazi ya kuboresha mfumo huu inaendelea vizuri kwa hiyo, Rais katekeleza ahadi yake lakini matatizo ya maji bado yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba mimi niende moja kwa moja Jimboni kwangu. Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini na hususan wa vijiji vifuatavyo:-

Naomba radhi nivitaje vijiji vyote 17, vijiji vya Vyejeruse, Ngoima, Milambo, Igunga, Songoro, Madaha, Chiori, Hamai, Mtakuja, Kikima, Chukuru, Jinjo, Changalo, Itorwa, Mlongia, Mapango na Chandama vya Jimbo la Kondoa Kusini wamenituma niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi hao wanasikitika sana kwa kunyimwa maji kwa mfululizo wa miaka miwili na nitaeleza kwa nini wamesema hivyo; na wananchi hao wanasema hivi, Waziri wa Maji amewaonea kwa kuwanyima maji hivyo vijiji 17. Kwa nini wanasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, katika vijiji hivyo wananchi wapatao kama 50,000 ndiyo wanaoishi katika vijiji hivyo. Hao wananchi wanategemea chanzo kimoja tu cha maji Mtaro wa Ntomoko, hawana chanzo kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo Bunge lako Tukufu, tangu uasisiwe mradi huo na Marehemu Baba wa Taifa, Bunge lakoTukufu limekuwa likipitisha fedha kila mwaka kuhudumia mradi huo. Napenda kulishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kufanya hivyo. Lakini kinachonisikitisha ni kwamba kwa miaka miwili, 2005/2006 na 2006/2007 fedha zilitengwa, lakini hakuna hata senti tano iliyopelekwa kwenye Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2005/2006 shilingi milioni 30 zilitengwa ili ziweze kwenda kuhudumia mradi huo ili wananchi waweze kupata maji, lakini hakuna hata senti tano iliyopelekwa mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, wakati nilipokuwa nachangia katika Wizara ya Fedha mwaka jana nilisema hili kwamba tunanyimwa fedha na huduma za maji zimesimama katika mtaro huo. Hapa majibu ya Serikali ilikuwa ni kwamba wanakwenda kuangalia namna ya kusaidia, lakini hakuna kilichofanyika mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 kama ilivyokuwa imedhihirishwa katika swali langu la leo, Bunge lako Tukufu lilipitisha shilingi milioni 100 kwa kujua tatizo la maji katika eneo hilo, na kwa kujua kwamba mradi huo haungeweza kufanya kazi kama tusingetenga fedha. Sikuwepo leo wakati swali langu linaulizwa, lakini Waziri mwenyewe amekiri kwamba hajapeleka hata senti tano mpaka leo. Ndiyo maana wananchi wa vijiji hivyo 17 kwa kweli wanasikitika sana kwa Serikali kuwanyima maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu ni sikitiko kubwa, lakini jibu la Naibu Waziri amesema mradi huo haujafa. Lakini katika jibu lake kasema vijiji 16 sijui kwa nini kijiji kimoja amekipunguza, ni vijiji sita tu ndivyo vinavyopata huduma ya maji. Sasa alichosema kwamba mradi haujafa na alichokuwa anajibu sielewi ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli matokeo ya kutokupeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ni yafuatayo, mradi huo wote umevurugika sasa hivi kwa hiyo, huduma hakuna hata hivyo vijiji sita alivyosema sivifahamu mimi, labda vipo katika Jimbo la Kondoa Kaskazini sina uhakika. Lakini katika Jimbo la Kondoa Kusini hakuna hata kijiji kimoja ambacho kinapata huduma ya maji mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kuvurugika kwa mradi huo ni kwamba wananchi hao wa vijiji nilivyovitaja wapatao 50,000 hawana maji kabisa hivi sasa wanahangaika kweli kweli. Matokeo zaidi ni kwamba wananchi wengi katika vijiji hivyo 17 hawafanyi kazi zingine za maendeleo licha ya kutafuta maji usiku na mchana; na mbaya zaidi sasa hivi ni kwamba wanyang'anyana maji na wanyama wakali kama fisi, simba, chui na tayari akinamama wanne wamekwishambuliwa na wanyama hao wakali na wapo hospitali wamelazwa. Lakini hapa Serikali inasema kwamba huduma ya maji inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kibaya ni kwamba wananchi kwa kuwa maji wanayotafuta huko; na mimi mahali wanakoyatafuta sipaelewi na matokeo yake wanatafuta maji machafu na hivyo kudhurika sana na magonjwa mbalimbali kama Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, athari za kutokuhudumia mtaro huo ni nyingi. Sasa naisihi Serikali ichukue hatua za dhati kukabiliana na tatizo hili na siyo kukaa mezani na kutoa majibu ambayo hayaridhishi.

Mheshimiwa Spika, napenda niwambie wapiga kura katika eneo hilo wamekwishanipigia simu kwamba hawakuridhishwa kabisa na jibu la swali langu la leo. Hiyo nawahakikishieni wamenipigia simu tayari. Kwa hiyo, majibu yanayotolewa hapa hayaridhishi na wananchi wanakiri kabisa kwamba hawakuridhika. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, ulitukataza kwamba tusiwaombe Naibu Mawaziri, kwa hiyo, namwomba Waziri atembelee eneo hilo ajihakikishie mwenyewe hali halisi ya mtaro wa Ntomoko.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba hizo fedha shilingi milioni 100 zitolewe ili mradi huo ukarabatiwe, vinginevyo shughuli nyingi hazitafanyika hata ujenzi wa sekondari utakwama kwa sababu sasa hivi hawajengi. Kwanza, maji ya kunywa ama maji ya kutumia nyumbani hayapatikani, mifugo inapata matatizo, utafute tena maji ya kujenga shule kweli inawezekana!

Mheshimiwa Spika, pia naomba kama fedha zitatolewa tunaomba Mhandisi toka Wizarani aende akasimamie, hatuna Mhandisi katika Wilaya ya Kondoa. Kutokana na hilo naomba Mhandisi mzoefu kwa ajili ya Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kwa kweli Serikali ichukue hatua zaidi. Sisi katika maeneo haya kama Mheshimiwa Lazaro Nyalandu alivyosema ni kwamba ni shida sana kupata maji ya visima virefu na ndiyo maana uliasisiwa mtaro huo. Sasa kama mtaro huo hatuwezi kuutunza sijui tutakuwa na chanzo kingine kipi cha kuwapatia wananchi wa eneo hilo huduma ya maji. Lakini kama kuna chanzo kingine sisi tunaomba basi katika hayo mabwawa ambayo tumeyatengea fedha basi tunaomba hata mabwawa machache yachimbwe katika eneo hilo ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende kwenye eneo la pili. Eneo la pili, ni huu mradi wa maji na usafi wa mazingira. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametaja mradi huo na katika maelezo yake amesema kwamba Wilaya 14 zinazotekeleza mradi huo utekelezaji wake umefikia asilimia 85. Sijui kama ni kweli. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba kasi ya kutekeleza mradi huo wa maji na usafi wa mazingira vijijini ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa ilianza kutekeleza mradi huo mwaka 2005, lakini mpaka leo hakuna mradi mmoja uliokamilika. Kwa hiyo, mnaweza kuona wananchi bado wana shida, lakini mradi unasuasua na tatizo lake ni nini, ni urasimu tu. Tatizo lake ni urasimu, kwa hiyo, naomba basi urasimu upunguzwe ili angalau ile miradi ya Benki ya Dunia iweze kutekelezwa kwa kasi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza anafuatia Mheshimiwa Estherina Kilasi na tutaona kama muda utakuwepo kwa mchangiaji ambaye anafuatia ambaye ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo hii, hoja ya Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mimi naomba nianze kwa kuwapongeza Wizara hii ya Maji kwa kazi nzuri kwa kweli ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kipindi hiki ambacho wameshika Wizara hii. Unapofanyiwa mazuri ni lazima ushukuru. Mimi ninampongeza Waziri mwenyewe na Naibu Waziri. Kwa kweli Naibu Waziri amekuwa ni kielelezo kizuri sana kwamba hafanyi kazi akiwa mezani, anafanya kazi kwenye mazingira yote na hii inajidhirisha pale anapojibu maswali. Kwa sababu anajibu swali mahali anapafahamu na amefika inakuwa ni fasaha zaidi kuliko anavyoletewa majibu na wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nachukua nafasi hii kumshukuru kwa sababu mara ya mwisho ametembelea Wilayani kwangu Mbarali, tulizunguka kwenye vijiji na nilipowambia wananchi Naibu Waziri wa Maji anakuja walifurika kwa wingi sana; na hii ilinionyesha jinsi watu wanavyokuwa na kiu ya tatizo la maji. Maji ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu. Kuna mahali unakaa, namshukuru Mheshimiwa Lazaro Nyalandu amelichangia kwa utaalamu zaidi ni kwamba mwenzetu amesoma na akaona ni kitu gani ambacho kingeweza kusaidia Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, tulipata matumaini tu mazuri kwamba ili kuweza kugawa sawa kwa Wilaya zote za Tanzania nzima, sharti waende kwa awamu kwa maana ya vijiji 10 kwa kila Wilaya, wakikamilisha tutakuwa tumejua tumefikia asilimia ngapi, na nyote ni katika kufanikisha Ilani ya Uchaguzi ambapo ndani ya miaka mitano tunategemea Serikali ya Chama cha Mapinduzi iwe imepunguza tatizo la maji vijijini kwa asilimia 65. Ukisema vijijini kwa asilimia 65 maana yake ni Mikoa yote na Wilaya zote, lakini vile vile kwa Miji kwa asilimia 90. Kwa maana ya kuwa tusione ndoo tena Jiji Dar es Salaam katikati watu wanatembea na mikokoteni wamebeba maji. Kwa hiyo, hilo nafikiri kwamba tutaenda sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hali inavyokwenda na Bajeti tunayoiona sasa ni ndogo haiwezi kukamilisha zoezi hilo miaka iliyobaki ni miwili. Sasa sijui wenzetu watuambie wamejipanga vipi na sasa tunaachana. Kwa sababu fedha tunazotegemewa nyingi ni za wafadhili na wafadhili wana masharti yao. Leo nimeuliza swali langu la nyongeza kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Paschal Degera hapa kwa sababu imenigusa kwamba Halmashauri yangu na zingine 11, mwaka jana zilikuwa kama Halmashauri thelathini na kitu hazikupata fedha, mwaka huu zimepungua zimebaki Halmashauri 12. Lakini tulipangiwa tupate maji vijiji 10 na Mheshimiwa Naibu Waziri alipopita huko kote alitoa maelezo hayo na wananchi wapo tayari kuchangia, lakini tunategemea fedha za wafadhili, sasa hawatapata maji.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingine tutakapokuwa tumefikia hivyo vigezo maana yake Wilaya zingine zitakuwa zipo mbali kuliko Wilaya zingine. Hivi hatuweza kuwa na fedha zetu wenyewe zingine kama walivyochangia wenzangu kwamba pale ambao tumeshindwa kukidhi masharti na vigezo vya wafadhili basi hizo fedha zitumike kupunguza tatizo la maji. Kwa sababu tuna ahadi mbili hapa, ya kukamilisha Ilani ya Uchaguzi na vile vile kutatua tatizo la maji kwa wananchi ambao wana shida ya maji sawa sawa kwa nchi nzima. Sasa hapa tunaachana, ningeomba Mheshimiwa Waziri afikirie ni jinsi gani ya kushughulikia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi kosa si la wananchi na wala siyo la wawakilishi ni la wataalamu. Nyie wenzetu tukija Waheshimiwa Wabunge, kuwaambia kwamba huko kuna tatizo ni lazima mtusikilize. Unaweza ukapiga *mark time* Wizarani unasema mtaalamu huyo hana uwezo basi abadilishwe uletewe mwingine inachukua miaka miwili, mitatu mpaka tunapofikia hapo. Mimi nilikuwa na Mhandisi wa Wilaya ya Maji mmoja pekee yake katika Wilaya nzima yenye ukubwa wa kilomita 16,000 na Kata mbalimbali, azunguke, aainishe matatizo ya maji, inamchukua muda, mke wake ndiyo mchoraji wa ramani zote. Sasa kweli hiyo kazi itafanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninashukuru kwa mwaka huu kwamba nimeongezewa Mhandisi mmoja wa Maji angalau kazi itakwenda vizuri. Nilitaka niliseme hilo. Lakini vinginevyo sina tatizo kwa Wizara hii, ninapopeleka kilio changu wamekuwa wakinitekelezea kazi kwa haraka sana na inakamilika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna Mradi wa Maji wa Madibira ambao umetajwa hapa na Mheshimiwa Waziri ulianza mwaka 2003 na umekuwa ukipewa fedha kidogo. Sasa juzi tulipata milioni 15 nilitaka nilisema hili; na wananchi wamechimba mitaro kwa mikono yao na mabomba hayakuweza kutosha. Sasa mwaka huu walitakiwa wapewe fedha zingine, lakini kutokana na hilo tatizo sijui kama utakamilika. Sasa nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, wananchi wametumia nguvu zao zote na kila siku wananipigia simu sasa mitaro bado na yanahitajika mabomba mia moja na kitu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa jicho la pekee kuhakikisha kwamba mnaunga mkono wananchi hao na huo mradi umechukua miaka mitatu bado mabomba 125 tu na kupata tanki la maji ambalo halitagharimu zaidi ya milioni 18 ili liweze kukamilika. Kwa hiyo, hili nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake, awaambie wananchi wa Mbarali hasa Kata ya Madibira kwamba sasa tatizo lao litatatuliwa haraka sana iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchimbaji wa mabwawa, hili tumekuwa tukilizungumza kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, sehemu kame kama hizo za kwangu na katika Wilaya zingine. Mabwawa yangekuwa ni *solution* kubwa sana ikilinganishwa na fedha ambazo tunazitumia kuchimba visima vifupi ambavyo vikichimbwa gharama zake ni zaidi ya shilingi milioni 8 kwa kisima kifupi. Visima vingine ni zaidi ya shilingi milioni 100 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa Wilayani kwangu nina mfano mzuri, visima 84 vilichimbwa, visima vinavyofanya kazi ni 14 tu, ni fedha ngapi ambazo tumezitumia katika kuchimba hivyo visima. Tungechimba bwawa moja likavuna maji ambayo yangetumika kabisa kutawanya maji na vijiji vingi vingeweza kupata maji. Sasa ndiyo maana Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kasema tuna huo mradi wa Ziwa Victoria ungeweza kutawanya maji katika Mikoa mingine. Hapo tungechimba bwawa kubwa likakinga maji na kuyatawanya kwenye vijiji kungeweza kusaidia. Sasa la msingi wataalamu watusaidie kwenye Wizara yake Mheshimiwa Waziri kuainisha na kufanya hayo maandiko kwamba tutatatua namna gani tatizo hilo. Mabwawa mangapi makubwa au visima virefu vingapi badala ya kutoa hizo fedha ndogo ndogo za kuchimba visima

vifupi vinafanya kazi mwaka mmoja, mwaka wa pili vinakuwa havitoi maji tena. Maana yake vinajiziba.

Mheshimiwa Spika, la tatu, kwa upande kwa Wakala wa Wachimbaji Visima vya Maji, vifaa walivyonavyo. Walikuja kule kwangu karibu vijiji vitano wamechimba visima vya maji bila kupata mafanikio. Lakini uchimbaji wao gharama yao ni kama shilingi milioni sita na nusu na wananchi wanakuwa wamechangia zile fedha. Wakichimba wakimaliza fedha zinalipwa, lakini maji yanakuwa hayatoki, lakini maji wanakuwa hawajayapata kwa sababu gharama tayari wameshazitumia.

Mheshimiwa Spika, sasa tunauliza je, hakuna vifaa ambavyo vinaweza kutumia kupima kujua kama hapo kuna maji au hakuna maji. Kwa sababu wanakuwa kama wanabahatisha. Kuna kijiji kama cha Kanganga, Maogele, Maramba, Ikonga, visima vyote vilichimbwa kwa zaidi ya milioni sita kwa kila kisima, lakini visima vinachimbwa mpaka mwisho lakini havitoi maji na wenyewe wanakiri kwamba hapo kwa kweli hakuna maji. Ukiwauliza vipimio wanasema vipimio walivyopima palionyesha kwamba kuna maji, lakini wanapomaliza kuchimba kisima maji hakuna.

Kwa hiyo, wanahitaji kusaidiwa kwa kweli kupata vifaa ambavyo vitasaidia kuainisha sehemu ambazo kwa kweli wachimba kisima watapata maji. Mashine zao zinazunguka Tanzania nzima ni kidogo wanakwenda kwa awamu hapa leo, kesho kwingine. Kwa hiyo, wanachukua muda mrefu sana kuweza kukamilisha zoezi la uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kama nilivyosema yaliyonigusa zaidi ni hayo, kuomba Wizara ya Maji iangalie kwa jicho la pekee, tumejipanga vizuri sisi pale Mbarali katika kutunza vyanzo vya maji, Hefya mnaifahamu, lakini siyo chanzo cha maji, sisi tunapokea maji. Wenzetu wanaozunguka Wilaya ya Mbarali kwa mfano, Wilaya ya Njombe na Makete mito yao ndiyo inayotiririsha maji kuleta kule Mbarali. Kwa hiyo, na sisi tunaomba watuangalie kwa jicho la pekee kuhakikisha kwamba tunapata maji ni sehemu kame halina maji, lakini na wenzetu wanaozunguka Wilaya ile wasaidiwe ili waweze kutunza vyanzo vya maji kusudi mito ile ambayo inatiririsha maji isikauke mapema na hatimaye na sisi tupate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Estherina Kilasi ahsante sana. Tunazo kama dakika 12 nimeletewa taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Ania Chaurembo anaweza kuzitumia vizuri kabisa. Kwa hiyo, namwita yeye. Halafu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ataanza kuchangia saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa ningependa kuzungumza kuhusu habari ya maji kama tunavyofahamu maji ni uhai kama walivyotangulia wenzangu kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji ambalo lina watu wengi sana na limekuwa na tatizo sugu la maji katika maeneo mbalimbali kama Mheshimiwa Waziri

alivyokiri hapa katika hotuba yake. Lakini nimefarijika kidogo kuona limepewa kipaumbele Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa ndiyo Jiji la Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la miundombinu ya majitaka katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam sasa hivi ukienda katika mitaa mbalimbali utakuta kuna maji taka ambayo yanatoka katika mashimo ambayo hayana vifuniko vya kufunikia; na katika utafiti tuliofanya imeonekana kwamba kuna baadhi ya watu wanaiba vile vifuniko ambavyo vinafunikia hayo mashimbo ya majitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kwa sababu maji yale ni maji ambayo siyo salama, yanatoka katika vyoo, hutiririka katika majumba makubwa na itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, alizuia ujenzi wa nyumba za maghorofa katika eneo la Kariakoo. Baadaye akaja akaruhusu kwa sababu alisema kwamba miundombinu ya majitaka haiwezi kutosheleza ujenzi wa maghorofa katika eneo la Kariakoo. Sasa kwa akili yangu naangalia kabla ya hiyo miundombinu yenyewe haijaboreshwa majengo ya maghorofa tena yameruhusiwa kujengwa katika eneo la Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari zake sasa ni msongamano wa majitaka unashindwa kufika baharini na matokeo yake yanasambaa tu ukienda Mtaa wa Mkunguni sasa hivi karibu na Mtaa wa Sikukuu utakuta kuna majitaka ya chooni na pale kuna soko la Kariakoo, ukija Mtaa wa Msimbazi hali kadhalika. Kwa hiyo, katika hali hii naomba huo utaalamu ambao unafanywa sasa hivi kuhusu kufuatilia miundombinu yote ya majitaka ufanywe kwa haraka zaidi kwa sababu athari kubwa zinaweza zikatokea na wananchi wengi watapata matatizo ya kipindupindu na kuharisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam sasa hivi ikinyesha mvua mafuriko yanakuwa makubwa na mimi kidogo hapo nachanganyikiwa. Kwa sababu nikiangalia pale eneo ambalo lipo Dar es Salaam lipo chini ya Bahari ya Hindi na Bahari inameza maji ya chumvi na maji ambayo yanatoka katika mito yote ya Tanzania. Sasa ni kitu gani ambacho kinazuia Serikali kuboresha vizuri hiyo miundombinu ambapo ikinyesha mvua maji katika Jiji la Dar es Salaam isiwe tena mafuriko, ni aibu sana kusikia Jiji lile linakuwa na mafuriko wakati ukitazama pembeni unakuta kuna Mto Msimbazi, ukiangalia kuna Mto Wami unaingia, ukiangalia bahari yenyewe iko karibu kabisa kwa mfano, *Salander Bridge,* ile barabara ya shule ya Tambaza kila ikinyesha mvua inajaa maji kwanza, halafu baadaye maji ndiyo yanatoka. Hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli suala hili litiliwe mkazo. Dar es Salaam lisiwe Jiji ambalo lina mafuriko ya maji ya mvua. Vile vile naomba Serikali iangalie wananchi ambao wanapata mafuriko katika maeneo siku za mvua. Malalamiko makubwa ya wananchi ni kwamba kuna watu matajiri wamepewa maeneo wamejenga nyumba zimeziba mifereji ya majitaka ambayo ingepeleka maji baharini na nyumba zao zipo zimejengwa na Serikali inaziona nyumba zile. Tunaomba basi Serikali iangalie nyumba zile. Kwa mfano hai ni sehemu moja iko Sinza kuna mtu akajenga nyumba ya ghorofa nne katika mfereji wa majitaka na mfano mwingine wananchi wamekuwa wakilalamika katika bonde la mpunga la Msasani, kuna mtu tajiri kaziba mfereji unaosababisha

wananchi wengi wanapata matatizo na tulishuhudia watoto wakitembea ndani ya majitaka ili kutoka ndani ya nyumba na nyumba zote zimefurika majitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili Wizara iliangalie kwa makini sana. Jiji la Dar es Salaam ni Jiji la Ikulu, si vizuri Jiji lile likawa linapata aibu ya majitaka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nilikuwa nataka kuzungumzia kidogo kuhusu suala la maji salama. Kumekuwa kunachimbwa visima katika maeneo mbalimbali, lakini visima vile vingine havitoi maji na inavyosemekana kutokana na maelezo ya Waziri ni kwamba kwanza unafanywa utafiti halafu ndiyo kinachimbwa kisima.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashindwa kuelewa. Ni kwa sababu zipi ambazo zinafanya kisima kinachimbwa halafu baada ya muda maji yanapotea. Kwa hiyo, waangaliwe hao wataalamu ambao wanapewa vibali vya kufanya utafiti katika maeneo ya kuchimba visima kabla ya watu hawajaruhusiwa kutumia gharama zao za kuchimba visima hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia kwa hakika hautoshi kabisa ni dakika nne au tano hivi hazitoshi kwa mchangiaji yeyote. Kwa hiyo, saa 11.00 jioni tutakuwa na wachangiaji wawili. Tutaanza na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na tutahimitisha na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Baada ya hapo sasa ataanza Naibu Waziri wa Maji aweze kujibu hoja na baada ya hapo ni mtoa hoja mwenye Mheshimiwa Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nikumbushe tu kwamba kuna maonyesho ya vitabu na machapisho na majarida ya Chuo Kikuu Huria yapo katika eneo letu la tafirija. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu elimu ndiyo kitu muhimu basi tusikose kuwaunga mkono Chuo Kikuu Huria kwa kwenda kuangalia hayo. Kwa sasa naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea niseme tu kwamba baada ya wachangiaji wawili basi kama nilivyotamka mapema tutarejea kwa Wizara ambao Naibu Waziri atagawana muda na Mheshimiwa Waziri. Muda wao wawili ni dakika 75. Dakika 15 za Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kama ameongezewa na Mheshimiwa Waziri basi atakuwa amepunguza kutoka kwenye dakika 60 za Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunaendelea namwita sasa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kwa mchana huu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa kuwa si mara yangu ya kwanza kuzungumza katika ukumbi huu moja kwa moja naomba niende

kwenye hoja na nitajielekeza zaidi katika hoja kubwa mbili, moja ya Kitaifa na moja zaidi ya jimbo langu. Labda nianze na hoja ya Kitaifa.

Kwa kuwa vile vile nimeiandika hoja hii kwa maandishi basi nitapenda Mheshimiwa Waziri wakati wa majibu anijibu kikamilifu ni kuhusu suala la *City Water,* nilikuwa nimeomba Waziri anipe ufafanuzi kuhusu masuala kadhaa na mimi ninaelewa kwamba suala hili sasa hivi liko kwenye kitu kinachoitwa *arbitration,* kinafanana na Mahakama kwa hiyo, sihitaji undani wa kuzungumzia kilichoko kwenye *arbitration.* Lakini nitapenda Waziri anipe maelezo kwanza kama taarifa tulizosoma kwenye vyombo vya habari ni kweli na kwamba tunadaiwa fedha nyingi sana kwa taarifa zilizoko kutoka kwenye vyombo vya habari, pia kwa taarifa nilizonazo tunadaiwa zaidi ya dola za Marekani 164,000,000. Sasa hizi ni fedha nyingi ni zaidi ya fedha za Bajeti labda Wizara mbili au tatu lakini sisi Watanzania hatujapewa taarifa, nimepitia kitabu cha Waziri sikuona kwenye hotuba ya Waziri akieleza chochote kuhusu suala hili, kwa hiyo nitapenda anipe taarifa ya kina. *(Makofi)*

Lakini vile vile ninajua kwamba kutokana na uzito wa jambo hili sisi tunapata taarifa kutoka nje na nisingependa tuwe tunapokea taarifa kutoka nje wakati tuna Bunge letu tunaweza kuihoji na ikatueleza. Kuna *Centre for International Environmental Law* ambayo iko *based* kule Geneva pamoja na *International Institute for Sustainable Development* ndiyo wanaotusaidia katika kesi hii lakini Serikali haisemi kitu na ningependa Serikali itoe kauli na namna gani tutawasaidia kwa sababu hawa wamejitolea kutusaidia ili fedha hizi nyingi sana tusije tukashindwa huko Mahakamani kwa hiyo wanasimama kwa upande wa Serikali na hilo wanashirikiana na Shirika linaloitwa *LEAT* la kwetu pamoja na *TGNP* ningependa kwanza niwapongeze hayo Mashirika pamoja na hayo ya nje kwa kutuonea sisi huruma na kutaka kutusaidia ili fedha hizi nyingi tutakapofika mahali tusiwe basi tumeathirika. Lakini ningependa yote niliyouliza Waziri anipe ufafanuzi wa kina na maelezo ili tujue ni kitu gani kinaendelea na kesi iko wapi na iko kwenye hatua gani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningependa kuligusia kidogo la kisera. Mheshimiwa Waziri mwaka jana nilikuwa nimeomba na iko kwenye kitabu cha *Hansard* ukurasa wa 11 suala la *Water Rights.* Suala la *Water Rights* lipo, nimelivalia njuga toka mwaka wa 1998 na hatimaye Maafisa wa Wizara ya Maji walikuja mpaka Karatu wamepima vyanzo vyetu na hatimaye wakaniambia namna na njia pekee ya kuweza kubadilisha au kurekebisha hizi *Water Right* ni kwa kuleta sheria mpya. Sasa toka mwaka 1998 hadi leo ni muda mrefu sheria hiyo haijafika, Waziri anaongelea bado kutumia Sheria ya mwaka 1978 Na. 42 lakini hakuna mkakati anaouzungumzia kwamba sheria hii mpya sasa italetwa lini ili wale watu waliopo chini ya vyanzo vya maji katika mashamba hasa ya mikataba na nimetaja ni mashamba ya mikataba katika vijiji vya Mang'ola Juu na katika maeneo ya Endashangwet ambapo wananchi walikaa katika maeneo hayo mapema kabla hata mashamba ya mikataba lakini wakubwa hao walipofika walichukua maji yote na watu walioko chini walikosa maji. Sasa tunahitaji utaratibu wa kisheria ili zile *Water Rights* ya zamani ambapo mto mmoja mzima unaweza kukabidhiwa mtu mmoja na wananchi wote wa chini wakakosa maji. Tungependa Serikali sasa ni lini italeta sheria hiyo ili hali hiyo ambayo inawahimiza wananchi iweze

kurekebishwa inavyotakiwa.  Lakini si Karatu tu hii sheria inaathiri vijiji vyetu vingi kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba nirejee sasa nizungumze kama Mbunge wa Karatu.  Kwanza napenda nimshukuru sana Naibu Waziri pamoja na Waziri wake kwa jinsi walivyokuwa wanatekeleza kazi zao lakini hasa kwa jinsi walivyokuwa makini kwa kupokea ushauri vile vile.  Mwaka jana nilitoa mapendekezo kwamba mradi wa Benki ya Dunia wa vijiji 10 uweze kupelekwa kwenye ngazi ya Halmashauri na isimamiwe katika ngazi hiyo.  Naona Mheshimiwa Waziri amelipokea hilo na fedha hizo sasa zinapelekwa kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba sisi Karatu tumejaribu hili, wananchi ukiwaamini inawezekana.  Nihakikishe tu kwamba katika vijiji vyetu vya Karatu 45, vijiji 35 leo vina maji na hii imewezekana kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe wanachangia nguvu zao wanatoa fedha na hata baada ya mradi kuwa tayari wanalipia au kuchangia maji kwa kiwango walichokubaliana wao, kwa hiyo, ukiwashirikisha inawezekana.  Kwa hiyo, katika miradi hii ya *Quick Wins* pamoja na vijiji 10 kwa kila Wilaya kwa nchi nzima mimi ninaunga pendekezo la Waziri kwamba fedha hizi zipelekwe kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee sana nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake, mwezi  Juni, 2007 tulipofika hapa nilikuwa nimemsumbua sana kuhusu fedha za *Quick Wins* zipelekwe hasa kule jimboni kwangu Karatu kwa sababu tulikuwa na mradi mwingine ambao unasaidiwa na wafadhili na wafadhili walitaka kuona Serikali yetu inasaidia nini kama ishara ya Serikali kuchangia hasa katika kijiji cha Rhotia. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba kabla ya mwisho wa Juni, 2007 fedha hizo zitapelekwa kwenye Halmashauri, naomba nitoe taarifa rasmi kwa Waziri kwamba fedha hizo zimeingia tayari kwenye Halmashauri na utaratibu wa utekelezaji unaendelea kwa kijiji cha Rhotia lakini pia kwa vijiji vya Endabash, Laja, Kansay, Qaru, Endamarariek, Bassodawish, Endallah na Khusmay. Kwa hiyo, nadhani ni jambo jema Waziri kama amefanya kazi njema tumshukuru kama siku zote tunavyosema sisi Upinzani huwa hatupingi na hasa tunapokuwa Wilaya tawala kama Karatu ambapo CHADEMA tumetwaa huwa hatupingi lakini tunasukuma ili maendeleo na malengo ya Kitaifa yaweze kukamilika.  Lakini alichosaidia Mheshimiwa Waziri kwamba kwa mradi wa Rhotia ilikuwa tukose fedha kutoka kwa wafadhili wetu wa *Saint Joseph* kule Marekani na hawa wafadhili wameshatuandikia sasa kwamba wako tayari watatusaidia kwa hiyo, bila ya kitendo cha Waziri kusukuma tusingepata fedha hizo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie vile vile kwamba katika fedha za miradi ya vijiji 10 Wilaya ya Karatu tunashukuru na kwa hili kabla ya kulizungumzia naomba nimshukuru Mkurugenzi wangu wa Halmashauri Bwana Oyer, pamoja na Baraza la Madiwani chini ya CHADEMA ambao wamesimamia vizuri mpaka tumepata hati safi na mpaka tumestahili kuingia katika mradi huu, sio mradi huu tu tumeingia kwenye miradi yote mikubwa.  Kwa kweli namshukuru kwa sababu kuingia huko ni jitihada kubwa sana ya Mkurugenzi pamoja na timu yake. Mara nyingi tumeambiwa kwamba kuna

migongano naomba nimhakikishie, Mheshimiwa Waziri Mkuu ananiangalia, Karatu hakuna tena mgongano, kuna ushirikiano na mshikamano kati ya Mkurugenzi na timu yake na tunafanya kazi vizuri sana. Sasa naomba vile vile pamoja na hayo unanikumbusha nimshukuru na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Lazaro. Sasa katika vijiji hivyo 10 na naomba nivitaje kwa sababu baadaye nitapenda kuzungumzia pia hivi vijiji ni vijiji vya Kansay, Laja, Bugeri, Getamok, Khusmay, Makhoromba, Endamarariek pamoja na Matala. Hivi vijiji vyote vimeingia wananchi wamekwishaandaliwa na naomba tu niseme sasa kwamba niombe mambo kadhaa Wizarani. Mwaka jana niliomba kwamba *bureaucracy* katika maandalizi ya miradi hasa ya Benki ya Dunia ni kubwa sana, muda wa maandalizi ni mrefu na bahati nzuri mimi nimekuwa mjumbe katika mikutano ya Kimataifa nikiwakilisha Bunge letu hasa kule *ACP EU* najua utaratibu wa vyombo hivi. Lakini ni vyema tukafanya utaratibu *bureaucracy* ikapunguzwa kwa sababu wananchi wanapongoja hasa mahali ambapo hakuna maji basi adha inakuwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye vijiji vingine watu hawalali mpaka leo na hasa katika vijiji hivi 10 kwa mfano Qaru wakati wa mwezi wa tisa au wa kumi watu wanalala nje wanasubiri maji kwenye foleni na hasa watoto wa shule na kwa utafiti nilioufanya hata watoto wa shule wanachelewa kwenda shule. Naomba nitoe hili kwa sababu Wilaya ya Karatu haina mto hata mmoja juu ya ardhi. Wilaya ya Karatu inategemea miradi ya maji inayotoka kilomita zaidi ya 15 au miradi ya visima virefu na kwa utaratibu huu mnaweza kuelewa tunapozungumza kwamba kwa Karatu maji ni uhai, nadhani Mheshimiwa Waziri atanielewa. Kwa hiyo, ninapotoa shukrani ni kwa misingi hiyo kwamba mtu yeyote anayetusaidia hata kama ni kwa kiasi kidogo tukapata maji Karatu sisi tunashukuru kwa sababu ni kuongeza uhai kwa watu wetu wa Wilaya Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza hili nilitaka vile vile Mheshimiwa Waziri nimwombe kitu kimoja. Wananchi wetu bado kwa sehemu kubwa hawajapata elimu ya hii sera ya kuchangia ningependa Waziri atusaidie na atoe tamko bayana ili wananchi wajue, kwanza sera yetu ya Taifa inazungumzia nini. Mathalani vijiji vya Karatu karibu katika vijiji vyote 45 tuna Bodi saba na katika Bodi saba, Bodi tatu tayari zimekwishakuelewa wanalipia maji na sisi wala hatuiti kuchangia tunalipia maji shilingi 5/= kwa ndoo. Sasa shilingi 5/= kwa ndoo imefanya maajabu makubwa sana na mfano mzuri ni pale kwenye Bodi ya Kaviwasu pale Karatu ambayo ni ya vijiji sita au Bodi ya Gyewasu. Naomba vijiji vilivyobaki na wao waige mfano mzuri kwa wenzao wa vijiji wa Kaviwasu na Gyewasu kwa sababu tunapolipia maji kwa kiwango hiki cha shilingi 5 kinaweza kuonekana kuwa ni nyingi sana lakini tukumbuke wakati wa shida ndoo moja tunalipia zaidi ya shilingi 300/= mpaka 500/=. Kwa hiyo unapopata shilingi 5/= kwa ndoo au shillingi 10/= kwa ndoo ni gharama ambayo ni ndogo sana lakini ni endelevu. Kwa hiyo, ningependa sera hiyo Waziri atusaidie iweze kuenea vizuri na tuweze kuwahamasisha wananchi wetu wakaielewa vizuri hii sera ya nchi yetu na hatuwezi kutegemea wafadhili milele. *(Makofi)*

Mfano mzuri ni kwamba kwenye Bodi ya Kaviwasu sisi tumeweza kulenga kwamba kwa miaka 20 ijayo katika mradi wa Kaviwasu tuna fedha za kutosha wenyewe kubadilisha mabomba yote katika vijiji sita kwa shilingi 5/= hizo. Sasa hii inaondoa ule

utegemezi kwa wafadhili na hii inatusaidia wakati wote mwananchi hakuna anayejua pale Karatu maji yanapatikana wapi, hakuna habari ya kwenda kufuata maji msituni, mafundi wanakwenda kwa sababu shilingi 5/= inafanya kazi zote. Kwa hiyo sisemi iwe shilingi 5/= lakini iangaliwe ni kiwango gani kwa kadri ya maeneo yanaweza. Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wa mwisho kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ni Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ambaye namwita sasa.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii nitachangia kwa ufupi sana na haraka. Naomba nizungumzie juu ya mabwawa ambapo Mheshimiwa Benedict Losurutia tayari ameshazungumzia, lakini nisisitize tu kwamba tunahitaji programu ya mabwawa katika Jimbo la Morogoro Kusini kwa sababu tumepata wafugaji ambao wamehamia. Sasa wafugaji hawa wanakuwa katika migogoro kila wakati na wakulima, kwa hiyo kuondoa migogoro wako tayari kuchangia mabwawa lakini programu ya mabwawa hakuna. Naomba tuanzishiwe programu ya mabwawa katika Kata za Mvuha, Tununguo, Kongwa na Dutumi, tafadhali sana hapo tutaondoa mgogoro kabisa kati ya wafugaji na wakulima. Wafugaji wanaopata mabwawa huko Kaskazini ndio wafugaji hao hao ambao wamehamia huko, kwa hiyo hakuna tofauti na hao jamaa. Tutaomba mtusaidie hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hoja yangu kubwa ni bwawa la Kidunda. Watu wa Morogoro Kusini hawana tatizo na uamuzi wa Serikali tangu ilipoanza ikatangazwa kwenye magazeti tukakubali, tukaelewa lakini limezuka tatizo la utekelezaji. Wapo watu wanakuja hawataki kuzungumza na *DC, DED* wala Katibu Tarafa na Mbunge na wao wanakuja kwa niaba ya Wizara ya Maji. Sasa tunataka kujua bahati nzuri nikawategea makusudi nikaelekeza uongozi wa Kata watu hao waishi kwenye mji wangu. Lakini hata nikifika hapo nikitaka kuzungumza nikiwaomba wanieleze nini kinatokea wanasema wao sio Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa lazima nimshukuru Naibu Waziri alifanya safari akaja kwangu akazungumza na wananchi na akaahidi kurudi tena kuja kufafanua, bahati mbaya hakupata muda, kazi ni nyingi. Lakini hawa watendaji, simwaliki Naibu Waziri namualika Waziri mwenyewe sasa hawa watendaji ambao wanakuja hawataki kutupa maelezo wanafanya nini? Wengine ukiuliza nao wanasema hao wanachukua *data* tu, wengine wanasema wao wanachukua habari ya mazingira na kwa bahati mbaya wanaokuja juu ya masuala ya mazingira wanatoka Zimbabwe, mimi nikajiuliza hivyo Tanzania hakuna wataalamu wa mazingira. Nikamuliza Waziri wa Mazingira akasema hao mimi siwajui. Ingekuwa wamekuja kutoka kwangu ningekueleza wengine wametoka Uganda kuja ku-*study* sijui wana-*study* kitu gani? Halafu anakuja wao anaweka alama kwenye nyumba za watu kwamba katika kijiji hiki, kitongoji hiki kinahama. Vitongoji vingine vyote vya kijiji vinabaki.

Mheshimiwa Spika, Mto Ruvu una mamba sana kule sehemu za *Selous* na kuzuia kujenga bwawa kule la Kidunda maana yake ni kuweka nafasi ya mamba kuongezeka

sana. Sasa unapohamisha Kitongoji tu katika kijiji unaacha kijiji hapo kabisa chote karibu na hilo bwawa maana yake nini? Hao hawataki kuwaeleza wananchi, hawataki kushirikiana na viongozi hata ngazi ya Wilaya wanatoka wapi? Nani anawaleta programu gani wanatekeleza. Nimeandika asubuhi kwa Mheshimiwa Waziri nikitegemea kwamba wataalamu wake watampa jibu tunataka tujue ni nani anayehusika na mpango wa kuhamisha wananchi hawa. Nani atakamilisha Sheria namba 3 ya Ardhi ya Vijiji ambayo inazungumzia mali za vijiji, nani atatuhamisha wapi? Nani atatulipa mali zetu? Nani atatulipa hata makaburi yetu, tuna mila ya kuhama nayo. Nani? Ni nani huyo ambaye atakuja kwetu kuzungumza na sisi kutuambia sasa ninyi wananchi wa Manyunywe, Vidwali, Kiburumo, Bulachini, Kiganila mhame, nani? Pamoja na Kidunda? Wananchi wapo tu hawajui sasa kinatokea nini wananiuliza tulime mwaka huu tusilime kuna nini kinatokea. Mheshimiwa Waziri nimeandika makusudi asubuhi ili upate nafasi na wataalamu watoe majibu kwa sababu wananchi hawa sasa wamekwama hatujui shule zetu tunapohama nani atawajibika kutujengea, *dispensary* zetu, nani atawajibika kutujengea? Sisi tutalipwaje, tunataka maelezo kwanza.

Mheshimiwa Spika, yupo *engineer* anaishi kwenye nyumba yangu anafanya kazi Kidunda kilomita 55 kila siku anakwenda na kurudi ana-*waste* hata dizeli ya Serikali tu angeweza kuishi huko huko. Lakini huyo hatoi jibu ashirikiane na viongozi, nani anawajibika katika swali hili? Wananchi wa Kata ya Serembala wanataka kujua nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi nilikuwa nimeamua nisiunge hoja mkono mpaka nipate jibu la kutosheleza. Lakini naona aibu kwa sababu yule Waziri ndugu yangu na Naibu Waziri shemeji yangu. Sasa katika masuala kama haya mara nyingine lazima uangalie unaweza ukakosa ugali nyumbani. Lakini ninaomba maelezo kama maelezo hayatoshelezi kwa kweli wakati wa Kamati nitakuwa mkali na pengine nita-*withdraw* hoja yangu niliyounga sasa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa ninalotaka kulizungumzia limetamkwa asubuhi. Tamko kabisa kijana hodari ndani ya Bunge hili amesimama ametamka haifai kuliacha tu.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu ametamka kwamba maji ya Ziwa Victoria ni maji yetu. Wabunge likitamkwa jambo kama hili ndani ya Bunge lazima Wabunge kuunga mkono kuonyesha ukweli huo na kitendo hiki kimeonyeshwa na Mheshimiwa Edward Lowassa wakati yuko Waziri wa Maji aliithibitishia dunia kwamba maji haya ni yetu na tutatengeneza mradi wa kupeleka maji Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi hatuna haja ya kwenda kushtaki Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, sisi tutumie maji na yule anayeona nongwa akashtaki. Akienda kushtaki sisi kama Taifa tutachangishana tutaandamana na kuonyesha kwamba msimamo wa suala hilo ni msimamo wa Taifa na sio msimamo wa mtu binafsi. Huwa nikizungumza sana napanda jazba ni bora niishie hapa naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, hata hivyo ulikwishapanda jazba. Lakini vizuri umesimama hapo kwa sababu jazba ikigeuka ikiwa mori ingekuwa taabu zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Pia napenda kumshukuru Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wangu wa Maji kwa jinsi anavyonielekeza katika majukumu yetu ya kazi tukishirikiana vizuri na hali kadhalika Katibu Mkuu Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Christopher Sayi, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji. Aidha, napenda kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja za Wabunge zipo nyingi, kuna ambazo tumezipata leo hii baada ya hotuba yetu ya Wizara ya Maji lakini pia kuna hoja mbalimbali ambazo zilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha na pia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu na pia wakati wa hotuba ya Wizara zingine hapa na pale walikuwa wakichangia kuhusu maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajitahidi jinsi ninavyoweza kwa hii nusu saa nianze na zile za leo na baada ya hapo nitajaribu nyingi niwezavyo zile zilizotolewa hoja za nyuma na kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambazo za kwao hatutazifikia ninawataka radhi lakini tutahakikisha kwa maandishi kila kitu tutawatayarishia na kuwagawia. *(Makofi)*

Hoja ya kwanza ilikuwa ni pongezi mbalimbali tulizopewa na Waheshimiwa Wabunge naomba kwa niaba Waziri wangu wa Maji nishukuru kwa pongezi hizo na niwataje waliotoa pongezi kwa Wizara hii akiwemo Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba na Mheshimiwa Yono Kevela. *(Makofi)*

Baada ya hapo napenda niongelee kwa kifupi kuhusu hoja ambazo zilitolewa ambazo zinahusu uchunguzi wa miradi ya maji vijijini. Katika hoja tatizo liliongelewa na Mheshimiwa Joel Bendera ambaye yeye alitaka kujua tatizo la maji katika mji wa Korogwe pamoja na mradi mkubwa ule ambao wa *Handeni Transmission Main.* Napenda kujibu kwamba kwa utaratibu wa programu, uibuaji wa miradi na uwekaji wa vipaumbele vya utekelezaji wa miradi hiyo hufanywa na Halmashauri ya Wilaya husika. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ili mji huo pamoja na vijiji vinavyozunguka viwekwe katika vipaumbele chini ya programu ya maji. Mheshimiwa Mathias Chikawe na yeye pia alizungumzia suala la kuhusu huduma ya maji ya mji ya Nachingwea na vijiji vyake. Suala hili Serikali bado itaendelea kulifanyia mazungumzo na *BADEA* na wafadhili wengine mbalimbali ili kupata fedha kwa ajili ya mradi huu tuwe na ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, yeye alizungumzia tatizo la Maji Moshi Vijijini kuanzia Mbokomu, Foyeni, Kiwalaa na Korini Kusini. Utekelezaji wa mradi wa maji katika vijiji vya Mbokomu, Foyeni, Kiwalaa, Korini Kusini na Rau utatekelezwa katika awamu ya mradi wa maji wa Moshi Vijijini unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani *(KfW)* na pia kupitia programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Hoja inayofuatia kutoka kwa Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, yeye alikuwa na maswali matatu, upimaji wa maji vijijini Wilayani Lushoto, pia alitaka kujua upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Lushoto ni asilimia ngapi na pia upatikanaji wa maji safi na salama mashuleni Lushoto. Halmashauri ya Wilaya ilifuatilia kwa undani suala hili kuona namna ya kutatua, aidha, namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwaelimisha wananchi ili washirikishe Wilaya kwenye masuala ya maji. Upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wilaya ya Lushoto kwa hivi sasa ni asilimia 59.6 ambayo ni kubwa kuliko wastani wa Taifa wa asilimia 55.7. Uibuaji wa miradi ya maji na upangaji wa vipaumbele upo mikononi mwa wananchi kupitia Halmashauri za Wilaya hivyo mpango wa kupeleka huduma ya maji mashuleni unapaswa kuwekwa na Halmashauri ya Wilaya kwenye mipango yao mingine ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, yeye pia aliulizia tatizo la huduma ya maji Mkoa wa Kigoma eneo la vijijini. Tunamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wa Mkoa Kigoma ili kuhakikisha mipango ya huduma ya maji vijijini inaboreshwa kwa vile kuingiza Bajeti zake katika Halmashauri ya Wilaya husika kwani huko ndiko ambako kwa hivi sasa fedha zote zinapelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, aliulizia vijiji vya Bitari, Kiganzo, Mwandiga havipati maji vizuri. Halmashauri ya Wilaya Kigoma Vijijini iweke mradi huo kwenye mipango yake na kuutengea fedha ambazo tunapeleka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, alizungumzia tatizo la maji katika Vijiji vya Mtakuja, Ngisala, Mabatakelo na Kuatiti. Tunamshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri kuhakikisha anaviingiza vijiji hivyo katika Programu ya Maji ya Wilaya yao.

Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mbunge wa Rombo, yeye aliulizia tatizo la maji Ukanda wa Tambarare, Wilayani Rombo na pia hoja ya kutafiti visima virefu. Tunamshauri Mheshimiwa Mbunge, aendelee kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ili hatimaye eneo hili liingizwe katika vipaumbele vya Miradi ya Maji katika Programu ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, aliulizia kuhusu Mradi wa Kibigili kwenda hadi Vijiji vya Kizonzo, Mseko na Mgongo. Pia na yeye namwomba hivyo hivyo, awashirikishe Halmashauri kuingiza hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika vifungu vinavyofuatia ni maswali yaliyoulizwa kuhusu ukarabati na upanuzi wa Miradi ya Maji Vijijini. Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, aliulizia kuhusu Mradi wa Maji wa Nyakagomba na Chamkorongo. Napenda

kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mradi wa Nyakagomba ni wa muda mrefu na ni Mradi mkubwa ambao unahitaji fedha nyingi. Tulishajadiliana naye na tukajadiliana pia na Halmashauri yake ya Wilaya, Mradi huu sasa hivi umepangiwa katika miradi kumi ya maji ambapo Mradi wa Chamkorongo sasa ndio utaingia katika miradi ile midogo midogo ya maji. Kwa hiyo, naomba awafahamishe wananchi wake kwamba wavute subira, Mradi wa Nyakagomba sasa umepatiwa ufafanuzi wake na utatuzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma H. Kilimbah, Mbunge wa Iramba, alitaka kujua uendeshaji wa Miradi ya Maji Vijijini na ushiriki wa watu binafsi katika kutoa huduma ya maji vijijini. Miradi ya Maji iliyojengwa miaka ya 1975, imeharibika kutokana na uhaba wa vyanzo.

Kwa mfano, chanzo cha Mradi wa Wembele, kinakauka kutokana na uharibifu wa mazingira ya maeneo hayo. Miradi yote inayojengwa hivi sasa, inakamilishwa na wananchi wenyewe. Wananchi hao ndio wanaopanga bei ya maji na kulinda miradi ili iwe endelevu.

Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mbunge wa Jimbo la Maswa, yeye alitaka kufahamu kuhusu ukarabati wa Bwawa la Nyusola na upatikanaji wa huduma ya Maji Mjini Maswa na pia katika Jimbo la Maswa kwa ujumla. Napenda kumfahamisha kwamba, kwa robo ya nne ya mwaka 2006/2007, Wilaya ya Maswa ilitumia shilingi 75,042,000 kwa ajili ya miradi midogo midogo katika Vijiji vya Bukangilija, Dulungwa, Isanga, Jija, Lulalago, Malampaka, Ipililo, Shinyangamwenye, Mwaburutu, Sengwa na Igulungobo.

Mheshimiwa Spka, kutokana na kupasuka kwa Bwawa la Zanzui, kiasi cha shilingi milioni 50 kilitumwa Maswa mnamo Mei, 2007 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji Mjini Maswa, kwa kutumia visima vya maji. Aidha, ili kuanza kujiandaa kukarabati Bwawa la Zanzui, kiasi cha shilingi milioni 150 tayari kimelipwa kwa *DDCA* kwa ajili ya kuandaa ukarabati huo. Pia kwa mwaka 2007/2008, Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa Bwawa hilo. Kiasi kingine cha shilingi 290,593,420 kimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu mingine, ikiwa ni pamoja na mtambo wa kusafisha maji kwa ajili ya Mji wa Maswa. Aidha, katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayoanza rasmi mwaka huu 2007/2008, vijiji vinane vya Lalalago, Njiapanda, Jihu, Mahegele, Jija, Masanwa, Masai na Nashanwa, vitahusika na kupewea huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William V. Lukuvi, alitaka kufahamu ujenzi wa Bwawa la Iguruba utaanza kutekelezwa lini. Mkandarasi tayari anakusanya vifaa, eneo la ujenzi tayari na ataanza kazi wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, alitoa ushauri kuhusu Sera ya Kujenga *Piped System,* ambayo ni mtandao wa mabomba unaounganisha vijiji badala ya kuchimba visima kwa kila kijiji. Napenda kumshukuru kwa ushauri wake aliotupa.

Katika kuamua aina ya teknolojia itakayotumika kwenye Miradi ya Maji, Sera ya Maji inawapa wananchi husika nguvu ya kuchagua.

Hata hivyo, jambo la msingi hapa ni gharama ambayo hulipwa na watumiaji huduma wenyewe. Kwa kawaida mtandao wa mabomba huwa na upotevu mkubwa wa maji ikilinganishwa na kisima kimoja kimoja. Hali hii huongeza gharama ambayo kwa wananchi waishio vijijini huwa ni mzigo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, ambaye yeye alikuwa anaulizia tatizo la maji Wilayani Masasi. Napenda kumfahamisha kwamba, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutafuta chanzo cha fedha zitakazotosheleza ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika mwaka huu wa fedha, Wizara imetenga kiasi cha shilingi milioni 346 ili kutekeleza miradi midogo midogo itakayochukua muda mfupi na kuwezesha huduma ya maji kuwa bora mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, aliulizia tatizo la maji kwenye Mji wa Misungwi. Mawasiliano kati ya Wizara na *MCC* bado yanandelea japo matumaini ni madogo. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 410 kwa ajili ya uimarishaji wa huduma ya maji kwenye Mji wa Misungwi.

Mheshimiwa Stephen M. Wasira, aliulizia tatizo la maji katika Mji wa Bunda. Napenda kumfahamisha kwamba, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Mji huo wa Bunda. Kwa mwaka 2007/2008, shilingi 636,445,000 zimetengwa ili kuboresha huduma ya maji ya mji huo.

Mheshimiwa Spika, sehemu inayofuata ni Programu ya Maendeleo ya Huduma ya Maji. Naomba niiache programu hii kwa kuwa Mheshimwa Waziri ataiongelea. Inayofuata sasa ni uendeshaji wa skimu kubwa za maji vijijini. Katika sehemu hii, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, aliulizia kuhusu Vijiji vya Imami, Kazamoyo, Nkambule, Lukelo na Makende, Wilayani Tunduru, visima vyake havijatengenezwa. Napenda kumfahamisha kuwa, vijiji vihamasishwe kuchangia fedha kwa ajili ya kutengeneza visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, anasema Serikali ihamasishe jamii kuhusu kujenga mabwawa na kuvuna maji ya mvua. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu kujenga mabwawa na kuvuna maji ya mvua. Tunamshukuru kwa ushauri wake huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yono S. Kevela, hoja yake inahusu uongozi wa miradi kuwa ni wa kisiasa na hivyo kuathiri huduma. Anapendekeza uongozi uliopo ubadilishwe. Sisi tunamjibu kwamba, Wizara imepokea ombi hilo na italifanyia kazi ili kuweza kuweka mabadiliko yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba sasa niingie katika masuala ambayo yalichangiwa na Waheshimiwa Wabunge siku zilizopita katika hoja mbalimbali za Wizara nyingine. Napenda kuanza na Waheshimiwa Wabunge, ambao walichangia hoja

zinazohusu uchunguzi wa maji. Wabunge hawa walizungumzia Mji wa Masasi, Vijiji vya Manyovu, Shunga - Wilayani Kasulu, maeneo ya Mangaka, Chitowe, Nangomba - Wilayani Nanyumbu na matumizi ya maji ya Mto Mungonya kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika Vijiji vya Kamala, Mahembe na Kalinzi katika Jimbo la Kigoma. Naomba niwajibu kama ifuatavyo: Wabunge hao ni Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa na Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa muda mrefu kutoa maji kutoka chemiu chemi za Mbwinji hadi Masasi, bado unaendelea na tunasubiri wafadhili ambao tumewaomba ambao ni *BADEA*. Lakini wakati huo huo naomba pia niongelee kuhusu uboreshaji wa huduma za maji katika Kijiji cha Shunga, Wilayani Kibondo kwamba, unaendelea kwa ufadhili wa *Red Cross* na kwa gharama ya shilingi milioni 178. Miradi ya Maji katika Vijiji vya Mubanga, Nyamkolonko na Kilungu vilivyoko Tarafa ya Manyovu, utatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Aidha, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kasulu, itachunguza Miradi ya Maji katika Tarafa zote zile ambazo zimeorodheshwa. Vijiji saba vya Sengenya, Chipuputa, Ndechela, Nandembo, Ulanga, Chivirikiti na Mangaka, Wilayani Nanyumbu, vitapata huduma ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Vijiji vya Chitowe na Nangimba, vinaendelea kuhamasishwa viunde Kamati za Maji. Aidha, chini ya Programu hiyo, Wizara itashirikiana na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu hoja ambayo ililetwa kwa maandishi na pia ilichangiwa siku za nyuma na Wabunge wawili; Mheshimiwa Juma A. Njwayo na Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika. Hoja yao inahusu Mradi wa Maji wa Makonde na Ruchemo. Kiasi cha shilingi milioni 300 kimetolewa na wakandarasi wawili wa kukarabati mradi wamelipwa malipo ya awali ya jumla ya shilingi milioni 268. Kiasi kilichobaki, kimetumwa Mamlaka ya Maji Makonde. Kiasi kingine cha shilingi milioni 700 kimetengwa kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu 2007/2008 katika programu. Serikali itaendelea kugharamia matengenezo na uendeshaji wa pamoja na kuanza kutafuta njia sahihi za kuwezesha mradi huo kujiendesha wenyewe na hivyo kufikia lengo la kitaifa la kuwapatia asilimia 65 wananchi waishio vijijini ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja inayohusu utekelezaji wa Miradi ya Maji katika maeneo ya Mwandiga na ukarabati wa Mabwawa ya Kisaki, Kondoa, Zanzui na Maswa ili kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Maore. Mradi huo kuzeeka na kuchakaa na matumizi ya Mto Ruvu kwenda Olkesumet, Wilaya ya Simanjiro. Mradi wa Maji wa Nyakagomba, Jimbo la Busanda na kuboresha huduma ya maji ya Wilaya ya Kondoa. Hoja hii ilichangiwa na wafuatao; Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa Paschal C. Degera. Napenda kuwajibu kama ifuatavyo:-

Wizara itawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Same ili iweke kipaumbele katika kuchunguza chanzo kinachofaa kutumika kutokana maji ya Bwawa la Kalimawe kutokuwa salama kwa matumizi ya binadamu. Pia, Wizara imetoa ushauri kwa

Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kuupa kipaumbele mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvu kwenda Mji wa Olkesumet.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Nyakagomba utakarabatiwa chini ya Programu ya Maji kama nilivyoieleza hapo awali. Shilingi milioni 30 zilizotengwa mwaka 2005/2006, shilingi milioni 100 zilizotengwa mwaka 2006/2007 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ntomoko, hazikutolewa kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha, mradi huo umepewa kipaumbele na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa mwaka huu 2007/2008. Kwa kuwa Mheshimiwa Paschal C. Degera, amechangia pia siku ya leo, napenda nijumuishe tena majibu ya nyongeza kuhusu Mradi wa Ntomoko. Ni kweli tunakiri kwamba, Serikali iliahidi shilingi milioni 100 na kama nilivyoongea katika jibu langu la asubuhi kwamba, shilingi milioni 100 zilishindikana kupelekwa kwa sababu ya hali mbalimbali zilizojitokeza, fedha hiyo ikashindwa kupatikana na mradi huo haukuweza kutengewa fedha tena.

Hata hivyo, tumezungumza na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, tumekubaliana kwamba, kwa sababu kwa hivi sasa, fedha zote zinapelekwa kwenye Halmashauri, kwa hiyo, wautengee fedha mradi huo mwaka huu ili uanze. Tulikubaliana kwamba, kwa mwaka huu watatenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya Mradi wa Ntomoko. Hata hivyo, napenda pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Wizara tunafahamu kwamba, wiki mbili zilizopita, mtaro wa Ntomoko kulitokea tena mmommonyoko na baadhi ya mabomba yalichukuliwa. Kwa hali hiyo, kwa hivi sasa maji katika vijiji hata vile sita hayapatikani kabisa. Kwa hiyo, napenda nisisitize na kuwaomba Halmashauri kwamba, waupe kipaumbele Mradi wa Ntomoko. Fedha zitakapofika tu, waanzie kwanza kutengea Mradi huu ili uanze kwanza kushughulikiwa mradi huu kabla ya miradi mingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuna waliochangia kuhusu huduma za maji safi na uondoaji wa maji taka mijini na waliochangia katika hoja hizi ni Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti. Naomba nisome hoja yao ilikuwa ni kuhusu kuboresha huduma ya maji taka Kinondoni Shamba na Dodoma Mjini na huduma ya Maji Safi Ilala, uharibifu wa barabara na usambazaji wa maji kwa vijiji vilivyo umbali wa kilomita tano kutoka bomba kuu katika Mradi wa Maji wa Kahama na Shinyanga. Naomba nitoe majibu kama ifuatavyo: Mhandisi Mshauri anakamilisha utayarishaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dar es Salaam na atahusisha Kinondoni Shamba. Mradi wa Kuboresha Miundombinu unaotekelezwa na *DAWASA,* unahusisha kuunganisha huduma ya maji katika nyumba za wateja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, miji yote ambayo haina mifumo ya maji taka, itafanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu na kutayarisha makabrasha ya zabuni. Mradi huu utatekelezwa kwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira. Aidha, kupitia *EU Water Facility, Euro* milioni 2.67, zitatumika kuchunguza maji safi na maji taka katika miji saba ikiwemo Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Babati, Kigoma, Musoma na Bukoba. Vilevile mwaka 2008/2009, *Euro* milioni 58 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Upanuzi wa miundombinu ya maji taka Mjini Dodoma,

utatekelezwa chini ya Mradi unaogharamiwa na Serikali, pamoja na Serikali ya Uswisi kupitia *SECO*. Wizara itapitia tena Mradi wa Maji Kahama – Shinyanga, kuona uwezekano wa kutekeleza awamu ya pili ya mradi itakayojumuisha vijiji vilivyo umbali wa kilomita tano kutoka bomba kuu. Maeneo ambayo hayamo katika mpango wa sasa lakini yako umbali usiozidi kilomita tano, Mkandarasi ameagizwa aweke matoleo *(off takes),* kwa ajili ya kupata maji. Mkandarasi anatakiwa kukarabati barabara na mifereji husika kwa shilingi milioni 46.1. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ina jukumu la kukarabati barabara husika.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Wabunge waliochangia kuhusu tatizo la maji safi na maji taka Dar es Salaam. Wabunge hao ni Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimia Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Juma Said Omar na Mheshimiwa Anna M. Komu. Walitaka upatikanaji wa maji wa Kigamboni, Jimbo la Ilala, Kiluvya, Makoka na Mwongozo Makaburini. Napenda kuwajibu kwamba, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji Safi na Maji Taka, utakamilika 2008/2009. Maeneo ya Ilala, Kigamboni, Mlandizi hadi Kimara na Kiluvya, yote yatahusika.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie haya machache kwamba, kuna Wabunge ambao walipenda kufahamu kuhusu uendelezaji wa vyanzo vya visima virefu vya Kimbiji na ujenzi wa Bwawa katika Mto Ruvu. Wabunge hao ni Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha na Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya. Napenda kuwafahamisha kwamba, kazi ya uchunguzi wa Kimbiji inaendelea, mpango wa kuviendeleza utaanza katika mwaka huu wa fedha 2007/2009. Uchunguzi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda, umeenza na utakamilika Desemba 2007. Kazi ya ujenzi itaanza mara fedha zitakapopatikana. Mipango inaandaliwa ili Mheshimiwa Waziri, aweze kuzungumza na wananchi wa Kidunda kuhusu suala la Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie la mwisho kuhusu tatizo la kuzagaa maji taka Jijini Dar es Salaam, ambalo ameuliza Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, pamoja na Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya. Katika Mradi wa *WSPP,* mtandao wa mabomba makubwa umekwishalazwa, ikiwa ni pamoja na Kariakoo na utadhibiti kuzagaa zagaa maji taka. Mtandao huu ukishakamilika, utakuwa umekidhi sehemu kubwa ya maji taka ya jiji lote la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Waheshimiwa Wabunge, kuna ambao sikuweza kuwataja, tunaomba radhi, lakini ninaahidi tutawapa majibu kwa maandishi. Napenda nishukuru na ninaunga tena mkono hoja hii mia kwa mia. Asante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, asante sana. Kabla sijamwita mtoa hoja, ninapenda tu kuonesha mshangao wangu kwamba, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Sekta hii, hayumo Bungeni wakati wote huu wakati majibu yanaendelea!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa dhati, wewe mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa busara na hekima zenu, zinazowezesha kuongoza na kusimamia kwa utulivu Shughuli za Bunge.

Napenda kutoa pongezi na shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, walichangia hoja yangu, ambao naamini michango yao ina nia njema kabisa ya kuboresha huduma za maji nchini. Jumla ya Wabunge 33 walichangia kupitia Hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na kupitia hotuba ya Waziri Mkuu. Aidha, Waheshimiwa Wabunge 75, wamechangia hotuba ya Waziri wa Maji kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge kumi wamechangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotualika mimi na Naibu wangu, kutembelea majimbo yao ili kuona mafanikio na matatizo katika utekelezaji wa Miradi ya Maji. Napenda kuchukua nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutajitahidi kadri itakavyowezekana kutembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu Wizara yangu, kwanza, kama ilivyo ada, napenda kuwatambua waliochangia wote kama ifuatavyo: Waliochangia kupitia Hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni kama wafuatao; Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi na Mheshimiwa Paul P. Kimiti.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kupitia Hotuba ya Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Mudhihiri M. Mudhihiri, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda na Mheshimiwa Mussa A. Zungu.

Mheshimiwa Spika, waliochangia Hotuba ya Waziri wa Maji kwa maandishi ni Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimia Joel N. Bendera, Mheshimiwa Mathius M. Chikawe, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa

Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Omary S. Kwaangw' na Mheshimiwa Diana Chilolo,

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Dr. Wilabrod P. Slaa, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Annia S. Chaurembo, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha na Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ningependa nitoe maelezo ya jumla katika baadhi ya maeneo. Eneo la kwanza ambalo ningependa kulitolea maelezo ya jumla ni mgawanyo wa majukumu katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2007/2008, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itaanza kutekelezwa rasmi. Programu hiyo inakwenda sambamba na utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa Sekta ya Maji. Programu hiyo inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na wahisani. Hadi mwaka 2010, programu hiyo imekisiwa kuhitaji jumla ya Dola za Marekani milioni 951, ambapo Serikali itatoa Dola za Marekani milioni 251 na wahisani kwa pamoja watatoa Dola za

Marekani milioni 700. Kwa misingi hiyo, Serikali itaongeza fedha za ndani za uwekezaji katika Sekta ya Maji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maji Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi *(Decentralization by Devolution),* mara nyingi inajulikana kama *D by D*. Sera ya Maji inasisitiza usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kufanyika katika ngazi za chini kadri inavyowezekana. Programu itatekelezwa katika ngazi za Halmashauri, Ofisi za Maji za Mabonde na Mamlaka za Maji Mijini. Serikali Kuu, itatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Hilo ni jukumu kubwa ambalo Serikali Kuu inalichukua katika utekelezaji wa programu hiyo. Pia Serikali Kuu, itatoa ushauri wa kitaalam, itazijengea uwezo Halmashauri zote nchi nzima na itazijengea uwezo Mamlaka za Maji Mijini na Ofisi za Maji za Mabonde na itaratibu utekelezaji wa programu hiyo katika ngazi zote. Kwa hiyo, tuelewe fika kwamba, wakati tunakwenda katika utekelezaji rasmi wa programu hii mpya ya maendeleo ya sekta, utekelezaji utafanyika katika ngazi hizo na kwamba, Halmashauri zina jukumu kubwa pamoja na mamlaka hizi ambazo nimetamka. Serikali Kuu, haijitoi katika jukumu la kuhakikisha kwamba, huduma ya maji safi na salama inawafikia wananchi. Serikali inachukua jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba, inatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufafanuzi tena katika eneo la huduma ya maji vijijini. Utekelezaji wa miradi ya maji vijijini chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, utafanyika katika ngazi za Halmashauri. Halmashauri zitawajibika kujipangia Miradi ya Maji kulingana na mipango na vipaumbele vitakavyojiwekea katika maeneo yao. Halmashauri zitakuwa na jukumu la kuwahamasisha wananchi, kuibua miradi ya maji na kuchangia gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ya maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kwa yale ambayo ametueleza katika Bunge hili Tukufu kazi, wameyafanya kule Karatu basi msimamo ndiyo huo huo wa kisera. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wenzetu wao ndio viongozi wa wananchi katika kuibua miradi ya vipaumbele na kuipitisha kwenye Halmashauri zao. Si tu kusema kwamba, wananchi wameibua miradi, Wananchi wetu tunawafahamu katika maeneo yote ya Tanzania; kuna ambao wana uwezo mkubwa na kuna ambao hawana uwezo mkubwa. Kwa hiyo, sisi kama wawakilishi wa wananchi hawa, tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba tunasaidiana nao kuhakikisha kwamba tunaibua hii Miradi ya Maji kwa kadri vipaumbele ambavyo tunaviweka katika Halmashauri zetu.

Pia Halmashauri zitasanifu Miradi ya Maji na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo katika ngazi za vijiji. Serikali Kuu, itabakia na jukumu la kutafuta fedha tu za uwekezaji. Kutoa miongozo ya utekelezaji kisera na kiufundi, kufuatilia utekelezaji na kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kuzipatia wataalam, vifaa na nyenzo. Serikali imesikia, Serikali ya Awamu ya Nne ni sikivu, vilio vile ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa Bungeni, kuhakikisha kwamba Halmashauri na mamlaka za maji zinapatiwa nyenzo za kutosha za vifaa, hili jambo litatekelezwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa programu hii ya maendeleo ya sekta ya maji.

Napenda nitoe ufafanuzi katika eneo la usimamizi wa rasilimali za maji. Maji ni rasilimali nyeti, inayopungua kutokana na ongezeko la watu, uchafuzi wa vyanzo vya maji, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Ili kuwa na rasilimali endelevu, mfumo shirikishi wa kutumia maji katika mabonde unatumika kama ilivyoainishwa kwenye sera ya maji. Wizara yangu itaziimarisha ofisi za mabonde na vyombo vya watumiaji maji, kwa kuzipatia nyenzo na watalaam. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi katika utunzaji wa rasilimali za maji na mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa ufafanuzi katika eneo kuu la Mradi wa Maji Dar es Salaam. Mheshimiwa Naibu Waziri, ameuzungumzia kwa kiasi fulani lakini naomba nitoe maelezo ya ziada ya ujumla katika eneo hilo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Rasilimali ya Ulaya, inatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu na maji safi na maji taka ya Dar es Salaam. Mradi huu ulibuniwa mwaka 1997 na kuanza kutekelezwa rasmi mwaka 2004. Tuko katika utekelezaji wa kazi mbalimbali katika mradi huo. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kuchunguza vyanzo vya maji na kutayarisha mipango ya upanuzi wa huduma ya maji safi na maji taka, kukarabati mitambo ya kusafisha maji Ruvu Chini na katika mtambo wa Ruvu Juu na pia katika mtambo wa Mtoni.

Kazi nyingine ambayo inafanywa ni kulaza mabomba makuu ya kusafirisha maji kutoka katika mitambo hadi Jijini Dar es Salaam na pia kulaza mabomba ya usambazaji maji. Kazi hii ni kazi kubwa, imeanza muda mrefu tangu mwaka 2004 na bado inaendelea. Sasa hivi ukarabati wa mitambo umefikia asilimia 75, umefikia kwa kiwango kikubwa, mitambo iko katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 2004 wakati tumeanza kazi hiyo.

Katika chanzo cha maji Ruvu Chini, pampu za uvutaji maji nne zote zimeshafungwa, mpya kabisa, hakuna tatizo la kusukuma maji, labda itokee tatizo la ukatikaji wa umeme, lakini kwa kuwa umeme upo, hakuna tatizo la kusukuma maji. Kazi ya ulazaji wa mabomba makuu imekamilika kwa asilimia 100. Mabomba yale makuu yanayotoa maji kutoka kwenye mitambo kupeleka katika tanki kuu ambalo liko *Wazo Hill,* lenye ukubwa wa mita za ujazo 35,000 na mabomba makubwa na madogo ya usambazaji, kazi hiyo imefikia asilimia 60 mpaka hivi sasa. Pia ujenzi wa mifumo ya maji taka kwa Jiji la Dar es Salaam, umefikia asilimia 85. Mradi huu kama nilivyosema awali ni mkubwa kwa hiyo, haukosi matatizo katika utekelezaji wake. Tume-*experience* matatizo ya hapa na pale, kama ufungaji mitambo wakati wa ujenzi na hiyo ilisababisha ukosefu wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Nakumbuka hivi karibuni tu wakati bomba lilipasuka katika maeneo ya Mpiji, lilipasuka wakati wa harakati za matengenezo na kusababisha Mji wa Dar es Salaam kukosa maji. Lakini tunasema kwamba, kasi tunayokwenda nayo sasa hivi ni nzuri na mambo yakienda vizuri, tunategemea mradi huu utakamilika ifikapo mwisho wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pia ufafanuzi wa miradi ambayo imeombewa fedha katika Shirika la *Millenium Challenge* la Marekani. Serikali, imekuwa katika majadiliano na *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ili igharamie ujenzi wa Bwana

la Kidunda, upanuzi wa mtambo wa kusukuma maji Ruvu Chini na ujenzi wa miradi ya maji katika Miji ya Bunda, Geita, Tarime, Misungwi, Bukoba na Bariadi. Baada ya *MCC* kutathmini miradi hiyo, imeendelea kuwa na mawasiliano na Serikali kuhusu tathmini zao. Serikali bado inaendelea katika mchakato wa majadiliano na Shirika la *MCC* katika kuhakikisha kwamba, tunamudu kupata fedha kutoka Shirika hili kwa ajili ya miradi yetu hii mikubwa, ambayo nimeitaja ya maji. Mengi yametokea katika taratibu hizi za majadiliano kati ya Serikali na *MCC* na hasa kwa upande wa Sekta ya Maji.

Tunatarajia kwamba, ifikapo Septemba, 2007, basi Bodi ya *MCC* itafanya maamuzi rasmi ya miradi gani ambayo imekubaliwa kufadhiliwa na *MCC*. Lakini katika mchakato wa majadiliano na *MCC,* kuna vipengele vingine ambavyo vimejitokeza, *MCC* imeonesha dalili ya kupenda baadhi ya miradi ambayo hata hatukuiwasilisha katika wasilisho letu la *MCC*. Hivyo ikapendekezwa kwamba, *MCC* nayo iingize katika tathmini ili Bodi itakapofanya maamuzi Septemba, kama kutakuwa na uwezekano basi miradi hii nayo iwemo katika miradi ambayo itafadhiliwa na *MCC*. Miradi hiyo ni pamoja na maji katika Mji wa Morogoro, maji kwa Jiji la Dar es Salaam, kupitia visima virefu ambayo haikuwemo katika miradi ya mwanzo. Pia, kuna miradi midogo midogo michache ambayo nayo imo katika *MCC* imeangalia ikaona katika vigezo vyake, pamoja kwamba hatukuiwakilisha, ingependa kuichukua na kuitathmini na kuhakikisha kwamba, ikikidhi vigezo basi tutapatiwa fedha chini ya programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa basi kuomba fedha ni jambo moja, kupata ni jambo jingine. Tunapoomba pamoja na juhudi kubwa ambazo Wizara ya Maji inafanya kwa niaba ya Serikali, mawili bado yako mawazoni mwa Serikali kufanikiwa na kutokufanikiwa. Sasa muda wote Serikali katika azma yake ya kuhakikisha kwamba inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inafanya maandalizi kamili. Pamoja na kusubiri maamuzi ya *MCC* lakini kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, baadhi ya miradi ambayo tumewasilisha *MCC* ikiwemo miradi ya maji ya miji inayozunguka Ziwa Victoria, ikiwemo miradi ya maji Mjini Bukoba, Misungwi, Bunda, Bariadi Tarime na Geita, imetengewa fedha kwa ajili ya maandalizi chini ya Programu ya Sekta ya Maji. Kwa hiyo, kutakuwa na shughuli kadhaa ambazo zitafanywa tukitegemea kwamba katika mchakato wa *MCC,* Mungu akijalia tukiwa tumefanikiwa, maana yake kazi za mwanzo zitakuwa zimeshaanza na kwa namna hiyo tunategemea pia kwamba, *MCC* itakuwa imehamasika kwa kutuona kwamba sisi tumeanza kutekeleza miradi hii na kwa maana hiyo, wao wahamasike kuweza kutupa *support* ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limezungumzwa kwa jazba kubwa au kwa simanzi na limefuatiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengine baada ya Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu kulizungumzia. Suala hili linahusu matumizi ya maji kutoka Ziwa Victoria. Sasa niseme basi ile mikataba ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitaja au kusema kwamba nchi ilipopata Uhuru ilikana mikataba yote ya zamani, ambayo Serikali Huru ya Tanzania haikushirikishwa, ikiwemo mikataba yote ya Mt Nile yote ya mwaka 1929 na ule mkataba baina ya nchi mbili za Misri na Sudan wa mwaka 1959. Mwaka 2004 Serikali ilitoa tamko rasmi hapa Bungeni, kusisitiza msimamo huu na kwamba, tuko tayari kujadili mfumo wa ushirikiano wa nchi za Bonde la Mto Nile. Baada ya kukaa na mikataba hii mara tu nchi yetu ilipopata Uhuru mwaka 1961 na kuikana mikataba hiyo

ndani ya Umoja wa Mataifa, tulibaki tukiwa hatuna mikataba yoyote na nchi yoyote kuhusu matumizi ya maji ya Ziwa Victoria au maji ya Mto Nile. *(Makofi)*

Hali hii haikidhi mahitaji muhimu ya uendelezaji na utunzaji wa rasilimali za maji zilizopo katika Bonde la Mto Nile, kama hatuna ushirikiano na nchi nyingine ambazo zinahusiana na bonde la mto huu. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 1997 taratibu za awali zimeanza kufanyika kati ya nchi ambazo zinashirikishwa katika Bonde la Mto Nile. Ziko nchi kumi ikiwemo Tanzania, Kenya, Uganda, Ruanda, Burundi, *DRC*, Ethiopia, Sudan, Elitrea na Egypt.

Mwaka 1997 taratibu zimeanza kwa maongezi, kwa sababu haileti mantiki kwamba, nchi ya Egypt kwa mfano, igombane na Tanzania kuhusu maji ya Mto Nile wakati haishiriki katika kutunza hali nzuri ya mazingira katika Ziwa Victoria au vyanzo vya Mto Nile, kwa mfano, sisi tukishindwa kwa gharama kubwa ya utekelezaji wa miradi ambayo inatakiwa maana yake wao watakuwa wanapata maji machafu na haitaweza kuwasaidia katika maendeleo ya nchi yao. Kwa hiyo, 1997 mpaka sasa 2007 hususan miaka kumi tumekuwa katika majadiliano na nchi hizo kumi, ushirikiano wa matumizi ya maji ya Mto Nile. Majadiliano haya yanamaanisha kwamba, tunataka nchi hizi zote ambazo zimo katika bonde zihakikishiwe usalama wa matumizi ya maji ya Mto Nile kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba, kwa nini Tanzania isitumie maji yale? Lakini tutumie maji yale kwa uwiano na kwa usawa ili tusifikie mahali ambapo nchi itaishikia silaha nchi nyingine kwa ajili ya maji haya. Hilo linawezekana na hilo tulikuwa tunahangaika nalo kwa muda mrefu na siyo suala dogo la kuweza kusema kwamba tungeweza kulimaliza kwa siku moja, mbili au kwa mwaka mmoja.

Majadiliano kwa kipindi chote hicho yamekamilika katika kikao cha 15 cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Nile. Kikao cha 15 cha Baraza la Mawaziri wa nchi za Mto Bonde ambacho kimefanyika mwezi Juni, mwaka huu 2007, Mjini Entebe zimefikia mwisho wa makubaliano ya mfumo wa ushirikiano wa matumizi ya maji ya Mto Nile. Pamoja na makubaliano hayo ya Mawaziri, kipo kifungu kimoja kinachohusu usalama wa maji *(water security),* ambacho bado kinatafutiwa muafaka wa ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, makubaliana ya mfumo wa ushirikiano, mkataba ule una vipengele 39 kikiwemo kipengele cha usalama wa maji. Tumejadili vipengele hivyo kimoja baada ya kingine; vipengele vizito kikiwemo kipengele hiki na kipengele kingine ambacho kizito pia ni kile cha upashanaji habari. Nchi nyingi zingependa kuendelea na miradi yao tu bila kuambiwa nchi nyingine. Lakini kwa kufanya hivyo, kunaweza kukaleta madhara kwa nchi nyingine, lakini siyo suala rahisi kwa kila nchi kukubaliana na jambo hilo. Kwa hiyo, vipengele 38 na 39 vimefikiwa muafak. Kipengele cha 39 nacho kimefikiwa muafaka kasoro sehemu ndogo tu ambayo hiyo inataka ipatiwe uamuzi katika ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazofuata, kifungu hicho kilichobakia kitawasilishwa kwa wakuu wa nchi, kwa maamuzi ya mwisho. Ushirikiano uliopo sambamba na majadiliano, nchi zote zimekuwa zinatekeleza miradi ya pamoja kama vile mafunzo,

kujenga uwezo, miradi ya umeme, miradi ya mazingira, miradi ya kilimo na miradi rasilimali za maji. Hii miradi ambayo tulikuwa tunaitekeleza kwa kipindi chote hicho, imetuwezesha kujijengea imani na kuondosha hali ya kutoaminiana katika nchi hizi za mabonde. Sasa hivi tulipofikia hapa niseme kwamba, Tanzania haijawahi kunyimwa kutumia maji ya Ziwa Victoria au Mto Nile na Taifa lolote. Ndiyo maana Serikali yetu iliamua kuanza kutekeleza mradi wa maji kwenda Shinyanga na Kahama. Kwa hiyo, itakuwa vigumu sana kufungua shauri lolote dhidi ya Serikali ya Uingereza na hatuna haja ya kufanya hivyo. Serikali kumi kwa ushirikiano na kwa ridhaa zetu wenyewe, tumefanya majadiliano marefu sana. Miaka kumi siyo safari ndogo. Najua kwamba, mijadala kama hiyo katika nchi nyingine imechukua miaka 40 na zaidi, lakini kwa bahati sisi tumeweza kutimiza kazi hiyo ngumu kwa kipindi kifupi cha miaka kumi, tutarajie kwamba, sasa tutakuwa na makubaliano ya ushirikiano katika nchi hizi na hatutakuwa na hofu yoyote ya kutumia, tutaendelea kutumia maji hayo tukiwa na uhakika kwamba tuna ushirikiano wa pamoja na nchi zote majirani katika bonde hilo.

Naomba sasa nitoe maelezo ya jumla kuhusu suala lingine kubwa ambalo Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa alilizungumzia kwa kina. Suala hili ni kuhusu *City Water* na *Bi-Water* au masuala mawili ambayo yamewasilishwa kama malalamiko. Kuna mashauri kwenye vyombo viwili vya usuluhishi wa Kimataifa; la kwanza ni *City Water* dhidi ya *DAWASA.* Shauri hili na madai ya Serikali kupitia *DAWASA* kwa *City Water* yanafikia dola za Kimarekani milioni tano. Shauri la pili ni lile la *Bi-Water Gulf* dhidi ya Serikali, shauri hilo linakadiriwa jumla ya dola milioni 20 mpaka dola milioni 25 wakiidai Serikali. Hadi sasa katika mashauri haya takriban shilingi bilioni 5.35 zimetumika katika kesi hizi mbili na tunadaiwa shilingi bilioni 6.3. Madai haya ni kwa ajili ya gharama za uwakili *(legal fees)*, kwa *Mkono and Company, Fresh Fees* na Denton, Mawakili ambao wanashughulikia shauri hili. *(Makofi)*

Madai hayo pia ni kwa ajili ya *expert fees,* kwa ajili ya mashahidi, watalaam na masuala ya fedha ya uendeshaji wa makampuni ya maji. Tatu, ni gharama za usafiri na nyingine katika mafungu haya mawili. Tunatarajia kwamba, kesi hizi zitaigharimu Serikali jumla ya takriban shilingi bilioni 11, kwani sehemu kubwa ya kazi za mawakili zimeshamalizika sasa na inatarajiwa kuwa hukumu na maamuzi yatatolewa kabla ya mwisho wa mwaka huu 2007.

Mheshimiwa Spika, gharama za mawakili ni *Euro 380* ama *US dollar* 500 kwa saa kama gharama za kisheria ama *(legal fees),* pamoja na gharama zote za usafiri na hoteli. Gharama hizi ni za kawaida kwa mawakili kwa mawakili wa kimataifa wa usuluhishi. Tunaweza tukaziona ni gharama kubwa lakini ni gharama za kawaida na mkataba wetu na *Mkono and Company,* ambaye naye ana mikataba kama hiyo na mawakili wengine wa nje, uliridhiwa na Mwanasheria Mkuu. Hapa hapakuwa na ujanja wa Serikali kuweza kukwepa malipo haya na tusingeweza kukwepa malipo haya ya mawakili, kwa sababu kwanza, tumeburuzwa katika kesi, sasa hatuwezi tukasema kwamba hatuendi kwenye kesi hiyo.

Kwa hiyo, kusema kwamba tunakwenda kwenye kesi hatuwezi pia kusema tusilipe fedha kwa ajili ya gharama za mawakili. Kuna mwenzangu mmoja ni mtaalamu

katika taaluma ya sheria, akasema bwana sisi wanasheria tuone tu hivi ni mahodari sana wa kazi na tukiamulia kazi kuifanya, tunaifanya kwa uhakika. Mimi nina imani Mheshimiwa Nimrod Mkono, ataifanya hii kazi kwa uhakika na kampuni yake kama alivyoniambia huyu bwana. Anasema kwamba, tunaifanya kwa uhakika lakini kuna tatizo moja kubwa, sisi bila hela akili huwa haifanyi kazi. Tukiacha kuwalipa maana yake uandaaji wa masuala haya, utetezi wa hoja hizi utakuwa mgumu kwa maana hiyo ni kwamba, masuala hayataweza kufanyiwa kazi. Mheshimiwa Nimrod Mkono, amekuwa akishiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ambalo limetolewa hoja, ushiriki wa yeye mwenyewe Mheshimiwa Nimrod Mkono. Naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Nimrod Mkono, amekuwa akishiriki kikamilifu katika kazi za Mawakili, amekuwa akihudhuria kesi hizo mwenyewe mwanzo hadi mwisho, pamoja na mwanasheria wake na tumekuwa tukikutana naye mara kwa mara ofisini kwetu na ofisini kwake na kujadili maendeleo ya kesi hizi, ameweza kuwashawishi pia. Katika hili naomba niseme kwamba, hivi karibuni mwezi wa nne wakati limezungumziwa shauri hili mara ya mwisho Netherlands, Mheshimiwa Nimrod Mkono mwenyewe alikuwepo tangu mwanzo wa shauri mpaka mwisho. Baada ya hapo ameendelea kukusanya ushahidi na kutengeneza makabrasha ya kufaa.

Pia Mheshimiwa Nimrod Mkono ameweza kuwashawishi mawakili wa nje kutuvumilia katika kuendelea na kazi licha ya kwamba, wanatudai zaidi ya shilingi bilioni tano, kati ya zote zilizotumika kwa kazi zote ambazo zimefanywa hadi hivi sasa. Serikali imekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa fedha, tumeona katika bajeti hii. Kwa nchi yetu hii tunahitaji fedha nyingi zaidi kuliko vile ambavyo Bunge Tukufu tunaliomba liidhinishe. Katika shida hiyo ya upatikanaji wa fedha, hatukuweza kulipa madai ya *Mkono and Company* kadri walivyokuwa wakihitaji. Lakini kwa juhudi zake ameweza kuwashawishi hata wale wawakilishi wa nje, kuweza kuendelea kufanyakazi pamoja na kwamba wanatudai. Najua kwamba, haya ni makampuni makubwa, lakini ni makampuni ya gharama. Kwa sababu ni makampuni ya gharama, nashukuru kwamba wanamudu kuweza kufanyakazi pamoja na kwamba, bado wana madai yao kwa wateja kama sisi.

Namshukuru sana Mheshimiwa Nimrod Mkono, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na naomba niwahakikishie Wabunge kwamba, wanafanyakazi nzuri, kazi kubwa na mimi kama Waziri wa Maji, nina imani kubwa, siwezi kuitolea kauli ya moja kwa moja. Lakini nasema nina imani kubwa kwa usimamizi wa *Mkono and Company.* Kwa kadri tulivyokuwa tunafuatilia mashauri haya mawili, nina imani kubwa kwamba katika mashauri hayo mawili, nchi yetu ya Tanzania itashinda katika mashauri haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi ni kuhusu Bwawa la Kidunda na fidia kwa wananchi wa Morogoro Kusini, kwa ujenzi wa bwana hili. Ulipaji wa fidia kwa ajili ya vijiji vitakavyoathirika kutokana na ujenzi wa Bwawa la Kidunda utafanywa baada ya kumaliza kufanya uchunguzi wa athari za

kimazingira *(Environmental Impact Assessment)* na kutambua wale watakaohusika. Pia uthamini uwe umeshafanyika ili kujua stahili ya malipo kwa kila anayehusika. Kazi hii inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu 2007.

Nadhani nimezungumza kabla kwamba, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni moja ya miradi ambayo tumeiombea fedha chini ya *Millennium Challenge Cooperation.* Uamuzi haujatolewa, nimesema tuna mategemeo kwamba, *MCC* itatupa hela lakini hatuna uhakika kama itatupa hela. Kwa hiyo, kwa maana hiyo mpaka sasa suala la fidia bado halijafikiwa kwa vile hata fungu la fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda bado halijaidhinishwa. *MCC* ikisema kwamba fedha hazipo; maana yake fidia nayo itakuwa haipo. Lakini kitu gani kinafanywa sasa hivi na Serikali, katika maandalizi kupitia *DAWASA* na mkandarasi, *No Consult* inafanya uchunguzi wa athari za kimazingira. Mwanzoni Serikali ilikuwa inatarajia kuwa na bwawa kubwa sana.

Katika uchunguzi huu wa athari tuna dalili za kupunguza ukubwa wa bwawa hilo, ili ziendane na taratibu nzuri za utunzaji wa mazingira. Stadi inaendelea, *No Consult* watamaliza tathmini hiyo ndani ya mwezi huu wa Julai, 2007 na watawasilisha tathmini yao, tutaijadili. Katika kujadili tathmini ile ndipo hapo tutaweza kuelewa ni vijiji gani ambavyo vitaathirika na fidia kiasi gani ambayo itahitajika. Lakini katika hatua hizi niseme tu kwamba, mimi naweka ahadi kwamba katika harakati hizi nitafanya ziara katika maeneo husika ili kuweza kuongea na wananchi, kuwafafanulia hatua ambazo tumefikia na kuwafafanulia nini kitafanyika baada ya hapo iwapo tutapata fedha kutoka *MCC,* basi fidia itafanywa kwa vijiji vile ambavyo vimetambuliwa kuathirika na bwawa hili na tutaifanya hiyo fidia bila ya upendeleo na bila ya mapunjo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa ridha yako, nitoe ufafanuzi katika baadhi ya hoja ambazo zimezungumziwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Katika Programu ya Sekta ya Maji kuna hoja maalum ambazo zimetolewa hasa na Mheshimiwa Mgana I. Msindai.

Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Pascal C. Degera na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti. *(Makofi)*

Hoja zenyewe zilihusu shilingi bilioni 19.2 na kwamba kule Same Mashariki, Serikali iliahidi kutoa shilingi milioni 20 mwaka 2006/2007. Aliyekuwa Waziri wa Maji aliahidi nyongeza ya shilingi milioni kumi ambazo mpaka sasa pesa hizo zilikuwa hazijatolewa na kwamba kuboresha huduma za maji katika Wilaya ya Sikonge ili kufikia asilimia 65 mwaka 2010; kuna Vijiji vya Chikonji na Liwawa, vipatiwe fedha haraka.

Niseme kwamba, maeneo makubwa yalikuwa ni haya, Kwikwins vipi na hasa baadhi ya fedha za *quick wins* ambazo zimetolewa hivi sasa, Halmashauri nyingine hazikupata fedha hizo. Naomba niseme kwamba, fedha shilingi bilioni 18.89 za *quick wins* zilitumwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa yote nchini Juni, 2007.

Shilingi milioni 353 zilitumwa kwenye Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri 84 zilipata fedha za maendeleo, pamoja na za kujijengea uwezo ambapo Halmashauri 37 hazikupata fedha za maendeleo kutokana na kutotimiza vigezo vilivyopo kwenye mfumo wa kuzipatia Serikali za Mitaa ruzuku ya maendeleo.

Shilingi milioni kumi zilizoahidiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Same, hazikutolewa kutokana na ufinyu wa bajeti. Halmashauri ya Wilaya imeshauri kutoa kipaumbele kwa Mradi huo wakati wa kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Maji na kutengea fedha zinazohitajika. Aidha, fedha za vijiji kumi zitatolewa mwaka huu chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa mwaka 2007/2008, fedha za kutekeleza Programu ya Sekta ya Maji zimekasimiwa kwenye Halmashauri za Wilaya ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Chikonji na Liwawa.

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umetekelezwa katika vijiji 14 ambapo vijiji saba ni vya Mtera, Chipogoro, Chaludewa, Ikuyu, Chamtumile, Igoji, Pwaga na Siluka, vipo Wilayani Mpwapwa katika Jimbo la Kibakwe. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, inashauriwa kuingiza kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili kukamilisha ujenzi wa Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba, kuna masuala kadhaa ambayo ingetakiwa niyajibu moja baada ya jingine, lakini kwa sababu ya uwingi wake, niseme tu kwamba, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimetolewa hapa Bungeni, Wizara yangu itazijibu kwa maandishi, hoja kwa hoja kwa Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kabla ya kumalizia, Mheshimiwa Charles Kajege, amezungumzia kuhusu Mkoa wa Mara kukosa hela za *Rural Water and Sanitation.* Mafungu yale ambayo ameyaona katika Kitabu cha nne kwamba, mikoa yote imepata hela kasoro Mkoa wa Mara. Niseme kwamba, katika Kitabu cha Nne si Mkoa wa Mara tu ambao haukuoneshwa kupata hela, Mkoa wa Mara na Mkoa wa Kilimanjaro imeoneshwa kwamba haikupata hela. Lakini naomba niwahakikishie kwamba, hayo yalikuwa makosa ya uchapishaji na tunawasiliana na Wizara ya Fedha. Mikoa yote ya Tanzania imetengewa fedha za miradi ya maji katika Kasma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji. Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na kuungwa mkono, lakini kama Kanuni zinavyohitaji tutaiamua baada ya hatua inayofuata. Katibu kwa hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kif. 1001 – *Administration and General* ............. Sh. 2,036,380,700.00

**MWENYEKITI:** Nitaanzia huku Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Paschal C. Degera na Mheshimiwa George M. Lubeleje. Hebu waorodheshwe kwanza hao. Nitaanza basi na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. *Vote* 49, Programu 10, *Subvote 1001, item 250100* – Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya karibuni inawezekana kwamba, mpaka hivi leo limeibuka wimbi kubwa la wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambao walikuwa wanajichimbia visima vyao wenyewe ama kwa matumizi yao binafsi au kwa biashara. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, hakueleza chochote katika kitabu chake hiki kuhusu sekta hiyo, nataka maelezo ya ufafanuzi; je, Serikali inaitambua sekta hii ya uchimbaji wa visima vya binafsi na kama inaitambua inasaidia vipi kuhakikisha kwamba, maji hayo ni safi na salama kwa matumizi ya wanadamu?

Kama Serikali haiitambui sekta hii; kwa nini imekaa kimya muda wote huu ikijua kwamba zoezi hili lipo na kama maji hayachunguzwi inaweza kuwa ni chanzo cha maradhi mbalimbali yakiwemo cholera na maradhi kama hayo? Naomba maelezo. Asante.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu au nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Hemed Salim Khamis kama ifuatavyo: Serikali imeweka utaratibu maalum kwa uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali. Wananchi na taasisi mbalimbali, zinaruhusiwa kuchimba visima maeneo yale ambayo hakuna huduma ya maji, lakini inabidi wapate kwanza kibali kutoka Ofisi Bonde husika ili waweze kuchimba katika maeneo hayo. Baada ya kuchimba, maabara yetu ya Maji inabidi kuthibitisha ubora wa maji hayo kabla ya kuruhusu maji hayo yatumike kwa wananchi na hasa katika maeneo yale ambayo maji haya hayatumiki na mtu binafsi bali yanafanywa kama maji ya kibiashara.

Kwa hivyo, kama nilivyozungumza katika hotuba yangu ni kwamba, Serikali imefanya tathmini ya sampuli kadhaa za maji ikiwemo pamoja na sampuli kutoka visima hivi ambavyo vimechimbwa na watu binafsi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nitamwita Mheshimiwa Peter J. Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote No. 49,* Programu ya 10, *Subvote 1001,* Kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri. Hili ni

suala la Sera tu.  Ukurasa wa 33 wa Kitabu cha Waziri, anaongelea suala la Mradi Mkubwa wa Maji wa Mfuko wa *ASP EU Water Facility,* kwenye miji saba ikiwemo Mji wa Kigoma, Tabora na Dodoma.  Mimi la kwangu nilitaka kuuliza jambo moja tu kwamba, amesema mwaka huu 2006/2007, wamekuwa wanafanya huu mpango. Ninachotaka kujua ni kalenda ya mpango huu kwamba, tayari mpango umepangwa sasa ili watu wa Mji wa Kigoma na miji hii iliyotajwa, tuanze kujua sasa kalenda hii itaanza kutekelezwa lini, kwa sababu leo Waziri amesema maji mijini yameongezeka kwa asilimia 74 kwenda mpaka 78 lakini unaweza kuliambia Bunge Tukufu ongezeko hili halimo kwenye Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Sababu ziko *very clear,* Mji umeongezeka lakini pia umeme Kigoma hatuna sasa. Kwa hiyo, zile mashine haziwezi kupampu maji.  Hapa hakuna kilichoongezeka, kwa hiyo nataka kujua kwamba, programu hii itaanza kutekelezwa lini?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Peter J. Serukamba kama ifuatavyo:  Majadiliano haya ambayo tulikuwa tukifanya, Serikali ilikuwa ikifanya pamoja na washirika wa maendeleo. Ni katika jumla pia kama nilivyosema katika hotuba yangu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.  Kwa hiyo, tunaanza kutekeleza sasa rasmi Programu mpya ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.  Vipengele hivi vya kuandaa mipango vimo katika mradi huo, kwa maana hiyo ni kwamba tumeanza kazi hiyo na tutaendelea mwaka hadi mwaka, kwa kipindi cha muda mfupi mpaka mwaka 2010 na tutaendelea na programu hii mpaka mwaka 2025, kipindi ambacho tuna mtazamo wa kuhakikisha kwamba,wananchi wote Tanzania mijini na vijijini wamepata maji safi na salama.  *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi niko pale pale kwenye *Vote No. 49,* Programu ya 10, *Subvote 1001,* Kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuelewa zaidi nimetoa ushauri kuhusu hati chafu.  Sisi kama Wilaya ya Nzega, katika Majimbo ya Nzega na Bukene tumeshindwa kupata hela za maendeleo kwa ajili ya maji vijijini kwa sababu ya hati chafu.  Hili ni tatizo kwa sababu wanaopewa adhabu pale ni wananchi na wananchi wenyewe hawajui kabisa mambo ya mahesabu yanavyokwenda na yanavyokorogwa.

Kwa hiyo, nilikuwa nimetoa ushauri kwamba, wakati wanapozungumza, kwa kuwa wafadhili hao hao ndiyo wametuambia walipokuwa wanatusamehe katika madeni katika *HIPC* wamesema kwamba, fedha hizo tuzipeleke kwenye maendeleo ya jamii ambayo ni elimu, afya, barabara na maji.  Sasa wafadhili hao wakikaa nao vizuri Wizara, naamini kabisa wanaweza kutuachia wananchi wasipate adhabu hiyo, wapewe adhabu Watendaji ambao wanajua hayo mahesabu yanavyokwenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, hebu kaa.  Hapa unaleta suala mtambuka linalohusu Sera za Fedha, yaani misaada na masharti ya misaada. Waziri wa Maji, hawezi kujibu hilo.  Kwa hiyo, sioni kama linahusiana, itabidi tuendelee na wengine.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Hapa ninayo mawili, Mheshimiwa Mwenyekiti au siruhusiwi pia?

**MWENYEKITI:** La kwanza nimeliondoa. Sasa labda hilo la pili, nalo lilenge katika tunachokifanya hapa.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu katika Wizara hii, nilizungumzia maji ya Bukene, kama Makao Makuu ya Jimbo na Makao Makuu ya Kijiji kwamba, pale lipo bwawa lililochimbwa lakini halikuchimbwa katika hali ya kiutaalamu. Mashine ipo ya kupampu maji kufika katika matenki matatu ili kuhakikisha maji yanapatikana katika mji mdogo (Mji wa Bukene), ambao ni Makao Makuu. Sasa nitamwomba Waziri anijibu kwa nini siku zote hizi maji yanakosekana Bukene *simply because* wataalam hawawezi kwenda kusawazisha pale ili maji yale yaweze kuingia katika Mji wa Bukene?

**MWENYEKITI:** Sawa hilo Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ridhaa yako, nitoe ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Teddy L.Kasella-Bantu kama ifuatavyo: Miradi ya Maji katika Miji Midogo na katika vijiji, inatekelezwa na Halmashauri. Halmashauri ndiyo inayosimamia upatikanaji wa Mkandarasi na kufuatilia utekelezaji kamilifu.

Kwa hiyo, pale ambapo Halmashauri zinapata matatizo ya kiutalaamu, Wizara yangu inakubali kupokea malalamiko yale ili kuona namna gani ambavyo tutatoa ushauri wa kitaalamu. Lakini mpaka hivi sasa Wizarani sijapokea malalamiko hayo kutoka Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, niko tayari kutuma wataalamu, ambao watakuja kusaidiana na wataalamu wa Halmashauri na Mkandarasi ambaye wamemchagua ili kuweza kutatua tatizo hilo la maji katika Jimbo lako. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie *Vote 49*, Programu ya 10, *Subvote 1001* na *Subvote* ndogo zaidi 250100 – Mshahara wa Waziri. Sina shida kwa kweli na mshahara wa Waziri, naomba nitumie tu kupata ufafanuzi katika kipengele hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwanza, kwa majibu yake mazuri sana kuhusu suala la *Bi-Water* na *City Water* na nadhani wote tumeelewa nini kinaendelea. Kwa sasa tatizo kubwa lililoko mbele yetu ni nchi yetu kushinda kesi hii ili fedha nyingi alizotaja Waziri zisiweze kutukimbia na kwenda nje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sasa hakuna sababu ya kutafuta mchawi, sisi tujielekeze katika sura ya kulinda rasilimali yetu. Lakini sasa ninaomba kupata ufafanuzi mdogo tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nilieleza katika mchango wangu kwamba, tuna mashirika au taasisi za nje zilizojitolea kwenda kwenye kesi hizi kutusaidia. Hawa ni watu ambao

hawahitaji senti yetu hata moja, wanatumia fedha zao kama nilivyoeleza. *Centre for International Environment* wanatoka Toronto kwenda mpaka *The Hague* kusaidia sisi kwenye kesi hii.

Hawa wengine wanatoka Geneva wanaenda kutusaidia. Mashirika yetu ya *LIT* na *TGMP* wametuma mawakili wao toka Tanzania kwa fedha zao ili Serikali ya Tanzania tusishindwe katika kesi hii. Sasa nilitaka tu Waziri anisaidie, hawa wenzetu huko nyuma walipata matatizo makubwa ya kupata ushiriki kutoka Serikali yetu, kwa maana ya kupata *documents,* hawakushirikishwa kikamilifu. Kwa hiyo, hata wanapoingia sasa kwenye kesi ilikuwa ni kazi kubwa.

Lakini pia nimepitia *documents* na kama Mheshimiwa Waziri atazihitaji, kwa wakati wake nitaweza kumpatia. Wenzetu wamekuja na hoja mpya sasa kwa sababu hili suala liko Mahakamani siingii kwenye undani, lakini wameleta hoja mpya ambayo ushiriki wao unatusaidia katika kesi ile kwa maana ya kujenga hoja ya kuisaidia Tanzania. Sasa Waziri anisaidie, ana mkakati gani wa kuwashirikisha hawa kama Mawakili, marafiki kwa upande wa kwetu ili waki-*team up* na *team* ya Mawakili wa Serikali, waweze kujenga hoja za nguvu na tuweze kupata ushindi katika kesi hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme kwamba, Serikali inayashukuru sana mashirika haya ya *Centre for Sustainable Development, GMP* na mengine, ambayo yameshiriki kwa kiasi kikubwa katika kui-*support* Serikali katika mashauri haya mawili. *(Makofi)*

Mnajua kwamba, katika kuongelea shauri la *Bi-Water* dhidi ya Serikali mwezi wa nne, baadhi ya mashirika haya yalishindwa kushiriki kikamilifu katika shauri hili kwa sababu ya vipengele vya sheria. Kwa hiyo, walikosa nafasi ya kuweza kushiriki kui-*support* Serikali. Tulisikitika kwa hilo. Lakini vipengele vya sheria ni vipengele vya sheria, hatuna uwezo wowote wa kuweza kuvitengua hivyo. Sasa kwamba; je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuendelea kuwashirikisha? Naweza kusema kwamba, hapa tulipofikia tumefikia mwisho, kabla sijaingia Bungeni nimepata taarifa ya mdomo na nilisita kuitamka kabla kwa sababu barua yenyewe sijaiona, lakini nimeelezwa na Maafisa wangu kwamba kesi ya *City Water* dhidi ya *DAWASA*, tumeshinda. *(Makofi)*

Kwa sababu nilipata taarifa kwa mdomo, *from reliable sources,* kwa hiyo, naona sasa bora niseme na pia shauri lililobaki la *Bi-Water* dhidi ya Serikali hili limefikia mwisho, linangoja sasa maamuzi, hakuna suala lingine baada ya hapo. Asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *Vote 49*, Programu ya 10, *Subvote 1001* na *Sub-Vote* ndogo 250100. Kwanza na mimi nataka

kuungana na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri jinsi alivyojibu swali ambalo lilikuwa nyeti. *(Makofi)*

Ni matumaini yangu huu utakuwa ni mfano kwamba, tunapouliza maswali ya Kitaifa tunachotaka ni ufafanuzi tu kwa sababu tunataka uwazi katika matumizi ya fedha za umma. Baada ya hapo katika mchango wangu, nilizungumzia juu dhana ya mabwawa kujengwa halafu yanaachwa bila miundombinu ya kuwawezesha watu kutumia hayo maji au mifugo kujengewa visima ambavyo mifugo inaweza ikanywea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano huu uko kule nyumbani kwetu Mwalushu na pia mfano mkubwa watu wa Bariadi uko pale Bariadi Mjini, tumekuwa na bwawa kwa zaidi ya miaka kumi lakini mpaka leo hatuna uwezo wa kutumia hayo maji. Kwa hiyo, nataka maelezo kwamba dhana ya namna hii inapoteza fedha, inatumia fedha nyingi lakini hakuna chochote ambacho kinawafaidisha wananchi. Kwa hiyo, nataka maelezo juu ya hilo.

Jambo lingine ni juu ya Lambo la Habia ambalo pia Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 30 amelizungumzia kwamba, utekelezaji umeanza. Sasa leo hii nimepiga simu Bariadi kwanza, naambiwa hakuna fidia ambayo imelipwa kwa wananchi. Najua kuna dhana ya nguvu mara nyingine lakini kwa miradi ya maji ni hatari sana kutumia dhana ya nguvu kuweza kuhamisha watu. Mimi napenda nipate maelezo, Waziri atafanya nini kuhakikisha kwamba, kuna fidia ambayo inalipwa kwa wananchi? Pia kuna Bwawa la Nanga, ambalo kwa muda wa miaka kumi tunazungumza kwamba, bwawa hilo hatulitumii kwa sababu mvua zinakuja halafu maji yanatoka, jambo hili ni la ufundi. Sasa ni mpaka lini tutaendelea kudai Serikali ilete wahandisi ili tuhakikishe kwamba, watu wa Nanga wanakuwa na maji na fedha iliyotumika kuchimba hilo bwawa kweli inawapa faida wananchi ambayo ni mali yao. Naomba ufafanuzi kwa hayo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako, nitoe ufafanuzi wa hoja mbili za Mheshimiwa John M. Cheyo kama ifuatavyo: Moja kuhusu mabwawa ambayo yamejengwa bila miundombinu ya kunyweshea maji mifugo na sehemu ya kuchota maji kwa matumizi ya kijamii ya binadamu.

Nikiri tu kwamba, hayo ni mapungufu katika *design* na Wizara yangu imeona hivyo, siyo Wizara yangu lakini pamoja na Wizara ya Mifugo ambayo kwa ushirikiano katika kusanifu miradi, tumeweka Mkakati Maalum, ambao tunahakikisha kwamba kwanza kunakuwa na uwiano wa ujenzi wa mabwawa katika Wizara hizi mbili zote za Serikali moja. Katika mabwawa hayo, usanifu utahakikisha kwamba, usanifu unaofuatia unajenga miundombinu sahihi na inayofaa kwa ajili ya matumizi ya maji ya binadamu na maji ya matumizi ya mifugo.

Kuhusu lambo la Habia kwamba watu hawajalipwa fidia ni kwamba, haijaanza kazi. Yeye Mheshimiwa John M. Cheyo, amepiga simu leo kwa hiyo ana habari za leo, lakini mimi nina taarifa za Wizara zinazosema kwamba, kazi imeanza. Kwa hilo nadhani

nisingependa kubishana naye. Tutalifuatilia na kuweza kuhakikisha kwamba kazi inaanza mapema. *(Makofi)*

Lakini niseme tu kiuhakika, Serikali kamwe haitatumia nguvu, kuwahamisha watu bila ya kufuata sheria na taratibu. Serikali hii ni Serikali ambayo imejikita katika kufuata kanuni, sheria na taratibu zilizopo. Kwa hiyo, wananchi wa eneo hilo itakapobidi kazi ifanywe kabla ya fidia, basi tutakuwa na makubaliano kamili kama ambavyo tulikuwa na makubaliano katika maeneo mengine. Baada ya kukosa hela mapema, watu walilipwa baadaye lakini watu wakaweza kuhama kwa hiari yao baada ya makubaliano ya uhakika na kuhusu Bwawa la Nanga limeharibika, naomba kusema kwamba, hii ni kazi ambayo kama nilivyozungumza, kisera na kwa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, hii ni kazi ambayo kama nilivyozungumza, Kisera na kwa Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ni kazi ambayo Halmashauri iitengee fedha na iikamilishe kwa sababu hivi karibuni tu tumepeleka pesa nyingi na tutaendelea kufanya hivyo. Madaraka sasa yapo kwa wananchi wenyewe kupitia Halmashauri zao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Waziri. Niseme tu, Waheshimiwa Wabunge wengi mnaosimama bado mnatumia kitu naweza kusema ni uvivu tu, kwa sababu mengi mnayoyasema yapo katika Kitabu cha Nne, lakini wote mnasema kushika mshahara wa Waziri, halafu mnataja mradi ambao uko Kitabu cha Nne. Kwa leo kwa sababu nimeendelea kuruhusu basi tena, lakini huruma yangu inaanza kufikia mwisho. Nadhani katika kasma nyingine hizo, tukifika *vote* nyingine itabidi turudi kwenye Kanuni, hatuwezi kila mtu anasimama tu watu kama 20, Mshahara wa Waziri halafu anataja mradi mmoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote* 49, *Program 10, Subvote 1001* na Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu ambao sijasikia majibu, niligusia juu ya matatizo ambayo mwaka jana vilevile wakati wa vifungu nilitaka maelezo na nilijibiwa. Sasa sina hakika kama Serikali inafuatilia vizuri haya tunayoyauliza hapa kwenye vifungu, sina hakika lakini leo nimerudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye Bonde ambalo linaitwa Bonde la Maisaka Mjini Babati. Katika lile Bonde wananchi wamewekeza mali, wamejenga nyumba, lakini Serikali iliona kwamba ni kama sehemu ya vyanzo vya maji na kuna visima pale. Lakini ikaonekana kwamba fidia inaweza kuwa kubwa sana na pengine vyanzo katika eneo hilo kwa eneo lililotengwa pengine maji siyo kwa kiwango hicho ambacho kinafikiriwa.

Sasa niliomba ufafanuzi mwaka jana na Mheshimiwa Waziri akiwa Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, alinijibu kwamba, jambo hilo litaangaliwa ili wananchi hawa kama kuna uwezo, najua fidia ile ni kubwa, basi Serikali iwafidie kama hakuna basi eneo

lililotengwa liangaliwe, lile ambalo lina vyanzo vya maji waishie pale ili Serikali isiingie kwenye gharama kubwa sana ya kufidia wananchi.  Nimeliandika lakini sijaona majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa pili ni kwamba, nilizungumza habari ya vyanzo vipya ya maji na mwaka jana vilevile nilisema kuna vyanzo katika eneo la Singe, yaani Kijiji cha Singe, maeneo ya Nakwa na maeneo mengine ambayo niliyazungumzia na leo nimerudia tena kueleza katika mchango wangu, lakini sijasikia jibu mahali popote, maana maeneo ambayo nimetaja ya Singe na Nakwa ndiyo yenye maji.

Napenda nipate ufafanuzi, Serikali sasa ina mpango gani au niseme tena, wakati kama huu hebu naomba nipate ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la kwanza, nimwombe Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', aniambie fidia kwa eneo gani mahususi, sikuweza kulipata eneo hasa ambalo alizungumza kwamba linahitaji fidia.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni eneo la Bonde la Maisaka. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, walikuja kwenye ziara na tukazungumza kidogo, ni Bonde la Maisaka.

**MWENYEKITI:** Bonde hili lipo mjini?

**MHE. OMAR S. KWAANGW' :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo lipo Babati Mjini.

**WAZIRI WA MAJI :** Mheshimiwa Mwenyekiti,  naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu fidia ya eneo la chanzo cha Maisaka kwa ajili ya maji  Mjini Babati ni kweli kwamba, fidia ya eneo lile ni kubwa na Serikali katika kutafuta hela ilipoona kwamba haitamudu kulipa fidia katika kiasi hicho, kama nakumbuka sawasawa ni zaidi ya shilingi bilioni 80.  Hela nyingi sana ambapo ilikuwa vigumu sana kuzipata na baada ya kupita muda mrefu wa kukosa pesa hizo, basi Serikali iliamua kupunguza ukubwa wa eneo hilo ili tuweze kupata fedha ili tuweze kupata fidia ambayo Serikali itaimudu kulipa.

Niseme kwamba, imechangiwa pia na Wananchi wa Babati kwamba eneo tajwa, ujenzi wa miundombinu ukaenda kwa kasi kiasi kwamba, tathmini ile ikapanda juu sana na kuzidi uwezo wa Serikali kupata pesa hizo. .Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kumbukumbu zangu zinaniambia kwamba, tayari tumetengea pesa Mamlaka ya Babati kwa ajili ya fidia kwa eneo dogo, siyo lile eneo kubwa ambalo tulilihitaji mwanzoni.  Kwa maana hiyo, kutakuwa na athari hata ya upatikanaji wa maji kwa Mji wa Babati, kwa sababu chanzo ni kidogo zaidi kuliko tulivyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii nyingine ya Singe na Nakwa, naomba niseme tu kwamba, nimepokea na nitaifanyia kazi, kwa sababu sina majibu ya moja kwa moja sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Waziri anasema hana majibu ataifanyia kazi, nakuomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nimekumbusha mara kwa mara kwamba, Kamati ya Matumizi maana yake siyo kudai upate unachokihitaji. Ukishapata ufafanuzi, hata ufafanuzi ukisema haipo fedha ni kwamba haipo fedha, ndiyo jibu lenyewe. Sasa ukisema tu itafutwe na tumepitisha bajeti, sasa sijui itakuwaje! Nakupa useme kwa dakika moja kama kweli kuna hoja ya ziada hapo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala si fedha isipokuwa sasa je, Serikali iko tayari kuiambia Halmashauri ya Mji kwamba, lile eneo ambalo lilikuwa kubwa sasa basi lipunguzwe libaki kwenye lile ili wananchi hawa kwenye maeneo mengine ambayo hayahitajiki waendelee na shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**WAZIRI WA MAJI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya hivyo hivi karibuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU :** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa sana Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', juu ya tatizo la maji katika Mji Mpya wa Babati, lakini majukumu mengine kama alivyoeleza Waziri, yatafanywa na Serikali Kuu na mengine yatafanywa na Halmashauri. Kama hilo analolisema la fidia na la eneo kutengwa ni kazi ya Halmashauri kuamua ni eneo gani lichukuliwe na eneo gani libaki. Tuwaachie Halmashauri kufanya wajibu wao na Serikali Kuu ifanye wajibu wake. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie *Vote Number* 49, *Program 10, Sub-section 1001*, Kifungu kidogo cha 250100, lakini sina mgogoro na mshahara wa Waziri, bali nataka ufafanuzi kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia juu ya mabwawa, kwetu hakuna kabisa na ni mgogoro mkubwa kati ya wafugaji na wakulima, labda anaweza kunifafanulia hapa tufanya nini kwani Morogoro nzima hakuna Programu ya Mabwawa?

La pili, naomba nimweleweshe Mheshimiwa wa Maji, wakati ule aliyekuwepo alishakwenda Kidunda na akaonana nao ingawa Bwawa linaitwa la Kidunda, lakini waathirika wakubwa wapo kwenye Kata ya Selembala; kwenye Vijiji vya Vidwali, Kibulumo, Gwilachini, Gwilajuu na Kiganila.

Je, Mheshimiwa Waziri, safari yako ungekuwa radhi kupitia Ubena, Ngerengere hadi Kiganila kwenye Kata ya Selembala na mimi nikakupokea nyumbani kwangu ili

uweze kuzungumza na wananchi hawa na uko radhi kulala kule ingawa hakuna umeme? Mheshimiwa Mwenyekiti, Asante sana.

**WAZIRI WA MAJI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kwa hoja mbili za Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, kama ifuatavyo:-

La kwanza, kuhusu Programu za Mabwawa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutoa ufafanuzi. Naomba nirudie hapohapo kama alivyosema Waziri Mkuu, uibuaji wa Miradi hii ya Maji na aina za teknolojia ambazo zitatumika kwa Miradi Maalum ya Maji, itafanywa au katika ngazi za Halmashauri.

Halmashauri inayosimamia Miradi ya Vijijini na pia miradi mikubwa mikubwa. Tutakapopanga na kuiibua basi kazi ya Serikali itakuwa kutafuta hela kwa ajili ya miradi hiyo. Tumeondokana sasa na mradi mmoja mmoja, Serikali moja kwa moja kushughulika nayo, imeingia katika uibuaji wa miradi kwa wananchi wenyewe.

Hoja ya pili ya ukaribisho, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha ni kaka yangu. Nafurahi sana, tena afadhali safari hii hakumhitaji Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo, niko tayari kuongozana naye katika vijiji vyote ambavyo amevitaja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, ili binadamu alale anachohitaji ni kitanda au godoro na siyo umeme na hata kule ambapo kuna umeme ninaarifiwa kwamba, wanapotaka kulala wanauzima ule umeme. *(Kicheko)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe uliposema kwamba, tunang'ang'ania hii *vote* ni kweli miradi yote iko kwenye Kitabu cha Nne. Tatizo ni kwamba, muda wa *guillotine* ukifika ndiyo hatufiki Kitabu cha Nne. Kwa hiyo, ndiyo maana tunakimbilia hapa, lakini tukikubaliana kwamba, ukifika muda wa *guillotine* tuongeze muda tutasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi niko katika hiyo *Vote 49*, *Program 10* na ninapenda niulize maswali matatu.

**MWENYEKITI:** Utamaduni wetu Mheshimiwa Michael L. Laizer ni kuibua maswali ya ufafanuzi mawili na siyo matatu au zaidi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Ninataka kuuliza Miradi ya *ADB*, ambayo inaendelea nchini lakini yote imesimama haijamalizika, wala hatujui kwa nini hiyo Miradi haiendelei.

Jambo lingine ni Miradi ya *World Bank*. Wakati wa uchaguzi tulizunguka sana kuwaeleza wananchi kwamba, tuna miradi ya *World Bank* vijiji kumi kwa kila Wilaya lakini umepita muda mrefu sana, tunaulizwa na wananchi kitu kinachoendelea na sitegemei kama, kuna Mbunge anayeweza akajibu. Naomba tupewe majibu ili wananchi yale majibu madogo ambayo hayaridhishi tunayowaambia, leo Waziri wa Maji atoe majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, katika Jimbo langu ambalo nadhani katika Tanzania nzima, ndiyo lenye shida ya maji, wananunua debe moja kwa shilingi 800. Pia kuna bwawa lililochimbwa wakati Waziri Mkuu, alipokuwa Waziri wa Maji na mpaka sasa halikuendelea na lipo kwenye Mradi wa *quick wins*. Naomba Waziri anieleze kama ataweza kwenye fedha hizo zilizopatikana za *quick wins*, kutoa fedha zote ili Mradi huo umalizike?

**MWENYEKITI :** Hujakitaja kijiji.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER :** Kijiji kinaitwa Mundara. Nadhani Ndugu Sayi anakifahamu ni mtaalamu anafahamu vijiji vyote.

**MWENYEKITI:** Ndugu Sayi ni Naibu Katibu Mkuu, lakini yeye hayupo hapa kujibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba kutoa maelezo au ufafanuzi kwa hoja tatu za Mheshimiwa Michael L. Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya *ADB* ni miradi ambayo ina uchangiaji kutoka Serikalini. Kuna Miradi ambayo inakwenda vizuri na kuna miradi ambayo mpaka sasa ilikwama kidogo, kwa sababu ya pesa ya uchangiaji kutoka Serikalini. Tumefanya maongezi na *ADB* na mimi binafsi nimeongea na Mkurugenzi Mkuu wa *ADB*, kuweza kutukubalia kutoa vifungu vya hela kutoka *ADB,* pamoja na kwamba, tumechelewa kuweka vifungu vya hela za Serikali, kwa sababu tunatarajia katika mwaka huu wa fedha, kuweza kuweka pesa hizo. *ADB* wametukubalia kwa maana hiyo ni kwamba, Miradi ya *ADB* itaendelea bila matatizo. Lakini naomba nitoe ufafanuzi pia katika Miradi hii ya *World Bank*. Tulipojadiliana na wahisani mbalimbali au washirika wa maendeleo, tulikuwa na mikataba ambayo inabidi kufuata taratibu mbalimbali na taratibu ambazo zimechukua muda na mpaka hivi sasa pesa hizo hazijatoka. Kwa hiyo, hatuna njia nyingine zaidi ya kuvuta subira ili tuweze kupata pesa hizo, tufanye miradi yetu ya maji kwa vijijini vile kumi.

Lakini katika mradi huu kuna pesa ambazo zimeshatoka tayari na hizi ni pesa ambazo tumeziita pesa za miradi midogo midogo, ambayo tumeiita *quick wins*. Tumezitangaza hizo pesa zimetoka kwa kila Halmashauri na kwa maana hiyo ni kwamba, pamoja na kuwa hizo za vijiji kumi hazijatoka, lakini walau kifungu kimoja cha *quick wins* kimetoka na pesa ambazo zimekwenda Longido kwa ajili ya Miradi ya *quick wins* ni kwa ajili ya matumizi ya Wilaya hiyo katika Halmashauri. Kwa hiyo, Miradi hiyo ambayo mmeipangia na kama Mheshimiwa Michael L. Laizer alivyosema kwamba, bwala la Kijiji cha Mundaha liko katika *quick wins,* maana yake sasa ni kuitekeleza *quick wins* hiyo lakini Halmashauri hiyo ikipenda kurekebisha, basi sisi tutahitaji taarifa ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nihamie upande wa kulia hapa, Mheshimiwa George M. Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Vote 49*, Programu ya 10, Subvote 1001, Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia kwa maandishi, ninachotaka ni ufafanuzi tu. Tuna mpango wa kuboresha huduma ya maji katika Miji Midogo tisa. Sasa kwa kuwa upembuzi yakinifu umechukua muda mrefu sana, karibu miaka miwili na sasa wameandaa usanifu, pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni. Je, huu usanifu pamoja na kuandaa makabrasha, hautachukua muda mrefu kwa sababu Mji wa Mpwapwa una matatizo makubwa sana ya maji? Je, utakamilika lini huu usanifu na kuandaa haya makabrasha ya zabuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Miradi hii ya miji tisa na Mpwapwa ikiwa ni mojawapo, usanifu wa kina unatarajia umalizike katika kipindi kifupi mwaka huu, kwa sababu programu nzima imepangwa na Serikali imeamua kuhakikisha kwamba, inamalizika mwishoni mwa mwaka 2008. Kwa hiyo, ili ujenzi umalizike ifikapo mwisho wa mwaka 2008, maana yake usanifu wa kina lazima umalizike katika kipindi hiki kifupi kijacho. Siwezi kusema *exactly* itakuwa ni muda gani, wakati nakuja Bungeni sikupitia kipengele hicho. Kwa hiyo, ninaomba tu tutakapomaliza Bunge, Mheshimiwa George M. Lubeleje, niweze kumpa taarifa kamili ya lini tunatarajia kumaliza kazi hiyo.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 49,* Programu ya 10, *Subvote* 1001 na Kasma ya 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo, wakati nilipokuwa nachangia nilieleza juu ya Mradi wa Ntomoko. Kwanza, namshukuru sana Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na kukubaliana na mimi kwamba, mradi ule umekufa kabisa. Alipokuwa anajibu sasa hivi amesema hata vile vijiji ambavyo alisema asubuhi kwamba, kuna huduma ya maji inapatikana, amekiri kwamba huduma haipo. Kwa hiyo, ukweli wenyewe ni kwamba, Mradi huo umekufa, kwa hiyo, napenda nimshukuru kwa kukiri.

Lakini napenda nimwulize hivi huyu mtaalamu aliyewapa jibu la namna hii, mtamchukulia hatua gani kwa kuipotosha Serikali? Hiyo ni moja ambayo nataka maelezo.

La pili, Serikali itachukua hatua gani kwa vijiji hivi 17 viweze angalau kupata maji, kwa sababu hatuna chanzo kingine cha maji? Waziri amesema kwamba, kuna shilingi milioni 150 zitatengwa na Halmashauri, hizo hazitapatikana leo; hao watu

watatumia maji kutoka wapi wakisubiri shilingi milioni 150? Naomba maelezo na hasa naomba maelezo kutoka Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ambayo ina uchungu na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja za Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Kwanza, *share* na Mheshimiwa Mbunge, masikitiko yake kuhusu ukosefu wa maji kwa wanavijiji 17, ni simanzi kwa Serikali, kwa sababu tunafahamu kwamba, juhudi ambayo tunaiweka ni kwa ajili ya kuondosha matatizo haya. Katika kila eneo ambalo kuna tatizo la maji, huo ni mzigo ambao tunaubeba kwa simanzi kubwa na kwa nguvu kubwa kuhakikisha kwamba, tunafikia malengo ambayo Serikali imejiwekea hadi mwaka 2010.

Kuhusu taarifa ambayo haikuwa sahihi kwa mtumishi ambaye ameitoa, hiyo niseme kwamba, tutachukua taratibu za kiutumishi ndani ya Wizara ili kuhakikisha kwamba, hilo jambo halitokei tena na linachukuliwa hatua muhimu.

Lakini kuhusu nini Serikali itafanya, Halmashauri imetenga fedha kwa sababu Serikali Kuu imeitengea pesa na pesa hizo ndiyo zitakuwa ni kianzio cha kusanifu Mradi ambao utaondosha kero ya upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wanavijiji hao wa vijiji 17. Kuna uwezekano mkubwa kwamba, pesa hizo hazitatosha kwa kipindi hiki. Serikali itafuatilia kujua kwa uhakika, kijiji kipi kimefanikiwa na kipi hakikufanikiwa ili tuweze kufuatilia mwaka hadi mwaka na ndani ya kipindi cha uongozi huu na ndani ya kipindi cha Serikali hii mwaka 2010.

Sisemi kwamba, tutangoja mwaka 2010, bali ninasema ndani ya kipindi cha Serikali hii, ihakikishe kwamba, tatizo kwa wananchi wa vijiji hivyo 17 Kondoa Kusini, limeondoka ama sivyo limepungua kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na Mheshimiwa Waziri, kusikitika sana juu ya vijiji 17, Mradi wao wa Maji kufa. Sote tunaokumbuka historia ya Mradi huu ulioanzishwa na Baba wa Taifa, alifanya kazi kubwa sana.

Ninapenda kujiunga na Waziri kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na kuwahakikishia wanavijiji hao wa vijiji hivyo 17 kwamba, tutafanya kila liwezekanalo ndani ya uwezo wetu Serikali Kuu, Serikali ya Mkoa na Halmashauri, kuhakikisha kwamba, Miradi hiyo inafufuliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mgana I. Msindai karibu. Huna haja ya kurudia, najua wote ninyi ni hiyo hiyo *Subvote* 1001, tuokoe muda sasa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mimi nilichangia kwa maandishi na ninashukuru aliposimama Naibu Waziri alinitaja na Waziri mwenyewe alinitaja, lakini hawakusema watasaidia vipi vijiji ambavyo nilivitaja kwenye mchango wangu wa maandishi. Vijiji hivi ni Malela, Igonia, Kipamba, Wamzai, Mgimba na Kinamkaba, wamekuwa wakinisaidia kila mwaka kwenye *quick wins* lakini sasa mwaka huu sijasikia wavitaje hivi vijiji. Mimi naomba wanifafanulie tu kama vitakuwepo kwenye mpango basi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba nitoe ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kwamba, hatua ambayo sasa hivi tuko nayo ya Kisera ni kwamba, uchaguzi wa Miradi ya Vijiji ni jukumu la Halmashauri za Wilaya husika. Halmashauri mbalimbali zinachagua kwamba, miradi gani na vijiji gani ambavyo tutavitekelezea miradi ya maji kwa mwaka huu ama kwa mwaka ujao au kwa kipindi kingine. Iramba Mashariki wamefanya hivyo, tayari wamechagua vijiji kumi ambavyo vitaingia katika Miradi ya Maji chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Lakini pia wamechagua miradi midogo midogo ya *quick wins,* hiyo ndiyo ambayo inaendelea nayo, pesa zimetoka sasa hivi kwa *quick wins* na zitatoka pia za Miradi ya vijiji kumi. Kwa hiyo, vijiji vyovyote vikiwemo Malela na vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, basi vile ambavyo havikuchaguliwa safari hii, waviibue katika awamu inayofuata ili viweze kupata fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kifungu hicho hicho. Nimechangia kwa maandishi, katika mchango wangu niliulizia ahadi za Mheshimiwa Waziri wa Maji aliyepita, kuhusu Bwala la Katoro. Mheshimiwa Naibu Waziri, ameshafika pale na nimekuwa nikifuatilia na nimeona matangazo ya mabwawa mengine lakini pale sijaona kitu. Sasa hivi Katoro watu wananunua maji kwa bei kubwa sana. Napenda kufahamu.

La pili, Naibu Waziri, amejibu vizuri sana kuhusu Mradi wa Maji wa Nyakagomba, ambao unanipa wasiwasi ulianza mwaka 1976 na mimi sasa huu mwaka wa saba, kila mwaka naulizia, ingawa mwaka huu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, sasa ufumbuzi wake umepatikana. Naomba nihakikishiwe kabisa kama mwaka kesho sitauliza tena suala la Mradi huo kwa sababu hata wananchi wananishangaa kila mwaka naulizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Bwawa la Katoro ni moja kati ya mabwawa ambayo yametengewa fedha na yamekwishafanyiwa usanifu na tathmini ya wazabuni imekamilika na Wakandarasi kuteuliwa. Kwa hiyo, tunatarajia hivi karibuni kazi itaanza katika bwawa hilo. Kwa sababu taratibu zile za uteuzi wa mkandarasi zimeshakamilika, Bwawa la Nyakagomba limeingizwa kwenye miradi kumi ya vijiji, kwa hiyo, nalo litatengewa fedha na kuweza kutekelezwa katika kipindi hiki cha mwaka 2007/2008.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati Naibu Waziri wa Maji, akijibu hoja mbalimbali alisema Mradi wa Misungwi uliokuwa utekelezwe na *MCC* sasa umetengewa shilingi milioni 400 na Serikali yenyewe. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa nielezwe sasa hizo shilingi milioni 400 zitafanya kazi zipi, hasa ikizingatiwa upembuzi yakinifu ulionesha kwamba, huo mradi ungehitaji shilingi bilioni 15; hizo shilingi milioni 400 zitafanya kazi zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ridhaa yako, kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majumuisho kwamba, kuna Miji sita ambayo tumeiombea fedha *MCC* na kwa kutaka kurahisisha kazi na kuhakikisha kwamba tunafanikisha pale, zile fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti amezizungumzia, zitakapoweza kupatikana, basi maandalizi ya mwanzo angalau yaweze kufanywa katika Miradi ya Miji hiyo sita ambayo tumeiombea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo za maandalizi ya mradi, pamoja na usanifu, hakuna ujenzi ndani yake. Tutakapopata fedha, maana yake ni kwamba, tutaweza kuanza sasa, hatutaanza moja kwa moja kama vile ambavyo ingekuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ili tumalize nisimwache hata mmoja, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro na Mheshimiwa Charles N. Keenja, kila mmoja dakika moja na nusu hivi.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninazungumzia *Vote* hiyo hiyo kwa sababu Waziri ndiye mwenye dhamana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, rudi kwenye hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu kwa maandishi, nilizungumzia upatikanaji wa maji Mji wa Himo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Himo una wakazi wengi ni Mji wa Utalii na ni Mji wa mpakani na wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, watapata maji. Mwezi ujao Mheshimiwa Rais atatembelea kule na nina uhakika katika moja ya kero ambayo ataulizwa ni upatikanaji wa maji katika Mji wa Himo. Naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni lini upatikanaji wa maji safi na salama katika Mji wa Himo utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Mheshimiwa Charles Keenja ni wa mwisho.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kwangu ni mafupi sana. Katika ukurasa wa 41, *paragraph* ya 70, Mheshimiwa Waziri amezungumzia aidha, maandalizi ya mpango mpya yatafanyika. Sasa nilikuwa nataka kujua mpango huo mpya unaoandaliwa ni mpya ama ni ile ile iliyopo, ambayo sasa hivi inaendelea kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba, ninaipongeza sana Wizara hii na pia naipongeza *DAWASCO* kwa kazi nzuri sana wanayoifanya pale Dar es Salaam. Inaonesha kwamba, Watanzania tukipewa nafasi tunaweza na kwa kweli wameweza. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile hili la Bwawa la Kidunda, inaelekea matatizo ya Kihansi yanaliingilia bwawa hilo pia. Sasa watakapokuwa wanafanya hayo, naomba Wananchi wa Dar es Salaam wawekwe upande mmoja na vyura upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana kwa hayo mawili.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja hizo mbili kutoka kwa Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro na Mheshimiwa Charles N. Keenja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mji wa Himo, ahadi ile aliyotoa Mheshimiwa Rais ni ahadi za Serikali na Wizara yangu itahakikisha kwamba, tunazitekeleza kwa nguvu na kwa kasi inayowezekana. Sasa hivi sijaweza kupitia mpango ambao umekamilika kwa ajili ya Mji wa Himo, lakini nitatoa majibu kwa Mheshimiwa Mbunge, mara tu baada ya Bunge hili kuahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelekezo ambayo Mheshimiwa Charles N. Keenja ametupa, tutayazingatia na tutahakikisha kwamba, katika majadiliano yetu na *MCC* na Wafadhili wengine, basi tutahakikisha mahitaji ya maji ya wananchi yanaweza kutimizwa pamoja na kuhifadhi mazingira yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa zimebaki zile dakika kumi, ambazo kwa Kanuni ya 81(6), inatubidi tupitishe kwa fungu zima. Katibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … … … … … ... Sh.978,499,900
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … … … … …... Sh 936,084,300
Kif. 1004 – *Information, Educat. Communication* … ... Sh. 163,453,600
Kif. 1005 – *Legal Unit* … … … … … … … .... Sh. 1,910,374,200
Kif. 1006 – *Procurement Management* … … … … ... Sh. 558,886,000
Kif. 1007 – *Management Information System* … … … Sh. 152,942,600
Kif. 1008 – *Internal Audit Unit* … … … … … … … Sh. 173,491,600
Kif. 2001 – *Water Resource Assessment*
*and Exploration* … ... ... .... .... .... .... .... .... Sh. 1,685,044,700
Kif. 2002 – *Central Stores* … … … … … … .... ...Sh.320,751,800
Kif. 2003 – *Water Laboratory* … … … … … … … Sh. 528,254,400
Kif. 3001 – *Urban Water Supply and Sewerage* … … Sh. 1,077,061,700
Kif. 4001 – *Rural Water Supply* … … … … … … Sh. 2,150,227,700
Kif. 5001 – *Water Resource Institute* … … … … … Sh. 601,574,600
Kif. 6001 – *Drilling* … … … … … … … … ...... Sh. 154,887,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … … … Sh.15,474,294,000
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … … … … … Sh.5,593,354,000
Kif. 2001 – *Water Resource Assessment*
*and Exploration* … .... .... .... ..... ..... ..... ..... Sh.18,062,550,000
Kif. 2003 – *Water Laboratory* … … … … … .... ...Sh.2,456,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Urban Water Supply and Sewerage* … … Sh.119,966,007,300
Kif. 4001 – *Rural Water Supply* … … … … … .... Sh.54,671,367,000
Kif. 5001 – *Water Resource Institute* … … … … … …Sh.1,494,400,000
Kif. 6001 – *Drilling* … … … … … … ... ... ..... .Sh. 7,272,780,300
Kif. 8001 – *Animal Production* … … … … … ..... ...... ..... ....Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati*

*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Bajeti ya Wizara yangu Fungu 49 kwa mwaka 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba, binafsi nimevutiwa sana na mwenendo wa Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa si kwamba, wengine hawafanyi vizuri sana, lakini nadhani kuna jambo hili la kujibu hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri ameonesha heshima kubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Natumaini utamaduni huu utaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ila tu kwa bahati mbaya ni kwamba, Spika, hawezi kutetea Jimbo lake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akumbuke, Urambo hakuna maji na hata kwa jirani yangu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hivyo hivyo hakuna maji. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, atawasilisha hotuba ya Makadirio, atakayefuatia kesho kutwa ni Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge, ambao watasafiri kwenye *weekend* hii, mkumbuke kwamba, tarehe 23 Julai, 2007 - Jumatatu, itakuwa ni zamu ya Wizara ya Usalama wa Uraia. Nimeona niwataje ili mjue na muweze kupanga ni Wizara gani mtachangia na kadhalika. Nawatakia usiku mwema. Naomba kutamka sasa kwamba, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*